

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,**

**BURA CONSTITUENCY, TANA RIVER DISTRICT, AT**

**MADOGO SOCIAL HALL**

**ON**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS AT BURA MADOGO CONSTITUENCY HELD AT  
MADOGO SOCIAL HALL ON 08.06.02**

**Present:**

Com. Prof. Okoth-Ogendo  
Com. Bishop Bernard Njoroge  
Com. Abubakar Zein

**Secretariat in Attendance**

Fatuma J. Isaa – Programme Officer  
Walter Mayaka – Assistant Programme Officer  
Diana Kivuti – Verbatim Recorder  
Omar Abdala Dhadho – Co-ordinator.

**Absent:**

Com. Dr. Maranga Charles.

The meeting was called to order at 10:00 am with Com: Zein in the chair.

**Com: Zein:** Habari zenu, ningependa kuchukua fursa hii kutangaza kuwa kikao rasmi cha Tume ya Kurekebisha Katiba kwa minajili ya kutoa maoni ya Wanakenya ya kurekebisha Katiba yetu. Jambo la pili ningependa kumuomba mshiriki wetu Bwana Dhadho atuongoze katika sehemu inayofuata.

**Bwana Dhadho:** Asante sana Commissioner Zein, Commissioners ambao wako hapa, Prof. Okoth-Ogendo, na Bishop Muingai Njoroge, Programme Officer Fatuma na Assistant Programme Officer Walter, kutoka kwa Tume, viongozi wa tabaka mbalimbali ambao wamehudhuria mkutano wa leo, Councillors, viongozi kutoka utawala wa mikoa, mabibi na mabwana, hamjambo. Mimi majina kamili naitwa Omar Abadala Dhadho, ndiye Co-ordinator wa Tume ya Mageuzi ya Katiba ya Kenya wilaya ya Tana River. Ningependa kuwajulisha Commissioners ambao wako hapa pamoja na sisi kwamba, hapa tulipokaa ingawa ni karibu na Garissa lakini ni wilaya ya Tana River na hapa tuko katika Constituency ya Bura na wilaya nzima tuko na Constituencies tatu, ambapo zingine mbili ni sehemu ya wakilishi bungeni ya Galole ambao pia inahusu headquarter ya wilaya hii ya Tana River. Tuko pia na sehemu ya wakilishi bungeni ya Garsen ambayo inaenda mpaka baharini. Kwa hivyo hii yote ni wilaya yetu ya Tana River na wenyeji wa hapa kuna kabila tofauti tofauti, tuko na Malakote, tuko na Waorma, tuko na Munyayaya, tuko pia na Wardhei. Hizi kabila zote na Wata pia, ni wakaazi wa eneo hili la Bura Constituency. Kwa hivyo tukipata matatizo ya utafsiri kwa wale ambao hawaimudu lugha ya Kiswahili tumeweka watu tayari ambao wataweza kutusaidia kutafsiri.

Kwa hivyo ningependa kuchukua nafasi hii pia kueleza ya kwamba kamati ya sehemu ya wakilishi bungeni ya Bura ni moja katika zile kamati ambazo tumekuwa na matatizo makubwa sana nazo kwa sababu imebadilishwa sasa ni mara ya tatu. Tulitengeneza ya kwanza lakini baadhi ya viongozi walikuwa wanalalamika kwamba tumeweka watu wasiojua kusoma na kuandika kwa hivyo ikabidi Commission ivunje hiyo kamati ambayo tulikuwa tumeiunda akabakia mtu mmoja tu. Baada ya hapo wale ambao wameandikishwa wakawa na matatizo mengi sana mmoja kati yao tayari ni marehemu, amefariki, ambaye anaitwa Hussein Maramba tulimchagua kuwakilisha watu wasiojiweza lakini sasa kwa bahati mbaya amefariki. Mwingine ni Johora Omar ambaye ni mke wa Chief wa area ya huku huku ambaye naye bwana yake ana matatizo ya kesi kwa hivyo ikabidi kwa sababu anashughulikia mambo ya bwana yake asiweze kuhusika kikamilifu katika kamati yetu. Mwingine naye alichaguliwa wakati alikuwa mja mzito kwa hivyo sijui kama sasa amejifungua ama bado kwa hivyo hakuweza kushiriki kikamilifu kwa kazi ambayo alikuwa amepewa. Mwingine naye amechaguliwa lakini amesema kwa sababu ya usalama hangeweza kushiriki kwenye vikao vya Bura. Wanne wakawa hawapatikani na kama vile munavyo jua waheshimiwa wabunge mara nyingi wanakuwa Nairobi na mwingine katika kamati hiyo pia ni Chairman wa County Council ya Tana River ambaye naye anaenda juu chini kwa hivyo tukabakia watu watatu pekee yake. Kwa sababu hizo na zingine ikabidi Commissioner Zein ambaye ni mwenyekiti tubadilishe tena hiyo. Tulipokuwa Bura tulijadiliana kwa muda mrefu na Mheshimiwa mbunge wa area hii Mohammed Galgalo na tukakubaliana sasa kamati ya sehemu hii ya wakilishi bungeni ya Bura iwe kama ifuatavyo:-

Member wa kwanza ni yeye mwenyewe area MP Mohammed Galgalo halafu tuko na Salat Garacha ambaye ni mwenyekiti wa County Council ya Tana River, tuko na Omar Dhadho ambaye ni mwenyekiti ni mimi Co-ordinator, tuko na Mohamud Wario, tuko na Hawa Luli Aden, Elizabeth Wanjiku, Nuru Mohamed ambaye atakuwa anawakilisha jamii ya Wata, katika ile kamati ya kwanza alikuwa amewachwa nje, tuko na Adan Ibrahim Aralle kutoka pande za Bangale, na Osman Abatano atakuwa akiwakilisha watu wa Madogo na Hassan Bagana atakuwa anawakilisha jamii ya Malakote. Kwa hivyo tumejaribu kiasi ya uwezo kuhusisha sasa kila jamii na kila eneo katika hii kamati mpya na wengi wa wale ambao tumewaandikisha bado kwasababu tulipitisha juzi tu. Lakini ningependa wale ambao tuko pamoja na wao, Wanjiku njoo msimame kidogo muonekane halafu tuendele. Kwa hivyo members ambao tuko nao hapa tuko na Mohamud Wario ambaye ni Team Leader wa kamati hii ya sehemu ya Bura, tuko na Elizabeth Wanjiku inua mkono wakuone, tuko na Hawa Adan Luli. Hao ndio wale ambao wako pamoja na mimi, Chairman wa County Council yuko na Mheshimiwa mbunge wa area hii ameniambia pia atakuja na wale wengine ni wale ambao ni (in audible) Asanteni.

Kwa hivyo nisingependa kuzungumza sana maana hiki kikao si cha Co-ordinator, ni cha Tume bali sasa kuweza kualika Sheikh mmoja Mzee Gure aje aweze kutuongoza kwa maombi tuweke mkutano mkononi mwa Mwenyezi Mungu ili tufanikiwe. Kwa hivyo tunafikiria kwamba tukianza kikao tukae pamoja mpaka mwisho wa kikao. Wakati mwingine watu inabidi wa break for prayers ama lunch lakini sisi tunasema kwa sababu mnatoka sehemu za mbali ni bora kwetu tufulilize tumalize mapema ili muweze kurudi Saka, Kala sehemu za ndanindani, kwa hivyo tutakuwa pamoja mpaka jioni na kamati ya sehemu hii imewatayarishia kitu fulani ambacho kitaweza kuwafikisha mahali ambapo mnaenda. Kuna chakula kidogo kina tengenezwa

kwa hivyo kabla watu hawajafurukana baada ya mkutano tutakula halafu ndio muende. Kwa hivyo karibuni na asanteni Mwenyezi Mungu awabariki.

**Prayers:** Rabanna Attina Fidunya Hassanata Wa fil Akhirati Hassanata Wa kinna Adhaba Naar (inaudible) Antakheru rahimin, Sallahu Alla Sayyidina Mohammad

**Com: Zein:** Asante sana Omar. Wananchi mimi nitachukua fursa hii kuwaomba walio wenzangu tumekuja nao wajitambulisha kabla sijaendelea halafu na mimi nitajitambulisha. Nitaanza na mkono wangu wa mwisho kule .

**Com. Bishop Njoroge:** Hamjambo wananchi. Jina langu naitwa Bishop Bernard Njoroge na nimefurahi kuwa hapa leo.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Hamjambo, mimi ni Prof. Okoth-Ogendo wa Commission.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana. Mimi ninaitwa Abubakar Zein kama alivyosema Omar Dhadho, na ninachukua fursa hii kuwapa mwongozo na mwelekeo tutakaotumia leo katika kutoa maoni. Kwanza kabisa kama mlivyoona mnapoingia pale kuna meza watu wanajiandikisha majina. Tutatumia orodha hiyo inayotoka pale ili kufuata mtu alijiandikisha kwanza ndiye atakayeitwa mbele kufuata orodha hiyo. Lakini ikifika wakati tukiwa na sababu za kutosha sisi kubadilisha mwelekeo huo kidogo tutawaarifu na kuwaomba mtupe ruhusa kwa mfano kukatokea bibi mja mzito ambaye hawezi kungoja kwa muda mrefu tutawaomba mtupe ruhusa tumpe fursa azungumze aende, au kukaja mzee sana tufanye hivo hivo au akaja mlemavu tufanye hivo hivo au wakaja watoto tufanye hivo hivo. Sijui kama mnatupa ruhusa hiyo?

Halafu ukishaitwa jina lako utakuja pale kwenye kile kiti utaje jina lako kabla ya kuanza kutoa maoni yako. Ni muhimu utaje jina lako kwa sababu hawa wafanyikazi tuliokuja nao aliowataja Omar Dhadho mtawapa sababu ya wao kuwa hapa kwa sababu leo tuna microphone mmoja tukianza kuizungusha (inaudible) sana. Huyu binti yuko hapa anaitwa Fatuma Jama , Fatuma ndiye kiongozi wa wafanyikazi wa Tume tuliokuja nao na kazi yake .....(inaudible)... uta sign register uta sign kitabu kwamba umetoa maoni, kama unaweza kuwaonyesha hicho kitabu, na ukiwa una maandishi yoyote utampa atayaweka kwenye file ..... (inaudible) anayekaa karibu na yeye Walter atakuwa akiandika kwa mkono .....(inaudible) kila neno hata moja lisipotee ndiyo maana msituone pengine ita fika wakati pengine tumesita hatuandiki useme mbona wale watu hawaandiki maneno muhimu mimi ninasema. Tunarekodi kila kitu. Si ni sawa hivyo? Sasa ukija ukisema jina lako itakuwa inaingia kwa rekodi kwamba wewe wazungumza maneno yapi.

Utakapopewa fursa uzungumze kuna njia tatu za kutoa maoni. Ukiwa umeitwa jina, ikiwa una maandishi unataka kuyatoa bila kuzungumza utakwenda pale moja kwa moja hata sasa hivi ukiwa unamaandishi yako hautaki kuzungumza utakwenda kwa Fatuma utoe maandishi yako na uandike kwa register kwamba umetoa. Hiyo ni njia ya kwanza. Njia ya pili utakuwa na maandishi lakini unataka upewe muda uchambue yaliyo muhimu peke yake, sio usome ule mswada, sio usome yale maandishi.

Uchague mambo muhimu peke yake ili uyataje na wale wengine waliohudhuria hapa wapate kujua umezungumzia nini. Halafu njia ya tatu na ya mwisho kwamba huna maandishi lakini wataka kuja kuzungumza wewe kwa kauli yako yaliyo moyoni na kichwani bila maandishi pia hiyo inaruhusiwa.

Kwanza tutawapa kila mtu dakika tano, ngoja, watu wakishaanza kubuna namna hiyo huwaambia ngojeni nimalize kuzungumza halafu ndio ubune sawa. Kisa na sababu ya sisi kusema tutampa mtu dakika tano kwa sababu tushazunguka sehemu zingine nchini Kenya kabla ya kuja hapa, na kuna sehemu zingine bado, na uzoefu wetu wa kazi unaonyesha kwamba ukimpa mtu dakika tano anaweza kukitumia dakika zile tano vizuri na akamaliza mambo yake. Kivipi? Kwamba uchague yaliyo muhimu na utuambie sisi mapendekezo yako. Kweli shida ziko nyingi nchini na hatukuzui wewe kuzungumzia shida lakini ukija ukizungumzia shida dakika tatu halafu utoe pendekezo dakika ya nne inakuwa vigumu. Shida sisi tayari tunazielewa, tumezisoma, uje useme mimi ninapendekeza mambo kadha kadha kadha. Ukienda namna hiyo mambo yote yatakwishwa sawa.

Sababu ya pili sisi kusema hivyo ni kwamba tunataka kila mtu apewe fursa, sijui kama tunaielewana? Ikiwa tutampa mtu nusu saa watu wengine watakosa kuzungumza leo, kwa hivyo tutakupa dakika tano lakini haina maana kwamba ukiwa bado una mambo muhimu wataka kusema sisi tutakuzuia tukuambie basi hapo mwisho nyamaza, tutakuongezea dakika moja. Utaambiwa muda wako umekwisha sasa malizia. Ukiambiwa malizia umepewa dakika ingine moja. Kama wale wengine tumeshawatembelea nchini wanasema basi langu la mwisho, langu la mwisho kabisa kabisa, langu la mwisho kabisa kabisa, anaendelea hivyo na hatujamsimamisha. Naona huyu kijana anachekeka, ni mmoja ya wale wanaotaka kusema namna hiyo. Kwa hivyo ikiwa bado una mazungumzo tutakupa fursa mwisho kabisa dakika mbili ili tuwe na uwezekano wa kumpa kila mmoja wetu fursa ya kuzungumza au si sawa hiyo? Si sawa?

Lingine la muhimu kufahamu ni kwamba watu wanatuuliza je nikitoa maoni hapa yakamkasirisha mtu fulani, si ninaweza kuchukuliwa mimi hatua? Huchukuliwi hatua yoyote, maoni yako uliotoa yanalindwa kisheria, sheria inawalinda ma Commissioner na Tume iwe inakulinda wewe kwa maoni yako. Lakini hiyo haina maana kwamba tuje hapa tuanze kukashifu watu. Kama jirani yako alikukosea sasa uje uanze kumtukana hapa tunamipaka, siyo? Na pia tutumie lugha ambayo ni lugha ya muruwa tunaweza kuzungumza mbele ya wazee, kuna wazee hapa wenye umri, Mwenyezi Mungu amewapa umri wa kutosha na wana heshima zao vijana pia tuwaheshimu, kina mama pia wamo, tutazungumza namna hiyo. Na sijui itakuwaje kwa sababu mimi ninaona hapa walioko ni wanaume pekee yake. Sijui kina mama itakuwa wako wapi, sasa pengine tungewawekea sehemu yao kwa vile kwa sababu ya desturi zetu, tuwaekee labda sehemu wakae, lakini tukiwaacha pekee yao nje hawatafahamu. Tuwatengee sehemu pale waweze kukaa, au si sawa hiyo? Na ikiwa kuna mama ambaye pengine anataka kutoa maoni, lakini kwa sababu ya ada zetu hangependa kusema maneno yake hapa, pia tunaweza kufanya mpango ukasema maneno yako kando. Ikiwa mama ana mahitaji kama hayo utuambie, waambie wale pale mabinti wawili walioko nje au Diana au Fatuma tutafanya mpango huo.

Jambo lingine la muhimu ni kama alivyosema Omar kwamba tutaanza kikao chetu sasa mpaka jioni, sawa? Kuna swali lolote kufikia hapo? Basi naona tuko tayari kuanza ningependa kumuomba Prof. Okoth-Ogendo atuanzishie kikao hichi kama mwenyekiti tuendeleo na kazi hii Asanteni sana.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana. Sasa tuanze na Daudi Jaldesa, please sit there.

**Daudi Jaldesa:** Kwa jina naitwa Daudi Jaldesa ningependa kutoa maoni yafuatayo:

1. Hakuna mwingine wa kusujudiwa ila Mwenyezi Mungu pekee, mwingi wa rehema,
2. Siku ya ijumaa ifanywe siku kamili ya kupumzika yaani Public Holiday kwa kila Mwanakenya,
3. Waislamu wapewe idhini ya kuvaa vazi lao na waenda nalo popote pale wanaotaka,
4. Serikali itambue haki ya wafugaji kama vile inavyotambua haki ya wakulima kwa kuwahakikishia maji safi, afya na usalama,
5. Serikali isaidie wafugaji kwa kuwaanzishia board yao sawa na ya wakulima kama vile Coffee Board, Cotton Board na kadhalika.
6. Serikali iheshimu manyatta ya wafugaji yaani temporary shelters vile inavyoheshimu makaazi yoyote katika jamhuri hii ya Kenya na iwalipe ridhaa kama manyatta hiyo italazimika kuhama kwa shuguli fulani ya Serikali kama vile barabara na kadhalika. Yangu ya mwisho kuhusu ardhi tunaomba jamii ya mahali fulani yaani mahali pale ndiyo wahusika zaidi yaani wawe wanamiliki kabisa. Kwa hayo, asante.

**Gobu Galano Banta:** Asalaam Aleikum wandugu wenzangu. Mimi kwa jina naitwa Gobu Galano Banta. Maoni yangu ya kwanza kile kitu ningependa kutoa maoni mtu akiua anawacha yatima na yeye pia Serikali inaenda kuua. Sasa yatima anabaki pande zote mbili. Tunaona hiyo ni hasara. Afadhali Serikali iweke sheria fulani, mtu akiua awekwe sharti fulani ya kulipa hiyo familia ambayo wameuwawa waume zao asikuwe pande mbili yote akuwe na yatima watakuwa na shida baadaye.

Chief achaguliwe vile anachaguliwa Councillors kwa mlolongo ama kwa kura sababu Chief yuko karibu na wananchi kuliko kila mtu na Chief akiwa ameandikwa na Serikali hawezi akavunja amri ya DC, DC akitoa amri akisema hamisha hiyo miji atahamisha kwa sababu atakosa kazi yake. Kwa sababu hiyo Chief achaguliwe kama councillors. Ardhi, hukumu ya kutoa ardhi itolewe na Serikali. Wacha wananchi wenyewe waanzishwe kabisa chini sababu ardhi inaenda kwa matajiri sana, wale maskini wa sehemu hiyo hawapati ardhi hata akipatiwa ardhi anapatiwa sehemu ya chorocho huko nyuma. Ile ploti ya biashara kubwa kubwa anapatiwa mwenye pesa. Kwa hivyo hii mambo ya ploti ama kutoa ardhi wacha ianzie kwa maskini iende kwa wakubwa.

Masomo, masomo tungependa wahamaji wajengewe boarding wakati wanahama kwenda nje watoto wao wapate nafasi ya kukaa hiyo boarding na kusoma sababu wakihama kama hakuna boarding utawachia watoto wako nani akuangalilie. Kwa sababu hiyo Serikali isaidie wafugaji kuwa wako kwa hali ya shida ya kusoma sana. Hii inaitwa Masinga, Masinga Dam huko

Kabete wanatuletea shida kubwa sana sisi wakaazi wa Tana River ama North Eastern. Maji yote wanatufungia huko juu, maji ambayo zamani yanasambaa kutoka huko yanawachiliwa area hii kulima shamba ya kando kando ya mto tumekosa kulima sababu maji yote wanafungia huko juu. Na hii Masinga Dam haina faida na sisi. Stima ina supplyiwa Nairobi na sehemu zingine na hiyo stima hatupati sisi, kwa hivyo Masinga Dam ama ilete stima hapa tujisaidie nayo kuchoma dirisha, milango, tufanye nayo kazi, kazi zetu zingine kama wengine. Aidha ama watuachilie sisi hayo maji kama kawaida tulime. Kwa hivyo Serikali kwa Masinga Dam imetulalia sana, Tume ya Sheria wachukue hiyo maneno Masinga Dam watupatie haki yetu. Wa Aleikum Salaam warahmatulahi wabarakatu.

**Mariam Kaolo:** Wale wote tumehudhuria hapa mkubwa kwa mdogo Asalaam Aleikum. Nashukuru sana kwa kupata hii nafasi. Mimi natoa maoni kama haya, mimi naitwa Mariam Kaolo. Maoni yangu mimi ninatoa ni maoni kama haya. Sisi tuko hapa Tana River tumeegesha hapatulipo zaliwa hasa nilipozaliwa, nilizaliwa hapa Tana River mimi. Na nikakuia hapa Tana River, na wakati Kenya ilipopata uhuru mimi ni mdogo sana, lakini kidogo kidogo nafahamu baba yangu alikuwa yeye ni mtu wa Serikali na ninajua mahali nilizaliwa. Kwa hivyo niliona hatari kubwa sana na ndio maana mimi kuchukua nafasi hii ya maoni nitoe maoni. Hatari niliona mwishowe tunakuja kukosa mahali ya kukaa. Tunakosa mahali pa kukaa mahali mimi nimezaliwa na nika kulia na nika zaa na mtoto wangu akazaa naona kwama ninaanza kuikosa. Kwa hivyo mimi maoni yangu ninayatoa leo mimi nilipoamka baba yangu alikuwa askari baba alikuwa anaishi mahali inaitwa Liboi, nilikuia Liboi mimi ndio mahali mimi nilikuta barrier ya Liboi ikiwa wewe si Mwingereza. Nikakuia hapa na baba yangu akaoa hawa majirani zangu ndiyo walinilea mimi. Tukihama na mifugo tunakaa barani na hao majirani baba yangu alinunua mbuzi, ng'ombe na ngamia tunaishi huko. Wakati mvua imekosekana ndio tuna shuka Tana River wanakuja wanakunywa maji. Wale wenzangu ndio wanalima, tunanunua (inaudible) tunalishia ng'ombe, na mvua ikinyesha tunahama tunatafuta mvua tunaenda juu kutafuta mahali pa kulisha ng'ombe tunaondoka tunaenda. Na nikiona lugha moja tunawaitwa hawa mimi mara ninasema hawa majirani zetu walikuwa sijui lugha yetu. Tukija tukitoka huku tunakuja na maziwa tukiwauzia tukiwaita munyo mpaka baba akakuja akawacha kazi tukarudi hapa Tana River tukiwa ni hio mifugo wetu. Tukapanda juu tena maana hatukai hapa karibu na mtoni, sisi ni watu wa kuhama hama.

Sasa maoni yangu ninaona sasa mambo yanaendelea kuwa mabaya yaani sehemu ile yangu ni kama wapi mpaka Liboi turudishwe hapo hapo tukae hapo kama vile zamani tunaishi maana ndio niliona hapo ilikuwa kuna masilahi, ilikuwa kuna maendeleo, tulikuwa na mifugo na sisi tunaheshimiana, tulikuwa tunakaa na undugu maana tunakaa mbali mbali. Jirani yangu tukisalamiana mpaka tufike mahali pa Serikali tupige ripoti ndio nimuamkue na yeye mpaka apige ripoti anione ndiyo tuamkuane na tukiwa hapa hapa Kenya. Nataka irudi kama vile zamani ndiyo maoni yangu nataka kutoa maana naona hatari maana nikikosa mahali mimi ninakaa nitaenda nikae wape, mtoto wangu atakaa wapi, na nitahamia wapi? Hakuna mahali nitahamia. Kwa hivyo ninataka nirudi pale pale kwangu na niachwe hapo hapo kwangu. Ndiyo maoni yangu kwa Serikali, vile za zamani tunaishi tuishi namna hiyo hiyo ndiyo ninaona pana amani.

Lakini wakati tunaingiliana ikawa mtu atachukuwa nafasi yangu ajenge na mimi sina pesa ya kujenga gorofa yeye ananijengea

gorofa kwangu na mimi sina hiyo pesa ya kujenga na Serikali inamkubalia na ni yangu kwa vile mimi ni maskini sina pesa ya kujenga hiyo gorofa, niliona Serikali wanatunyimaa. Wananinyima sehemu yangu kwa vile mimi ni maskini siwezi nikajenga.

Maoni ingine naweza kutoa mimi maoni yangu navyotoa nataka mtu yeyote tunayemchagua Serikali itupatie nafasi tuchague yule wetu tunayempenda. Si tuchague wetu tunayempenda halafu tupitishiwe tuambiwe amepita bila ya kupingwa na huyo mtu hajajulikana maana Serikali ilitoa maoni ya kusema kwamba tuchague wetu tunayempenda. Kwanini tusitolewe yule yule tumechaguliwa? Na hii ni ya pili ya pili, tukimchagua huyu mtu, kama hana manufaa na sisi tutataka Serikali itupe nafasi tumtoe tuweke mwingine atuendeleshe maana Tana River iko juu ya Kenya maana haina jina tunataka na sisi tuwe na jina tukanyange mstari wa mbele. Hatutaki kulemewa, naona Tana River tunalemelewa. Hiyo ni maoni ya pili.

Maoni ya tatu, natoa hiyo ndiyo ya mwisho mimi ninaondoka, maoni ya tatu, mtu kila 1`mtu aliumbwa, nikiondoka, kila mtu ana mila yake. Kila mtu ana mila yake. Mastori mimi nilizaliwa nikaona nyanya yangu na babu yangu wakitoa mastori ya zamani nasikia watu nchi hakuna Serikali ikiendeleshwa na kitu inaitwa kijo. Hiyo kijo ndio inatoa amri na ndio Serikali inafunga na Serikali ina nyonga hiyo kijo ya zamani. Nikaona watu wasichana wavulana wanapelekwa msituni wavulana wasichana wanapelekwa wanacheza mire watahiriwa wanakaa msituni wanakuja kutolewa na sherehe kubwa. Kwa hivyo hiyo ni mila yangu, mwacha mila ni mtumwa. Mimi nitaendelea na mila yangu. Ndiyo vile ninaona, nimetoa maoni.

Asalaam Aleikum

Wa a sallam aleikum

**Prof. Okoth Ogendo** - Halima Fumu, Halima fumu

**Halima Fumu:** Wenzangu, wakina baba na wakina ndungu zangu, wale tukorika moja, wale wamenizaa, wale wababu zangu, asalaam aleikum? Mimi sina mengi ya kusema. Maoni yangu ni moja tu ya kusema. Wakati sisi kwanza mimi nimezaliwa Mbalambala ng'ambo ndio wakati tumeishi, nimeishi huko nikaolewa halafu nikaja Garissa. Nimesikitika sana, tunasikia watu wanasema hii Tana River iwe ndiyo mpaka ya Tana River. Kufungua macho nasikia mababu zangu wanasema mpaka wa Kenya na Somali ni maili tisa. Hii Somali inapiganiwa tunaona ajabu watoto wetu watakula nini na mimi nina vijana, na mimi nimezaa wasichana, tukipeana mto Tana River wasichana wetu watalima wapi? Mazao yetu yalimwa ni gambo, watalima wapi ikiwa mto ndio mpaka wa Tana River, watalima wapi? Na mimi nimezaliwa nikaona tumekaa nchi ya gambo. Hawa hawa watu wanatetea hii ardhi iwe ni yao wanakuja mwaka mmoja ukinyesha ndio wanaona mto wanakunywa maji, mvua ikinyesha wanatoroka, wakija mahindi yako tayari. Wanatungojea tukivuna wananunua mahindi, kwa kila mvua ikinyesha wanaenda. Naonelea Serikali wafanye mpaka ule ule wa ukoloni.

Swala langu la tatu tena, naona sisi wakina mama tumefungua macho, tukaona wababu zetu wakati kijana anawachwa karibu anakua baleghe, msichana anakuwa karibu baleghe wanaenda nchi za Malakoteni wanamwambia mzee mmoja ni Mkijo wanamwambia mtoto yangu ametosha kutahiriwa. Halafu wanakusanya watu halafu kuna kijiji moja sijui kama sasa



wamewacha mila, wana kijiji moja inafanyiwa hapa sherehe mwanamume anapelekwa msituni anatahiriwa haonekani mpaka siku ile amepona, achinjwe mbuzi, avishwe nguo, atolewe nje mama yake amuone, na sisi wanawake tuwekwe nyumbani siku ile umepona ndiyo ununuliwe manguo utolewe nje ndiyo baba yako na mama yako wakuone. Sasa mwacha mila ni mtumwa. Sina mengine ya kusema.

**Hussein Yunis:** Mimi ni Hussein Yunis. Maoni yangu ni mbili. Maoni ya kwanza

1. Mpaka wangu wa Tana River ubakie pale pale ulipowekwa na wakoloni
2. Maoni yangu ya pili, sehemu ambayo tuko na Waislamu wengu tujitawale kwa dini yetu. Sina mengi.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Mohamed Koricha, Mahad Ali, Mohamed, Roha Rolla. Okey let me now go back to Mwanahamisi, oh that's Mohamed, endelea basi. Wewe ni nani? Mwanahamisi, wewe ngoja ngoja wewe ni nani? Mohamed, endelea.

**Mohamed Koricha:** Mimi ni Mohamed Koricha kutoka Tana River, Bura. Mimi maoni yangu ya kwanza ambayo ninatoa ni kuhusu mpaka wangu wa Tana River. Mpaka wa Tana River nataka urudishwe pale pale ambao uliwekwa na mkoloni zamani. Maoni ya pili, kama kuhusiana na viongozi kama county council hivi ningependa hiyo kazi ya county council ipewe jukumu ya kamati ya watu binafsi washirikiane pamoja na chief. Maoni yangu ya tatu, kuhusu usalama majeshi, ningependa pia majeshi yawe katika wananchi wenyewe. Nafikiri hiyo ndiyo maoni yangu ya mwisho.

**Com. Zein:** Unaposema unataka kuhusu majeshi yawe wananchi wenyewe unamaanisha nini?

**Mohamed Koricha:** Ninamaanisha ya kwamba kama majeshi ingekuwa chini ya wananchi wenyewe nafikiri tungepata usalama wa kutosha maana tungejua sehemu zile ziko na shida zaidi.

**Mwana Hamisi Odo:** Kwa jina naitwa Mwana Hamisi Odo, naishi hapa Madogo. Asalaam aleikum. Mimi maoni yangu, sina maoni mengi sana yangu ni machache. Mimi maoni yangu ninatetea hapa Tana River yetu. Tunataka ule mpaka waliokuwa wakoloni wametuwekea maili tisa mpaka wetu uwe huo huo, hatutaki kubadilishiwa mpaka wetu. Mimi yangu ni hayo tu, sina zaidi, asanteni.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Fatuma Sora

**Fatuma Sora:** Assalaam aleikum *Inna makke tutuu*

**Translator:** Amesema anasalamia walio hudhuria hapa wote

**Fatuma Sora:** *Andhubbi guddio hinkabbu, dhubbi hinkabbu hundhi karra dhubbat.*

**Translator:** Anasema yeye hana mengi ako na machache anataka kueleza Commissioners.

**Fatuma Sora:** *Wan amm tan gallan kana*

**Translator:** Anataka kuongea kuhusu mto

**Fatuma Sora:** *Sehemun tenn mpaka meli sita, dhubb guyya loll nuu loll kambare sunnit yoo nuu dhubban, tunn taam adha dhurr sankk itt dakkattan*

**Translator:** Amesema mpaka wa hapa Tana River na sehemu ya jirani ya North Eastern ilikuwa ni maili sita – oh – maili tisa yeye alikuwa amesema maili sita lakini – maili tisa kutoka mto kuelekea upande huo lakini sasa umesonga mpaka juu ya mto wenyewe. Kwa hivyo ndio shida ambayo anataka kuongea juu yake.

**Fatuma Sora:** *Wann dhurr saan dhatten itt dakkate kess dufti, sunnt guyya kaan nu fayya, ta dhibbin nuffayitu, sunnum guyya kaan nunnen harka kabn dhubbin tanti martam.*

**Translator:** Yeye pia amefuata maoni yaliyotolewa hapo mbeleni ya kwamba kila mila iheshimiwa katika taifa hili. Hayo ndiyo yake ya mwisho.

**Mahad Ali Loka:** Mimi naitwa Mahad Ali Loka. Yale ningeongea nimeandika mambo mengi sana lakini mengine sintaongea kwa sababu wale wataalam walikuwa mbele washaongea kwa hivyo siwezi nikarudiarudia. Kwa hivyo moja kwa moja nikienda kwa maoni yangu ya kwanza ni Katiba. Hii Katiba tuliyo nayo sasa imenyima Wakenya wengi kwa sababu kwamba Katiba hiyo mpya iandikwe kwa lugha ya Kiingereza, lugha ya Kiswahili na lugha ya mama, ili wakati huu tunaona shida vile sasa mpangilio wa Katiba unaendelea Wakenya wengi hawajui maana ya hiyo Katiba ni nini. Hata saa hii mkiuliza katika hii hall hawawezi kusema katiba ni kitu Fulani, baadhi yao sio wote lakini baadhi yao. Kwa hivyo Katiba hii iwapo itaandikwa kwa Kiswahili, Wakenya wengi wataielewa si kama wakati huu ambapo Katiba inanyima Wakenya nafasi ya kuijua. Kwa hivyo mapendekezo yangu Katiba iandikwe hivyo.

Jambo la pili ni ya ubunge, maoni ambayo ninatoa ni ya ubunge. Kulingana na Katiba tuliyo nayo sasa kuna wabunge mia mbili na kumi (210), na kumi na mbili (12) ambao wanakuwa nominated na President. Shida iko mahali moja, Kenya tuko na makabila mengi na baadhi ya makabila wananyimwa nafasi kama vile Orgiek, kama vile tukirudi Tana River kuna kabila la Wata, Munyanya, Malakote, Oroma na Pokomo. Ndio wakati huu kabila kama Wata, nikitoa mfano, hawana chochote katika Serikali hii. Serikali ni mbili, Serikali kuu na Serikali ya wilaya, lakini unakuta katika Serikali kuu hakuna representative. Sorry, sio kwa madharau lakini wakati huu wako na councillor moja na assistant chief moja pekee yake katika jamhuri ya Kenya hii. Kwa hivyo mapendekezo yangu ni ya kwamba hawa wabunge 12 wafanywe hivi, maoni yangu. Watoke kwa yale makabila ambayo hayajapata nafasi. Kuwe na kamati maalum katika wilaya, itoe mapendekezo, ipeleke mbele halafu ipeleke kwa Parliamentary Service Commission ambayo hiyo PSC ipendekeze kwa President halafu wapewe nafasi hiyo kutokana na makabila siyo kila mtu. Shida tukiangalia saa hizi mfano kama ndugu zetu Wakikuyu wako na zaidi ya wabunge ishirini na kama leo nominated Member of Parliament atatoka hapo. Na mtu kama Orgiek asiwe na mtu yeyote katika Serikali itakuwa Serikali imenyima nafasi ya watu fulani. Ama kama Wajaluo wakuwe na wabunge zaidi ya arubaini na watoe maoni yao

bungeni halafu mtu kama Wata ama Munyaya, ama Malakote, Orma awe na mbunge moja ama asiwe na mbunge hiyo inadhulumu nafasi ya Wakenya. Kwa hivyo mapendekezo yangu ni ya kwamba hawa nominated Members of Parliament tuwe namna hiyo na waongezwe kutoka kumi na mbili hadi ishirini au thelathini.

Jambo la tatu, elimu. Hivi nchi hii Wakenya wengi hawajaelimika na Serikali mara kwa mara inasema elimu ni ya bure, mara inasema elimu itakuwa na karo Fulani, hivi juzi Serikali ilitangaza ya kwamba elimu itakuwa ni bure. Lakini dakika hii vile ninavyokaa yaani kutoka darasa la kwanza hadi darasa la nane hivi ninavyokaa, wale maskini watoto wao dakika hii hawasomi sababu kuna malipo kidogo, kidogo za hapa na pale ambao wananchi wa kawaida wale watu katika mashambani hawawezi, hawawezi kujimudu na wanaendelea kukosa elimu. Kwa hivyo kufikia baada ya miaka mitano kumi itakayo kuja, ni kusema ya kuwa hao watu watakuwa wameshakuwa wamekosa mwelekeo kabisa. Kwa hivyo mapendekezo yangu ni ya kwamba elimu kutoka darasa la kwanza hadi darasa la nane iwe free, watu wasilipe chochote, iwe free ina iwe ni ya lazima kwa kila Mkenya.

Jambo lingine ambalo lazima niongee, nchi hii tuko na sehemu za mashambani kama vile mnavyojua, rural areas and urban areas. Lakini sehemu za mashambani unakuta watu wanakosa nafasi kubwa kubwa katika Serikali ama katika maisha. Nikitoe mfano moja, juzi ilitangazwa yakwamba waalimu wa kwenda kusomea ualimu Colleges tuzo ile ilitolewa ni 'C' na hii mahali tulipo dakika hii Madogo unakuta hata mtoto mmoja hajachukuliwa na hatachukuliwa sababu hiyo grade hakuna, ama hata kama iko pengine somo fulani amekosa na Tana River ni sehemu ambayo imewachwa nyuma kidogo kielimu. Kwa hivyo mapendekezo yale mimi ninatoa ni kwamba kulingana na katiba mpya nafasi isiwe moja kwa moja bali rural areas wapewe nafasi ya namna nyingine. Mfano kama watu wa Nairobi, Mombasa ama urban areas watakuwa 'C' wale watu wa rural areas wapewe nafasi ya D+. Ni ndiposa wanaweza kupata nafasi kulingana na wale wengine na iwe ni first priority wapewe. Sababu unakuta saa hii ikisemekana B+ ndio wataenda University ama wataenda chuo fulani unakuta mtu wa 'C' hawezi kuenda na labda huenda ikawa kiwango kikubwa cha elimu ni hiyo. Ikiwa Nairobi, ama Mombasa ama Nakuru wanataka B+ ndio waende University na Madogo iwe elimu ya juu ama grade ya juu iwe ni C na ni mtoto wa kwanza katika maisha yake, pengine hiyo jamii hawajaenda University itakuwa Kenya ama Katiba tuliyo nayo itakuwa imedhulumu baadhi ya wananchi. Kwa hivyo nafasi isiwe flat rate namna moja bali rural area wapewe nafasi nyingine.

Jambo lingine ni habari ya mpaka. Wazungumzaji wengi wamegusia mambo ya mpaka. Pia naungana nikisema ya kwamba mpaka wetu na North Eastern ubaki kama kawaida vile wakoloni waliweka. Shida huenda ikatokea ikiwa mpaka huo utabadilishwa kwa sababu mara kwa mara unakuta sisi wakaazi wa mto Tana utakuta mto una hama hama. Kama hivi dakika hii zogo karibu kutokea. Kuna mahali panaitwa Mulanjo hapa mto Tana ulibadilisha mkondo, sasa shamba za upande ule zikahamia upande huu wa Tana River. Sasa wale wakidai wakisema hiyo sehemu ni yetu na watu wakiendelea kusema ni yetu ni yetu mwishowe kutatokea umwagikaji wa damu maana kutatokea vuta ni-kuvute. Kwa hivyo hiyo ndiyo baadhi ya mambo ambayo ningependa Tume iangalie kusiwe na mabadiliko yoyote. Halafu hapo hapo Serikali ya ukoloni ama Katiba tuliyo nayo wakati huu haijatoa mpaka kamili kulingana na views zangu. Kwa hivyo Katiba hii iweke mpaka kamili na ndiyo unakuta

Wakenya siku hizi wanazozana kama vile Pokot huko, Mt. Elgon , huko Gucha na kadhalika unakuta watu wanazozana kwa ajili ya mpaka. Kwa hivyo mipaka iwe stated in the Constitution iwekwe katika Katiba na Wakenya wote wajue sio mipaka tu tunaongea na leo inabaliwa inakuwa vingine na kesho inabadilishwa ina kuwa vingine, hii inaleta mzozo katika hii jamhuri yetu ya Kenya.

Halafu ya mwisho, naona Doctor ananiangaliangalia sana akiniharakisha. Ya mwisho, sehemu za mifugo mimi ninaona Serikali imedhulumu watu wa mifugo kwa sababu ukiangalia sasa ni agriculture ingawa imechanganyika na mifugo lakini mifugo pia ni rasilmali kubwa sana, ni sehemu ya mapato katika nchi hii. Naona vile kulikuwa na KMC ilikuwa ikiingiza pesa za hali ya juu lakini sasa imeanguka. Kwa hivyo maoni yangu ni hivi watu wa mifugo wachimbiwe boreholes kila sehemu. Watu wa mifugo wachimbiwe boreholes na iwe ni lazima kwa mipangilio ya Katiba mpya. Pili, Serikali ipatie watu wa mifugo nafasi ya kupata elimu au maji. Nafikiri hapo sina haja ya kueleza. Kwa hayo machache sitaongeza ingawa baadaye naweza kuongeza vile mlivyosema. Nina mambo mengine, kama maoni hayatakuwa yameongezwa, nitaweza kuongeza. Nasema asanteni.

**Com. Bishop Njoroge:** Nimesikia umesema mpaka ubakie kama uliyowekwa na wakoloni Kuna makaratasi ya kusema kwamba wakoloni waliweka mpaka au umepata haya wapi? Ningetaka tu kujua.

**Mahad Ali Loka:** Kulingana na vile ninavyoelewa saa hii siwezi kukupatia lakini kuna maandishi na Katiba tuliyo nayo sasa imeeleza hali ya mpaka kati ya sisi na upande ule mwingine. Iko kwa Katiba.

**Bishop:** (inaudible)

**Mahad Ali Loka:** Nafikiri Bwana Commissioner, nikisema hivyo kwa mfano kama hii map ya Kenya tuko nayo sisi tunapakana na Tanzania, Uganda na kadhalika. Sio sisi tumeweka, sio sisi tumeweka, ni wakoloni ndio wameweka na bado tunafuata. Asante.

**Halima Rupia:** Kwa majina ni Halima Rupia, maoni yangu ni hivi. Ulinzi na usalama wa Taifa: majeshi na matawi yake viundwe na Katiba ili tuweze kuwa na uaminifu na kutenda kazi kama jamii bila dhuluma. Vyama vya kisiasa: vyama vingi vimeleta umaskini na vita vya makabila, kwa hivyo ikiwezekana kuwe na vyama viwili tu vya kutimiza demokrasia na kuleta nidhamu kwa jamii kama taifa na pia kuleta ustawi nchini. Mbunge: kwa sasa tukichagua mbunge akienda huko, wengine wanapotelea huko Nairobi, kama miaka tano hivi hatumuoni. Akienda ni kimoja, pengine kwa miaka mitano huja kama mara mbili peke yake. Kwa hivyo ikiwezekana mbunge ambaye hatekelezi kazi yake kwa raia uchaguzi uitishwe na wananchi ili wachague mbunge mwingine. Kwa hayo machache nasema Asalaam Aleikum Warahmatullahi Wabarakatu.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Juma Osman, amekuja

**Jibril Osman:** Asante sana mimi naitwa Jibril Osman niko na machache hapa ya kutoa maoni. Maoni yangu ya kwanza vile

wenzangu wa mbele walisema nii chief achaguliwe na kura sababu wamesumbua wananchi. La pili, Katiba mpya hii kwa maoni yangu iangalie mambo ya sheria ya MPs wale wanachaguliwa hii miaka tano hii kwa sababu wakichaguliwa miaka tano hatuwaoni, wanakuja siku ya kutafuta kura. Kwa hivyo maoni yangu ni kuweke kitu kingine kizuizi hapa kama iko Katiba mpya pengine, mimi nimetoa maoni yangu, baada ya miezi tatu akikosa kufika sehemu yake ashtakiwe ama achaguliwe mwingine.

Ya tatu maoni yangu naona uwezo wa Rais upunguzwe, uwezo wa Rais upunguzwe, sababu umekuwa zaidi. Nimeona ya kwamba saa hii yuko juu ya sheria ati hawezi kushtakiwa hata akikosa. Hiyo inamaanisha mambo yote yeye tu ndiye anafanya sababu yeye tu ndiye ako juu ya sheria. Huu upunguzwe awe chini ya sheria, maoni yangu.

Ya nne kulingana na dini hii yetu ya Islam, watu wakienda korti ya Kadhi rufani tukichukua Appeal ati tena tunakwenda High Court, sasa tunarudi tena ule upande mwingine. Mimi ninaona afadhali tukichukua rufani asitupeleke kwa hali ya High Court tena, tupeleke tu kwa Chief Kadhi halafu hapo ndiyo amalizike. Tumeanza na Kiislamu amalize kwa Kiislamu. La tano, mipaka ikae vile mipaka ya kila sehemu ama kila District kila watu mipaka ikae kama ile ya zamani kwa sababu ndiyo inaleta clashes mingi sana hapa. Mfano ninatoa kama upande wa Mwingi, mipaka yetu ya Tana River ilikuwa upande wa Nguni wamehamishwa wameletwa hapa sijui hapa katikati Sosoma imehamishwa anasema hapa Katumba imehamishwa hata sasa watu wanapigana sijui Serikali iko wapi waamue hii mipaka. Mipaka tunapendekeza ikae kama ile ya mbele.

Ya sita Katiba hii ambayo tumesema ile ya mbele ni mbaya tuunde ingine, mimi naona maoni yangu ni bure tunaunda katiba kwa sababu sheria ya Kenya inavunjwa na pesa. Hata ukiweka Katiba gani mimi nimeona maoni yangu pesa ndiyo inavunja ile Katiba. Kwa hivyo maoni yangu mpaka wale wanaiba kutumia hii pesa hata sheria haifanyi kazi, yule anasimamia sheria anafanya mambo ya pesa anawacha yale maneno mengine. Mimi ninaona umuhimu kabla bado kuunda sheria watu tumalize ule usaliti wa yale mambo mbaya mbaya.

Maoni yangu ya mwisho, mimi nimeona kwa maoni yangu upande wa Local Government wanachukua ushuru mfano nitoe kama Bangale pesa inayochukuliwa sehemu ile ni pesa nyingi. Halafu bila kubakisha sehemu pesa inapatikana pesa yote inapelekwa Hola halafu inapelekwa Nairobi. Ati tuongoje baadaye na hatuioni. Napendekeza sehemu ambayo imechukuliwa ushuru pahali ya Local Government wakati wa kupeleka pesa ibakishwe kiasi fulani pale mahali ambapo imepatikana hiyo pesa. Kwa hivyo mimi ni hayo, asante sana.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana. Kayo

**Kayo Jiba:** Mimi naitwa Kayo Jiba, napenda kutoa maoni kwa njia kamilifu kwa sababu katika area hii yetu ya Tana River kuna malalamishi kubwa. Somali anatunyanyasa, na watu wa Tana River wenyewe wanatunyanyasa katika area hii ya Madogo. Kwa sababu vile kusema mpaka ambao ya kusema North Eastern Province, mpaka huo wakolini waliweka na vile ulikuwa unawekwa hakuna matatizo yoyote. Lakini tokea Kenya ilipata Uhuru, haya matatizo yameingia mengi. Wale Wasomali wanatuua bila sababu yoyote katika area hii. Kwa hivyo mpaka uwe kama ule ule wa ukoloni wa zamani. Pia sisi

tulikuwa tunakaa ng'ambo ile na ng'ambo hii na hakuna shida yoyote. Somali akitoka huko anakuja kukunywa maji anaondoka anaenda kule kwao. Baada ya Kenya kupata uhuru Somali ametuhamia sisi. Kwa hivyo mpaka uwe ule ule wa ukoloni wa zamani. Kwa hivyo sina mengi ya kuongea, ni hayo machache. Asante sana.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana. Mohamed Gure

**Gure Mohamed:** Asalaam aleikum. Jina langu ni Gure Mohamed. Maoni yangu ya kwanza, kama mwenzangu amekua ametangulia amesema Chief achaguliwe kama Mbunge au Councillor. Ya pili, Councillor au Mbunge yule ambaye hakutosha kazi yake atupwe, achaguliwe mwingine. Jambo la tatu, watu wa kuhamahama wafugaji kila mmoja akae kwa district ile aliyetoka, asiwe anavuka huko na huko. Jambo la nne, mpaka wetu au mipaka yote ya Kenya ikae kama zamani wakati wa ukoloni. Ni hayo tu machache.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana, Mohamed Abalole

**Mohamed Abalole:** Kwa jina naitwa Mohamed Abalole. Maoni yangu ya kwanza ningependa kutoa mpaka wetu na North Eastern kama tunavyojua ni maili tisa kwa sababu kutoka tulipozaliwa tulisikia ya kwamba mpaka wetu ni maili tisa. Maoni yangu ya pili ni juu ya mahakama. Ningependa kutoa maoni, mtu akishashtakiwa sio kuwekwa tu ni suspect, ni suspect mwaka nzima na pengine hana hatia. Kwa hivyo ningependa mtu akishashtakiwa apelekwe kortini kwa one day.

Maoni yangu ya tatu kuajiriwa kwa Chief. Hawa ma-chief wanaojiriwa siku hizi utakuta mtu anaandikisha application watu mnia moja na utakuta mtu ambaye amepata hiyo kazi ni mtu ambaye hapendwi na wananchi, ni pesa tu ndiyo imemuajiri hata hana elimu. Kwa hivyo ningependa kutoa maoni yangu, Chief achaguliwe na wananchi. Maoni yangu ya nne, mila ya Afrika iheshimiwe, kwa sababu tunaona mila siku hizi inapuzwa zaidi. Maoni yangu ya tano, Bunge, na Councillors. Utakuta wakati wabunge wanaajiriwa na wananchi moja kwa moja anaenda City hutamkuta tena mpaka five years inakwisha, hata hajui wewe, hata ukienda huko Nairobi kwake anakuona kama wewe ni mbwa tu. Kwa hivyo ningependa katika Katiba hii ipitishwe mbunge yeyote ambaye amesahau sehemu yake, afutwe na wananchi wale waliomchagua.

Maoni yangu ya mwisho, ningependa Katiba hii mpya iangalie kuhusu mambo ya mahakama ambapo utakuta wewe una chuki na mtu na huyu mtu pengine ana madaraka kushinda wewe, unakuja kushikwa tu ukiwa huna makosa ambaye ni OCS ametoa amri ushikwe. Kwa hivyo utashikwa tu ukiwa wewe huna makosa na unaenda kuwekwa for three days four days na hutashtakiwa na unawachiliwa hapo hapo. Kwa hivyo uwezo huu wa polisi pia ningependa katika hii Katiba uangaliwe na upunguzwe uwezo wao. Langu la mwisho ndilo hilo.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana. Sasa Bishar Hassan

**Bishar Hassan:** Mimi kwa jina naitwa Bishar Hassan. Nafikiri mimi nitasoma na Kiingereza.

1. Reduce the Executive powers. The Civil Servants who were recruited by the independent Public Service Commission were protected from political influence. Unlike today the President could not dismiss the Civil

Servants at will, only the Public Service Commission could dismiss or discipline them.

2. Constitution should be dynamic. A Constitution reflects the political, social, cultural and economic values of a society at a particular moment in history. If these values keep changing the constitution itself has to change after every five years.
3. All Presidential appointees including Ministers and their Assistants, Attorney General, Permanent Secretaries, Ambassadors, and High Commissioners and Judges should be approved by the Parliament. Repeal or scrap section of Chief Authority Act which gives them power to outlaw excessive power of breaking up a social gathering or arrest people without warrant of arrest.
4. Provincial Administration should be abolished because their services are superfluous e.g. when they arrest people they make a citizen arrest and hand over to the police. In that case their service is not that important to my opinion.

The President's power to dissolve Parliament before its term should be scrapped, Parliament should have a fixed term and develop its calendar. It should be possible to impeach the privilege. Impeachment is a process in which the President is tried by the Parliament and if found guilty forced out of the office. Abolition of law or the constitution or corruption in office should be grounds for impeachment. Hiyo ndiyo maoni yangu.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana. Sadia Gutu

**Sadia Gutu:** Kwa jina naitwa Sadia Gutu. Akina mama wenzangu, akina baba Asalaam Aleikum. Mimi kama mama maoni yangu ningependa kusema tuko nashida hapa Kenya haswa wilaya ya Tana River. Shida ile tuko nayo ningependa kusema wale ambao wangetakikana kuchukuwa ID Card mambo mzaliwa Tana River anafanyiwa vetting tungependa iwachwe kabisa. Mzaliwa asifanyiwe vetting unless ni mtu anatoka nje ndiyo afanyiwe vetting.

Mambo ya pili, hiyo imezungumzwa na wengi lakini naipendekeza tu. Lazima kwenye kilio kingi kuna kitu. Hii habari ya kusema tunasikia fununu ati mpaka wa mto Tana na North Eastern ati ukuwe mto Tana. Hatuwezi kukubali. Serikali ichukuwe hiyo hatua, huo mpaka vile vile uliwekwa na mkoloni ubaki namna hivyo. Kabisa hatutakubali usiku wala mchana. Na tuko tayari kabisa vyovyote hatuwezi kukubali kwa sababu hiyo ni haki yetu. Kwa sababu tukipokonywa hiyo, hiyo mpaka ikishaondolewa saa hiyo watu wetu wa Tana River wako na mashamba huko, kuna wale wamejenga huko, wanaishi huko ati kwa vile sisi ni maskini hatuwezi kujenga magorofa tunapokonywa mpaka wetu. Hatuwezi kukubali hata kidogo, kwa hivyo hiyo lazima iangaliwe.

Pili, nataka kuzungumzia haki za akina mama kwa vile mimi ni mama. Ningependa kusema mtoto wa kike apewe haki sawa na mtoto wa kiume. Haki sawa ni kama elimu, mambo yote ile mtoto wa kiume anaweza kupewa apewe mtoto wa kike pia. Kama ni elimu, chochote kile, kama ni madaraka, sana sana sisi Waislamu tunasema mtoto wa kike hawezi kuwa Chief, hawezi ongoza. Hayo mambo ningependa iwekwe katika hii Katiba. Kama ni Chief, sisi wanawake pia tunaweza kuwa Chief, tunaweza kuwa hata P.C. Tayari saa hii tuko naye. Lakini we Muslims kwa dakika hii hatuna.

Mambo ya nne ama ya tatu, kuna mtu amefanya makosa anashikwa anapelekwa polisi anakaa kaa hapo station baadaye tena



anapelekwa kortini. Sasa kule kortini akipelekwa, hahukumiwi ikija ile tarehe amewekewa ikifika anaitwa, akija bila maongeo yoyote inasongeshwa tena tarehe ingine. Hatujui ni nini inaendelea, hafungwi, hawachiliwi, anazungushwa hapo. Kwa hayo machache sina mengi, hayo ndiyo maoni niko nayo. Asanteni.

**Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana. Madina Godana, Yusuf Marafu

**Yusuf Marafu:** Assalam Aleykum. Jina langu naitwa Yusuf Marafu, na nitaanza na maoni ya kwanza.

1. Amend Public Collection Act and provide that permits are not required for purposes of organizing fund raising event
2. The President powers to create ministries, public offices, districts, and provinces should be made subject to parliamentary approval.
3. The Government should employ (KPR) Kenya Police Reserve, like any other soldiers or else they might use Government guns illegally without their will because it is only liability to them if they don't earn. "Party prostitution" should be stopped i.e. shifting from one party to another party. Hayo ndiyo maoni yangu ya mwisho.

**Prof. Okoth-Ogendo:** Madina Godana, she is not there? Hassan Abdullahi

**Hassan Abdulla Mashongo:** Asalaam Aleikum, mimi kwa majina naitwa Hassan Abdulla Mashongo maoni yangu ya kwanza ninatoa maoni kuhusu boundary ile iliwekwa. Sisi zamani tulikuwa tukiishi ng'ambo ya pili, tuko na mzinga huko, tuko na mashamba huko. Baadaye tu Kenya ilipopata uhuru tukawa tunavuka upande wa pili. Lakini income yetu kama mzinga, mashamba yote yamebaki ng'ambo ya pili na sasa hao wageni ambao wamekuja kama Wasomali ati wanataka mpaka uwe mto Tana. Kama wao wanataka kuishi Tana River tu, waje tuishi na wao lakini wasivute mpaka kuleta hapa. Walete Garissa North Eastern kwenye mto Tana. Tuje tukae na wao kama Wakenya wenzetu na tushirikiane. Hiyo ni maoni yangu ya kwanza.

Ya pili, tuna watoto ambao wamesoma wanatosha kuajiriwa kazi ya Serikali kama ya AP, Polisi. Badala iandikwe district iandikwe kutoka location. Hawa vijana wetu wakitoka hapo waende district wale ambao wako district wameshapanda mimea tangu mbeleni, hawa wanaenda na wanarudi. Kwa hivyo waandikwe kutoka location badala ya district peke yake.

Maoni yangu ya mwisho, hawa askari wa KPR sisi tulikuwa tukisumbuliwa na bandits hapa na pale. Kutoka waandikwe hawa askari wa KPR, tumepata kidogo angalao sababu askari wako kambini hawa KPR tuko nawao, hao bandits hawajui wataingia na wapi na watatoka na wapi. Hawa KPR wa sehemu zingine wamepewa bunduki za kawaida na askari wengine. Hawa wetu wa hapa ni kama wamebaguliwa. Wanapewa ile bunduki ya zamani na ni mzito, kila wakati tunapiga kelele wabadilishiwe hii bunduki hawabadilishiwi. Kwa hivyo ningependekeza hawa KPR wabadilishiwe bunduki za kawaida sawa na wale KPR wa sehemu zingine. Hayo ndiyo maoni yangu ya mwisho.



**Prof. Okoth-Ogendo:** Mwanajuma Salat.

**Mwanajuma Salat:** Kwa jina naitwa Mwana Juma Salat, maoni niko na maoni mbili. Maoni ya kwanza niko nayo mpaka wa Tana River tuliowekewa ukae hapo hapo usiondolewe. Maoni ya pili, shule hii yetu ya primary kutokea class one mpaka eight wasome bure. Wengi wanakosa masomo. Maoni yangu ni hayo mawili.

**Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana, Madina Godana

**Madina Godana:** *Madina Godana. Mpaka tenn taa dhurran maal taa Ingeressa sunnitt dhabbarta hinkabnu nuu teneshannurra hissan hinfennu. Issi nussongan garr injee gull nudhibban dharga sha hinfennu.*

**Translator:** Anasema mpaka ule umewekwa na Waingereza hataki usonge huko wala huko usinyime hao wala usinyime pia wandungu zao.

**Madina Godana:** *Taa lammesittu, Nuu Islammu, Islammullen akk shiakabthi nuut dhandhenne adha tante kimila tante hintannu. Itt dhallanne, itt gugurdhanne, ilman itt gugurdhiffan. Dhandhenne hinlakkifnuu. Maneno yangu ni hayo*

**Translator:** Anasema wao ni Waislamu na pia wako na mila yao ya Kijadi, kwa hivyo hawawezi kuwacha mila yao ya Kiislamu wala mila yao ya Kijadi .

**Prof. Okoth-Ogendo:** Lalafa Dhadho

**Lalafa Dhadho Hato:** Naam, mimi naitwa Lalafa Dhadho Hato. Nitajaribu kufupisha maoni ambayo nitaweza kutoa machache. Kuhusiana na President Act, President yeyote katika Kenya ambaye amejaribu kufanya mambo ya corruption, wizi wa pesa, uwaji, anafaa ashtakiwe asiwe juu ya sheria. Ya pili, Katiba hii ya kwanza ambayo tuko nayo Kenya imepata uhuru, hii Katiba ni Katiba ya ukoloni tunataka hii Katiba - (inaudible) akisha na hajafanya miradi yoyote na amepotea, wale voters salimpitisha waandike kwa Speaker, Speaker awe na powers za kumuondoa huyo mjumbe halafu ifanywe re-election. Councillor yule amechaguliwa tena na katika Location kama yule Councillor hakuna miradi yoyote amefanya wale watu walimchagua from council wananchi wamemchagua, waandikishe waandike majina zao na voters registration iende tena halafu yule councillor aondolewe katika kiti chake.

Ya mwisho, mambo ya uhamiaji. Sisi kama Tana River tuko wengi lakini Tana River tuko kabila Tano, iko Orma, iko Wata, iko Wardhei Gabra, iko Munyayaya, iko Malakote, iko Pokomo. Hii uhamiaji yeyote ambaye si kati ya hiyo kabila tano akiingia Tana River lazima awe na documents maalum sehemu ametoka Kenya ya saa hii Katiba inasema ni uhuru wa kutembea kila mahali lakini uhuru huu saa nyingine ukiiangalia imeleta shida. Watu wa Tana River ni watu wa amani, lakini utakuta saa hii kuna shida nyingi kati ya uhamiaji. Kwa hivyo tunataka lazima yule amekuja katika district zingine iwekwe sheria ya kutoingia hiyo district. Yangu ni hiyo.

**Josiah Githinji:** Jina langu ni Josiah Githinji, yangu nitatoa kwa lugha ya Kiingereza kwa sababu nimeandika. The first one ni the Constitution itself. The Constitution should be supreme that it cannot be easily changed, amended or misused by the Executive or Parliament or the Judiciary. It should address itself to the needs, aspirations and vision, and mission of the State. It should be the final authority in the matters of law, power and should have a constitutional court which should be the highest in Kenya. The Constitution should only be amended by having a national referendum comprising all the people and all the stakeholders. The Constitution should be final in the matters of law, there should not be other changes, other amendments or other laws that actually hinders the peace of right of expression and the freedoms that we have. Then the Constitution should respect human and individual rights; the rights to privacy, the rights to protection against harrasment, freedom of enjoyment and basic rights. The Constitution should also address issues of social amenities, rights of employment and development, and the Constitution should also address issues of clean environment. The new Constitution, should also have a universal declaration of free primary education that includes, standard eight, it should be free education upto standard eight.

Kitu kingine nachangia, ni kuhusu the disabled people or people who are suffering - watu ambao wana disability. These people they have been neglected for long. The new Constitution should protect, guarantee and have privileges to their basic needs. The Constitution should assure that every disabled person should be given free carts, free hearing devices and allowances to meet their needs. Also the roads and houses should have a law insisting that people with disability are given equal access to enter those houses.

Citizenship, yaani uraia wa Kenya. All born in Kenya regardless of parental backgrounds qualify automatically to be Kenyan citizens. I mean maternity hospitals hospitals should be the place of registering Kenyans. Secondly on citizenship, every married woman married by a foreigner, the husband should qualify to be a Kenyan citizen. Every married husband, his wife should qualify to be a Kenyan citizen. The constitution itself should address itself like this - "Kenya is a multi-racial, multi-colour, multi-ethnic, multi-religious nation without any discrimination in terms of race, religion, colour, tribe, class, ethic or social economical class, equal rights, equal privileges, equal freedoms, equal persuits that are protected and enshrined in the new Constitution. And there should be equal rights to employment, equal rights to acquire skills, equal rights to acquire developments, equal rights to have the necessities of life."

Kitu kingine ningetaka pia kuchangia, ni the Electoral Commission na the Electoral Law. The new Constitution should set up these Electoral Commission and these should be protected by the law, where they manage elections, they conduct, and we have equal representation on behalf of every citizen.

Kitu ya mwisho ningetaka kuchangia ni protection of the freedom of consciousness and religion. Every person has a right and freedom to join any church or any religion without being interferred with. Every person should have a right to change his religion or to change the way he believes or to worship in the way that he feels like. Also these religious organizations have a right in Kenya to establish hospitals, to establish nursery schools, to establish learning institutions. In this aspect also, nobody

should be forced to participate in the activities of religion or to be hindered from joining such religion or that type of religious practice.

And the final one, concerning the President. Mwisho ni kuhusu the President, that Kenyans should have a President who has no power, he is just a ceremonial person with the Prime Minister akiwa ndiye Head of the Government, and he is the Head of the Government Business in the Parliament and he is the Chief Executive Officer of the Nation. He should be elected by the party.

And finally, the Judiciary. The Judiciary nimechangia that we should have a Constitutional Court, we should have the Court of Appeal, High Court, Regional Courts, Marriage Courts, the Family Courts and the Kadhi's Courts. Na hii ingine kwa sababu nimeandika, I will not read it, thank you, asante.

**Com: Zein:** Unapendekeza kwamba, uraia utolewe kwa usawa mtoto anapo zaliwa Maternity, kuna sehemu nyingi sana nchini Kenya hakuna maternity.

**Josiah Githinji:** Huko ambako hakuna maternity there is what we call Traditional Birth Attendants. They should be given the right to register that child.

**Hussein Farah Waju:** Jina langu ni Hussein Farah Waju. Jambo la kwanza ambalo ningetaka kuongea ama kutoa maoni juu yake ni Kadhi's Court. Ningependeza namna hii, Kadhi's Court katika nchi yetu ya Kenya iwe na full powers on Islamic laws like any other magistrate's court in the country. And should have enough responsibility to deal with Islamic affairs. Jambo la pili ambalo ningetaka kuongea ni kuhusu security. Ningependekeza namni hii, kwa vile area nyingi mpakani security yake siyo sawa, ma-officers ambao wako wawe well-armed with all facilities, accommodation and special allowances kuangalia usalama wa wale wakaazi wa hiyo area. Kwa sababu nasema hivi sehemu kama Mbalambala ambayo ni mwisho wa mpaka wa Tana River ni kilometer 80 kutoka hapa, na hata wakati huu mimi ninaongea hakuna communication yoyote, kutoka Hola mpaka hiyo area, hakuna simu, barabara ni mbovu, hakuna askari na askari wale walipelekwa pale walitoka hiyo area kwa ajili ya ukosefu wa hivi vifaa. Kwa hivyo zile areas tungependa wale ma-officers ambao watapelekwa pale wawe wako na silaha za kutosha, silaha ambaye wanaweza kukabiliana na majambazi, yaani sophisticated weapons.

Jambo lingine, kuhusu elimu, mimi ningependekeza sisi katika area hizi remote, we should have special categories ya elimu for teachers training and other institutions. Yaani tusifananishwe na area ingine ya nchi hii kama Kiambu, Nyeri ambapo wako na facilities, za kutosha. Kwa hivyo tusiwe tunaambiwa kwamba a candidate must have qualifications of C+ and above. Kwa hivyo napendekeza tukiwa na D+ sisi tunaweza kuenda these institutions kama Medical, Teachers Training & other institutions apart from Universities.

Jambo lingine, ni kuhusu mipaka. Mimi napendekeza three miles iwe mpaka wetu sisi na watu wa North Eastern Province. Uwachwe vile uliwekwa hapo na wakoloni sababu naona ma- Commissioners waliuliza mko na documents ya kuonyesha, I am sure there is a document. If I don't have it right now here, lazima kwenye ofisi za Serikali you are accessed to, mukiangalia mukijaribu kuchunguza ama kutafuta bila shaka mutapata. Otherwise hatungelisema, moja kwa moja yeyote ambaye amekaa hapa kutoa maoni yake, kwamba mpaka ni three miles, uko three miles na tunapendekeza kama wananchi maoni yetu three miles ibaki. Mfano, nitawaonyesha kama ni three miles right away. Mimi nikiingea hapa kuna sub-location saa hii iko ng' ambo ya Garissa, inaitwa Ziwani sub-location ambayo Assistant Chief yake yuko huko lakini utawala inatawaliwa na DO wa hapa Madogo. Kwa hivyo three miles itaonyesha ya kwamba three miles is there. Isitoshe, mashamba zetu nyingi ziko three miles kutoka River Tana, kwa hivyo napendekeza three miles ibaki vile iliwekwa na Serikali ya ukoloni.

Jambo lingine, lands adjudication system, should be introduced immediately to avoid unnecessary immigrant movement eg. Pastoralists and the spread of diseases to our animals. Yaani ninasema hivi, area yetu ifanyiwe demarcation, ili sisi wakaazi tuweze kumiliki ardhi yetu, tuweze kukaa, ili wengine wakitoka kwingine wakose nafasi ya kukaa. When it is temporary now, kila moja anaweza kutambaa ndani, kwa hilo tungependa hilo jambo liangaliwe ili tuweze kuweza kunufaika na ardhi yetu.

Jambo lingine ambalo ningetaka kuongea ni kuhusu Kora National Park. Mimi napendekeza namni hii, Kora National Park is in Tana River legally lakini Kora National Park imemilikiwa na Kenya Wildlife Services bila kujadiliana na wenyenji, kwa hivyo mimi napendekeza Kora National Park iwe de-gazetted na irudi kwa community. Sababu nikisema hivi, wakati wa ukame area zetu mvua huwa ni kidogo, sisi pastoralists tunaweka mifugo wetu katika Kora National Park wakati wa kiangazi na mali yetu wanakula hizo area. Lakini kwa vile iko katika Kenya Wildlife Service, hata mtu binafsi hawezi akaingia, na ukiingia unawekwa ndani. Kwa hivyo tungependa Kora National Park irudi mikononi mwa wananchi ya Tana River.

Jambo lingine, Kindaruma ama Kiembere Dams, ambapo electricity inatoka kupitia River Tana, wale wanapata manufaa ni districts zingine ambazo ziko jirani na sisi. Sisi watu wa Tana River hatuna manufaa yoyote na hiyo Tana River. Shida ya kwanza ambayo ni kwamba ina-cause water shortages, sababu zamani kabla ya kuwekwa Kiembere na other electricity generating powers, sisi mto ulikuwa ukivunja, watu wetu walikuwa wakilima. Kwa vile maji imekuwa controlled in that area, watu wetu sasa wanakosa hayo maji ambayo mto zamani ilikuwa inavunja watu wetu sasa wanachukua mpishi ya famine relief. Na sisi ni wilaya peke, wilaya hamsini na kitu, hamsini na mbili na tatu katika Kenya, ni Tana River pekee ambayo haina sitima. Kwa hivyo tungependa kama sisi watu wa Tana River hatupati manufaa kutoka mto Tana, tungependa hata haya maji ambayo yanafungwa na yanakuwa controlled yasiwe controlled, sisi tupate mashamba yetu. Nikimalizia, nikimalizia, the electricity generated from River Tana water benefits other district vile nilisema and not Tana River.

Jambo lingine, Bwana Commissioner, traditional pastoral cultures must be accepted. Zamani watu wetu, wafugaji, walikuwa wanatembea na mkuki, kisu arrows kuchunga mali yao lakini sasa imekuwa ngumu mtu hawezi akatembea na kisu, hawezi kutembea na mshale na hana uhuru wa kutembea nayo, na wanyama wao ndiyo hao wanyama. Kwa hivyo tungependa kuwa

na access ya kutembea na kitu kama hicho.

Jambo lingine, Screening Cards. Screening cards, hizi cards nyekundu is un-constitutional – there is nowhere in the Constitution of Kenya mwananchi wa Kenya awe na ID hii ya screening card. This card wakati ilikuwa introduced, it had a purpose and I don't know the purpose but, ki -Katiba tulijaribu kuwasiliana na wanasheria, it is not in Kenya's Constitution. Kwa hivyo tungependa hiyo card nyekundu iwe scrapped haswa area yetu huwa kwamba unless you produce that card watoto wetu hawawezi kupata kitambulisho. Kwa hivyo that card must be scrapped. Bwana Commissioner, this is the only chance tunapata tafadhali nakuomba unipatie nafasi kidogo.

**Response:** Summarize

**Hussein Farah Waju:** I am almost summarizing. We should have Islamic Bank operating in Muslim areas as other banks are charging interest rates na sisi Kiislamu interest is prohibited in our religion. Kwa hivyo tungependa Islamic Banks – tuwe na Islamic Banks ambazo hazitozi hizi riba. Jambo lingine ambalo sisi Waislamu tunapata shida ni kupata Birth Certificates, na Passports, hata wakati sisi tunaenda kuhiji Mecca tunakua na shida sana. Tunakuwa classified kama sisi si wananchi wa Kenya. Kwa hivyo Katiba mpya hii tungependa itulinde kama wananchi wengine wa Kenya. Waislamu wasibaguliwe, tuwe na access ya kupata Birth Certificates na Passports without any condition like any Kenyan.

Nikimaliza, President's terms, ziwe only two terms and not more than that. President powers iondolewe kabisa na the President should not be above the law. President should not be the Commander –in – Chief of the Armed Forces, he should only be the President of the country. Mwisho Commissioner, terms of prisoners being in prison remands should be one month only. Sababu mimi nasema hivi kuna watu wanawekwa prison remand for six months, wakati wanaletwa kortini wanaambiwa kwamba consent ya ku accuse is not achieved from the Attorney General. Hiyo ni colonial terms. Tungependa mtu kama yuko na hatia, apelekwe kortini ahukumiwe kama kuna jambo. Kama hakuna awachiliwe huru badala ya kuweka watu ndani ya custody for six months kusemekana AG, AG . Kwa hayo machache thank you very much.

**Com: Prof. Okoth-Ogendo:** Bwana Farah you don't want the President to be the Commander in Chief of the Armed Forces, who do you want to be the Commander in Chief?

**Hussein Farah Waju:** Nimesema President kwa vile yeye ni mwana siasa, ana deal na siasa, na mambo ya jeshi haiambatani na siasa, napendekeza Commander in Chief awe Chief of General Staff who is also an Army Officer. Thank you very much.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Thank you very much. Diriye,

**Hajir Sheikh Diriye:** Kwa majina naitwa Hajir Sheikh Diriye, ningependa kutoa maoni namna hii. La kwanza ningependelea wananchi wote katika Kenya wa declare their wealth, yaani kila mtu aseme ni mali kiasi gani akonayo. Hii, Bwana Commissioner, imeleta shida kubwa maana utaona tu mtu amepata mali haswa kwa mambo ya corruption, kesho nijirani yako,

amevamia ardhi yako, ameiba pesa, amejenga magorofa hapa. Sasa haswa hujui mali hii alizitoa wapi. Kwa hivyo katika Constitution kila mtu aeleze wazi haswa mali yoyote au nyumba yeyote akijenga, wananchi wawe na uwezo wa kuuliza yeye hii mali umetoa wapi, umetoa kwa Benki gani, umetoa kwa salary yako na kadhalika. Haswa kila mtu a declare wealth yake.

**Interjection:** Kila mtu?

**Hajir Sheikh Diriye:** Kila mtu. La pili ningependa kuchangia mambo ya taxes au ushuru ambaye Serikali ya wilaya inarokota Bwana Commissioner ningependa kuweka mkazo haswa ushuru wewote katika District ambayo unakuwa collected na Local Authorities – haswa 80% iwe kama basic needs kwa watu. Nasema hivi, kila district, nikiongea haswa katika Tana River naweza kusema ule ushuru ambayo unakuwa collected katika district, unaweza kuajiri watu wa sehemu hiyo, kupewa kama mshahara na hiyo pesa bado ibaki kama watu hawatatumia kufanyia ufiisadi ingine. Kwa hivyo nataka Constitution mpya, kila wilaya katika Republic ushuru wowote ambao unatoka kwa rasilmali yao watu wenyewe wapewe hiyo pesa as a basic need.

Ningependa pia kutilia mkazo upande wa Lands. Watu wengi wameongea upande wa lands lakini mimi ningependelea kusema, land katika Tana River ni mzuri vile mimi ninaonelea kugawanya ardhi. Maana ardhi ikigawanywa, hatutapata shida kama zilizotoka hapa. Land, nakuambia immigration imezidi katika Tana River, sasa hata population ambayo ya locals ambayo ilikuwa hapa zamani, miaka kumi iliyopita na wale wako hapa immigrants, unaona immigrant population ndio wako zaidi. Na land, ikigawanywa, makosa kama haya hayataokea. Kwa hivyo tunaomba Serikali ipitishie mkazo igawanye ardhi kwa wananchi wenyewe hapa.

La mwisho ningependa kuwaomba Commissioners, tumeongea maneno mengi hapa au watu wa Tana River maoni yeyote ambayo wanatoa hasa ya Bura Constituency, tunataka kuona ile Draft ambayo mukitoa maoni ya watu wote iwekwe katika board useme haya ndiyo yale maoni yenu kutoka Bura Constituency na sisi tutapeleka mbele haya. Hiyo tunaweza kuamini kwamba maoni yetu yamepelekwa au tumehusishwa katika Katiba. Kwa hayo machache asante.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Thank you Bwana Diriye. Let me explain this Bwana Diriye, after we have finished there will be a Bura Constituency Report which will be prepared by the Commission. That Report will come back to you so that you can verify whether we have accurately recorded what you have stated. Then there will be a National Report for the whole country which will also come back to you here. For sixty days (60), you will be able to discuss it and then the Commissioners will come back to you at your Provincial Headquarters to discuss the National Report plus the draft Constitution. So there will be enough time for you to verify that what you have told us has been recorded. Commissioner, you want to say something else?

**Com. Bishop Njoroge:** Nafikiri kama vile Bw. Chairman Prof.Ogendo amesema ile sheria ambayo imetuweka kama Commissioners imesema kwamba tukimaliza kuchukua maoni ni lazima tuandike Report ya Bura Constituency na tuandike Report ya nchi nzima, na ni lazima hiyo Report ya Bura Constituency na ya nchi nzima iletwe hapa kwenu, muiangalie siku sitini

(60), muone kame yale maoni muliolea yamefanya nini, yameandikwa. Ile shida munasikia tukiwa nayo kati ya wanakamati wa Tume hii na Bunge ni kwamba tunasema hauwezi kuondoa kwamba tusilete ripoti hiyo kwa wananchi ili waone kwamba vile walivyosema ndivyo yamefanya nini – yameandikwa, ikiondolewa ni kwamba watu hawatajua kama waliyoyasema imefanya nini – imeandikwa. Na ndio kile tuna sema tukiharakisha ni kwamba ni lazima tuondoe hiyo.

Jambo la pili, ili muweze kuelewa mukisikia Commission ina sema hivi na wabunge wanasema hivi kunakitu tunasema tukiharakishwa ili kwamba tusiwalettee hiyo report watu watakaoumia ni akina nani?

**Response:** Sisi

**Com. Bishop Njoroge:** Wabunge wataenda katika kura na watapata viti vyao lakini kile kitaumia ni Katiba, kwa sababu tusipofanya Katona wakati huu hakuna wakati mwingine wa kufanya nini – wa kufanya Katiba. Nilitaka kuwaeleza hivi ili mukisikia mambo mujue shida iko wapi. Sawa?

**Response:** Sawa

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana Bwana Commissioner Sasa Bwana Galgalo. Endelea Bwana Galgalo.

**Uwes Galgalo:** Kwa jina naitwa Uwes Galgalo na ninataka kutoa proposal kama hizi. The Constitution shall create clear check and balance between the three arms of the Government, that is Parliament, Executive and the Judiciary. They shall have equal powers such that one is not stronger than the other and the powers be clearly defined and administered in the new Constitution. The President shall not be above the law and the criminal proceedings shall be instituted against him while in office. A Presidential candidate must garner 50% of the votes cast in the whole country, and the minimum 25% votes to be acquired from five (5) out of the eight (8) Provinces shall be abolished. There shall be an Electoral Commission. The Chairman and the Commissioner shall be appointed by Parliament and they should elect the Vice-Chairman among themselves.

Election year, months and dates shall be known to all Kenyans just like national days and powers to dissolve Parliament shall be vested in the Speaker of the National Assembly. All appointments like Chief Justice, Permanent Secretaries, Heads of Parastatals and Ambassadors shall be made by Parliament. Screening Card shall be scrapped in the new Constitution since it has subjected the youths from Wardei Community to a lot of suffering when acquiring national Identification Card. The three miles border across River Tana should be maintained and the NEP residents who are currently living shall pay (in audible) to Tana River County Council. The pastoralists in Tana District and the minority tribe like Malakote, Munyoyaya, Wata should be given at least Kenya Shillings Fifty Billion (Kshs.50B) for twenty years from the consolidated funds to cash up tribes in the country. This money will be used on education, health, road network, clean water and electricity.

The Kadhi's Court shall be named Muslim Sharia Courts and allow to prosecute criminals from Muslim-dominated district. Currently, Kadhis have nothing to offer Muslims apart from divorce cases and marriages. Kenya Wildlife shall compensate people killed and farms destroyed by the animals. Currently, they give only thirty thousand (30,000/-) for any life lost after ten



years' complaint and nothing for farmers. I propose that for human life they should compensate between Kenya Shillings five hundred thousand (500,000/-) to one million (1,000,000/-), for farmers they shall pay between one hundred thousand (100,000/-) to five hundred thousand (500,000/-) depending on the destruction caused to the farm. For livestock they should compensate the following:-

Goats & Sheep - Kenya shillings, four thousand each

Cattle – twenty thousand each

Donkeys – eight thousand each

Poultry – five hundred

Camels – thirty thousand.

This compensation should be done three months after reporting the incident to the concerned officers. Otherwise, the Constitution should allow the killing of wild animals if there is no compensation offered. Our circumsion .....

**Interjection:** Please summarize.

**Galgalo:** Yes Sir. On circumsion, wananchi should be educated before banning circumsion for women. Nominated MP's should be given to minority tribes like Wata, Wardhei, Munyoyaya, Orma and Malakote. Thank you very much.

**Com: Prof. Okoth-Ogendo:** Thank you very much Bwana Galgalo. Omar Aideed

**Omar Aideed:** My name is Omar Aideed, I am representing the pastoralists and marginalized community. Nataka kusema hivi. The Constitution should provide the pastoralists and marginalized community with basic rights enshrined in the covenant of economic, social and cultural rights and also in the field of civil and political rights. The responsibility of natural resource should be under the resident control, ie. lands, parks, minerals. The vacancy for employment should be set aside for pastoralist and marginalized communities in all Government Departments. There should be no Land Adjudication in all pastoralists and marginalized community lands and it should remain under their control.

Kwa upande wa boundaries ningependekeza ibuniwe tume ambaye ita-concern with boundaries. The Constitution should contain a programme of implementing pastoralists and marginalized communities. The pastoralists and the marginalized communities, land should be privatized only under their interest. The Constitution, should protect the rights of the minority, pastoralists, the youth, women, handicapped and illeterate. The Constitution should compensate damages done by wild animals to pastoralists' livestock either to marginalized communities farms.

Nikisema upande wa Local Government. Local Government, all Councillors must be elected. One of the qualification. The other one is Councillor should have at least a minimum qualification of 'O' Level education. The Local Authority must be empowered to hire and fire all employees. Funds collected in Local Authority should be used within the Local Authority area. Another point is that where a Local Authority or a Councillor fails to efficiently managed the affairs of the Local Authority, two



third (2/3) of the residents should petition the Constitution to Court for the dissolution of the said Councillor and hold fresh elections. The same as MP. That's all thank you.

**Prof. Okoth-Ogendo:** Thank you very much. Bw. Hussein Dhadho.

**Hussein Dhadho Takano:** Jina langu ni Hussein Dhadho Takano. Kwanza kabla pengine sija endelea ningependa kushukuru Commissioners kwa kazi yao ambayo kwamba wanafanya, na ningependa kusema ya kwamba sisi pia tumefurahi ya kwamba muko hapa. Na yale maoni yetu tutatoa tunatarajia kwamba pengine yataandikwa na kuhifadhiwa vile tunavyosema. Pia niko na ombi. Mnavyoona hapa wale ambao kwamba tunaweza kujieleza vizuri wako wachache na ningependa pengine hawa wapewe muda wa kutosha ili waweze kujieleza.

Pendekezo langu la kwanza ni kuhusu mambo ya ardhi. Katika Serikali yetu kuna ardhi ya Serikali ambayo kwamba ni State land, na pia kuna ardhi ambayo inasimamiwa na Councillors ambayo ni Trust land. Ningependekeza, kando na hizi ardhi mbili, kuna ardhi ambazo kwamba ni za jadi kulingana na jamii zetu. Ardhi ambazo kwamba ni za jadi, nazungumzia kuhusu ancestral land. Ardhi kama hizo ningependa uwezo upatiwe wazee kwa sababu katika kila jamii hasa jamii zile ambazo kwamba zinaishi katika wilaya hii, wako na wazee wa mji, ambao ni council of elders wapatiwe uwezo wa kuweza ku-manage hizo ardhi na waweze kuzitumia vile wanavyotaka. Kulingana na hayo ambayo kwamba nimesema tunavyozungumza sasa hivi, kuna ardhi mingi ambazo kwamba ni za jadi na watu wetu walinyanganywa kwa sababu ya udhaifu wao wa kifedha, ama kwa sababu ya udhaifu wao wa kisiasa. Ningetaka Katiba hii ambayo tunaiandika sasa ichukue uwezo, ni maoni yetu tutatoa, kwamba zile ardhi ambazo ni za jadi, na zimechukuliwa kutoka kwa watu wetu, kwa njia moja au nyingine, zirudishwe kwa wenyewe mara moja.

Jambo la pili, ningependa kuzungumzia jambo ambalo kwamba kila mtu alilizingumzia hapa na hili ni jambo kuhusu mambo ya mipaka. Historia inatueleza ya kwamba, mwaka wa elfu moja mia nane themini na mbili (1882) katika nchi ya Wafaransa kulikuwa na mkutano huko ambao uliitwa Berlin Conference. Conference kama hiyo ndiyo ilikaa katika kitu ambacho kilitwa Scramble for Africa. Walikaa hapo, na hapo ndipo walijadili namna Africa itagawanywa na itawekwa hiyo mipaka. Kwa hivyo kujibu lile swali lilikuwa limeulizwa, ni kwamba hizi mipaka ambazo kwamba tunasema ni mipaka ya kikoloni, ilianzishwa katika mji wa France, Berlin Conference, ndiyo walikaa wakajadili na wakagawanya hizo sehemu kulingana na vile wao wangependa kutawala nchi. Kwa hivyo hiyo mipaka ya three mile strip, baina ya sisi na mandugu zetu ambao kwamba wako katika Mkoa wa Kaskazini, ibakie hivyo hivyo.

Na pengine nikiendelea kuelezea kidogo, katika mwaka wa elfu moja mia tisa sitini na nne (1964) kulikuwa na Commission ambayo ime-set up inaitwa NFP Boundary Commission, ambayo kwamba Chairman wa hiyo Commission alikuwa anaitwa, saa hii amekufaa, anaitwa marehemu Suleiman Jaba na Secretary wa hiyo Commission alikuwa Hassan Shoro Awodha. Na walipendekeza pia katika mapendekezo yao ya kwamba three mile strip iwe ndiyo mipaka kati yetu na wenzetu katika Mkoa wa Kaskazini Mashariki.

**Interjection:** (inaudible)

**Hussein Dhadho Takano:** Inaitwa N.F.D Boundary Commission. Miaka wa 1964 na hiyo reporti munaweza kupata katika Government Press Publication, Nairobi.

**Interjection:** (inaudible)

**Hussein Dhadho Takano:** Right, right that's what I am saying. Then, jambo lingine pengine kuielezea kuipeana nguvu hili neno la kwamba mipaka yetu ibakie hapo, ningependa kwamba Commissioners, mukiniruhusu, pengine nikiwapatia historia kidogo ya kuhusu hii town ya Garissa ambayo kwamba iko katika Mkoa wa Kaskazini saa hii. Garissa, inatokana na jina la wakaazi wa Tana River ambalo kwamba linamaanisha ni 'Gariso', ni jina la mtu, na Gariso ni mnyama ambaye kwamba anaitwa squirrel. Gariso means squirrel. Na jina la Garissa lilitokana na hilo jina. Na pengine nizungumzie mji kama Mbalambala, ambao kwamba saa hii uko katika mkoa wa Kaskazini Mashariki. Mbalambala linatokana na jina la mti ambao kwamba unaitwa 'mbalambale', na pia ni jina la mtu wa wakaazi wa Tana River. Na pengine pia nizungumzie town kama Ijara, ambayo kwamba inamaanisha 'kujenga' kwa lugha yetu. Kuna Hulugho ambayo kwamba inamaanisha 'to go through'. Hizi zote ni lugha za watu wetu. Yaani kile mimi ninazungumzia hapa ni kwamba hizi towns ambazo kwamba ziko katika Mkoa Kaskazini Mashariki kwa njia moja ama nyingine inaonyesha kwamba ziko katika mipaka ya Tana River District. Kwa hivyo hata kama saa hii tukisema pengine tunadai tuseme Garissa irudi katika chini wa utawala ya Tana River basi sisi nafikiria tutakuwa sawa. Pia ningependa,

**Interjection:** (inaudible)

**Hussein Dhadho Takano:** Bwana Commissioner, hizo ni pointi mbili peke yake, lakini nitajaribu. Pia ningependekeza kwa hii Katiba mpya ambayo kwamba tunaitaka kuiunda sasa, itambue, na iheshimu jamii zile ambazo kwamba zinaishi kando kando ya mto. Na watambulike kama wao ndiyo the rightful owners and custodians of the River. Pengine nitapeana historia kidogo, ukiniruhusu. Katika mila za jamii zetu, kuna umbilical cord ambayo mtoto akizaliwa huwa inakatwa. Kwa kimila hii umbilical cord baada ya kukatwa kuna mtoto akiwa katika tumbo ya mama yake symbolically hapo tunamaanisha basi watu wa Tana River wangukuwa fed through that River. They are bringing the linkage between the river and the baby in the same way as the umbilical cord does for the young baby.

Pia ningependa the ownership, ownership ya mto kwa sababu kama jamii kama Munyoyaya kwa mfano sisi tunasema sisi tunaita mto huu ambao tuna ita mto Tana, tunaita Galanmaro, jamii kama Malakote kwa mfano wanaita Chanamar na Pokomo wanaita Sanamar, yaani wote wanaeleweshwa hapa kwamba huu mto ulipeanwa hilo jina baada ya mtu ambaye kwamba anaitwa Maro. Kwa hivyo ningependekeza pia, badala ya sisi tukuwe na Tana River District, ikuwe Tana District, badala ya Tana River District. Kwa sababu kuna river zingine pia ziko katika Kenya, kama mfano Nyando, ambayo ni District, pia imekuwa named baada ya River Nyando lakini haijaitwa River Nyando District, iliitwa Nyando District. Kwa sababu kulingana na mimi naelewa kwamba pengine ukisema Tana River District itaaleweka kwamba ni district in the river, so ni kusema kwamba hakuna pengine

hiyo Tana River na ndiyo sababu tunakosa vitu kama electricity, na tunakosa mambo mengine.

Bwana Commissioner, ningependa, jamii, kwa sababu sisi ndio tuko na uwezo wa kuchaguwa mtu tunataka na sisi ndio tuko na uwezo wa kukataa yule mtu ambaye tumemukataa, ningependa Constitution iwe very clear on that, watu wapatiwe mamlaka ya kutosha, iwe katika Katiba kwamba tufute mtu yule ambaye kwamba tunaona hatufai na tumuweke yule mtu ambaye kwamba tunaona anatufaa. Nitaendelea zaidi lakini vile niliambiwa ni wache kidogo pengine nitakua na muda zaidi, ningenyamazia hapo.

Asante sana Bwana Commissioner na wengine.

**Com: Prof.Okoth Ogendo:** Bwana Dhadho,Tana River is the largest River in the Country - and it goes out into the sea through Lamu?

**Hussein Dhadho Takano:** Right.

**Com: Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Why do you want to own such an important national asset? Why should we declare it as an asset that belongs to the entire Republic of Kenya?

**Lalafu Gatu Hake:** Prof. anauliza ya kwamba mto Tana unaanza kutoka Central Province kupitia Eastern, Tana River na unaenda unaishia huko Lamu na ni mali ya Taifa nzima, na Bwana Dado anataka watu wa kando kando ya mto Tana waumiliki wao badala ya Wakenya wengine wote ambao wanautegemea. Swali lake ni hilo Professor.

**Hussein Dado Takano:** Asante sana Professor. Pengine sijaeleweka kidogo, sisemi mto Tana umilikiwe na jamii ambazo kwamba zinaishi kando kando ya mto. Kile ninasema lazima kuwe na touch baina ya ile community ambayo inaishi hapo na huo mto. Yaani kuwe na uhusiano wa karibu. Wacha sisi tufikirie kwamba mto, kwa vile katika historia yetu na mafundisho yetu ni kwamba mto ni kitu ambacho kwamba tunajihusisha nacho, we socialize. Tuko na hiyo social relation na mto. Ukiitwa pengine, ukiitwa na jina la mtu kwa mfano, kwa sababu ni vile historia iko, basi sisi tutasikia uzuri zaidi. But not necessary kwa sababu ati tunataka ownership ya mto.

**Interjection:** ..... (inaudible)

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana, please register, andika anwani yako kule. Bwana Duri, Wari Duri, sorry Guyo. Kunyo Guyo.

**Kunyo Guyo Jema:** Mimi jina langu Kunyo Guyo Jema. Kwanza nashukuru kwa leo sisi anakutana hapa mtu anakuja kutoa yale maoni yake. Na kila mtu anakuja, mwingine ana maoni mbili, tatu lakini mimi nina maoni kumi. Katika yale maoni yangu kumi.

**Interjection:** Eh! Fupisha, eh?

**Kunyo Guyo Jema:** Katika maoni yangu kumi mimi nitafupisha. Siwezi kuzungumza vile yalivyo. Kwanza, sehemu ya kwanza nitaanzia Government, naanzia Rais, maana Serikali ukianza lazima tuanzie Rais. Kwanza katika sehemu tufuate mtindo wa mseto ambapo mamlaka ya Rais na mamlaka ya nchi yagawanywe baina ya Rais na Waziri Mkuu. Ukiwa unauliza mimi sababu nitaweza sema lakini mimi ninasema kwa ufupi. Asante.

Sehemu ya pili, Katiba inasema kuna haki ya bunge, uhuru na kabila ndogo na kabila kubwa. Ikiwa kama vile makabila kubwa na kabila ndogo tuko pamoja, haki ni sawa na kila mtu. Lakini ikiwa uchaguzi unakuja, ni watu wengine wanasema mbele yangu, kabila zingine zinaweza kupata wabunge hata kumi. Hawa hawa, wakati tena wakugawa haki hata sehemu zingine ambazo unaweza kugawa kwa wabunge maalum hawa hawa tu tena wananyakuwa. Wale wengine kama sasa uhuru miaka thelathini na tisa (39) wengine hawajaingia bunge. Kweli iko haki?

Ingingine jina kabila ndogo lakini ni kubwa kama Tana River inamezwa na Pokomo, Munyayaya, Malakote, Wata, hakuna katika kabila linaitwa Adha. Hawa Adha sisi natoka Somalia, sisi wakoloni wanaweka namna hii. Meru, Embu na kabila zingine ziko upande huo nimesahau jina lao, tharaka, Mbeere halafu tunakuwa na Munyoyaya, Wata, Malakote, Pokomo huko huko chini. Ni nini wakati Kenya huru, sisi tunakuwa Adha? Wakati wa uhuru sisi tunakua Adha, kwanini sisi tunakua Adha. Wakati tulikuwa tunapata uhuru tulikuwa sisi Garissa hii ndiyo Gorisa. Ile Gorisa ile mchanga leli, hawa watoto hawajui. Garissa wakati wanajenga wanaanza nineteen thirty (1930) lakini mzungu anaingia kutoka nineteen twenty (1920) wao wako. Lakini kujenga na (in audible) anajenga nineteen thirty (1930) na wakati ule mimi niko hai. Kwa hivyo Garissa ni yetu halafu wakati wa uhuru watu wengine wanasema sisi tunataka Somalia na sisi tunataka Kenya ndiyo sisi tunapigana. Ndio sisi tunarudi Tana River. Wakati sisi tulirudi Tana River, kabila zote sisi tanawacha Garissa, sisi tunakuwa Pokomo. Hakuna orodha ya Serikali, hakuna orodha ya vitambulisho, sisi tuko hapa hapa kama (in audible). Kwa hivyo katika Katiba hii mpya sisi tuingie katika kabila za Kenya. Ikiwa wewe ni Munyayaya, ukiwa ni Pokomo, ukiwa ni Wata, ukiwa ni Malakote, akuje jina aingie kwa kitambulisho katika Kenya haki sisi tupate. Ndio vile vile katika bunge, kama sisi hatuingii bunge, ile bunge maalum tuna haki ya kuingia, kiasi ya kusoma. Hii ni moja. Ile namba mbili.

Namba tatu, mimi ninafikiri najumuisha yote pamoja kama vile namba tatu na ni juu ya kuajiri watu. Katika kabila anakuja Kikuyu anaandika watu mia moja katika majeshi, au polisi au hamsini na kabila zingine kumi au ishirini, lakini sisi nakuja Tana River jina ya Pokomo peke yake. Wakati jeshi inaandika, sisi hatupo, wakati AP inaandika sisi hatupo, wakati ya Polisi sisi hatupo. Hatuna ofisa yeyote katika majeshi au nini. Kweli katika ile Katiba ya mbele, sisi tuko na haki? Kwa hivyo Katiba hii sisi ni lazima jina la kuandika katika District, jina letu lije kamili, kabila hilo ataandika watu tatu, watu ishirini aweke kama ile kawaida kabila Kenya. Hii ndiyo kwanza yangu, mimi nitazungumza kwa ufupi, ufupi.

**Interjection:** Fupisha.

**Kunyo Guyo:** Nitafupisha. Jambo lingine, haki ya mpaka. Katiba ile ilikuwa ya ukoloni iliweka boundary ya Kenya ya

madola na toka huko akaja kwa District. Wakati anaweka District sisi tulikuwa maili tatu Tana River. Wakati Mc Millan na Doctor Nkurumah walikuja wakati ule tena ile ile boundary iliyokuwa imewekwa - Nani hamjui Doctor Nkurumah, nani hamjui, Mc.Millan wakati anakuja Kenya. Wakati huo sisi tulikuwa majeshi. Wao walikuja kuona maoni ya watu wa Garissa na watu wa Tana River. Ule ndio wakati sisi tuligawa tukaja upande huu tena. Kwa hivyo ile boundary, hata Katiba ya Kenya iko mahali pale, hata hii Katiba mpya inakuwa hivyo. Ni vile mama mmoja alisema. Ninyi mtasikia ikiwa mnakaa na radio huko, watu wa Tana River na watu wa North Eastern wameuwana, wamefanyana, wamefanya nini, juu ya nini? Juu ya huu mto. Kwa hivyo kama watu wanataka kuzidisha sisi tupigane, usongezwe. Mimi naambia nyinyi, lazima sisi tutatoa damu. Uhuru unapatika kila mtu kwa Location yake, kwa District yake. Kwa nini uhuru ya Tana River unakuwa wa watu wengine? Town ilikuwa yetu sisi tuliacha, tukaja sisi tukaweka Madogo tena. Mimi ni Councillor ya Madogo. Mimi ndiye niliaanzisha. Hakuna skuli hakuna nini, hii ndiyo sisi tunafanaya. Kwa hivyo mpaka usikuwe moved, hii ndiyo mimi nasema.

Haki ya Mahakama. Hii mahakama, nikiua mtu mimi ninyongwe, au nihukumiwe mwaka. Ukikosana na mtu ni lazima aingie jela baada ya siku kumi baada ya shiku ishirini ahukumiwe. Hiyo exhibit miaka yote wanaangalia mpaka miaka mbili mtu anakaa rumande - aa hakuna kitu we enda. Huyu mtu ashakufa, familia yake imekufa, hii ni haki gani? Katiba gani? Kwa hivyo Katiba mpya mtu ukishikwa baada ya fourteen days (14) kama makosa hayo hakuna, atoke. Wale experts kwa nini hao hawakusoma, ni kwa nini miaka mbili mtu anakaa katika jela? Hiyo amefungwa hata kama anawachwa. Kwa hivyo haki ya mahakama katika Katiba sisi tupate.

Mila. Mila ya ukabila, mimi ninasikia, hata kama unazungumza Kingereza Bwana Prof. Sisi tunazaliwa na desturi, iko desturi zingine za kishenzi kabisa. Lakini ile desturi yetu kama ni Wakristo, wana desturi yao, kama ni Islamu wako na desturi yao. Kwa hivyo unasema wacha desturi yako ufuate Kizunguni, na sisi ni Afrika, ni lazima hiyo mila yetu iheshimiwe katika Katiba.

Hukumu ya ardhi, mashamba. Mimi niko na shamba, babu na babu na babu, halafu vile sasa watu wanasema watu wanahamia, ukikuja shamba langu anakuja yeye anakata, anakwenda kwa Council anapata barua, anasema yeye ako na barua shamba langu linachukuliwa. Mimi kwenda mahakama, yeye anachukua wakili, wazee wale najua wote, wanazimwa. Huyu maana ana pesa anapata haki. Kwa hivyo haki ya shamba wazee wa nchi hii wahukumu shamba ili watu wajue lilikuwa la nani, wazee wahakikishe.

**Interjection:** ..... (inaudible)

Hii ndiyo haki tunayotaka sisi katika Katiba mpya. Kesi ya shamba ni lazima iwekwe katika Katiba mpya. Kwa hivyo unajua sasa mtu akisema maneno namna hiyo lazima yale alikuwa anafikiria yatazimika. Kwa hayo mafupi, mimi nitamaliza hapo. Asante sana Bwana.

**Interjection:** Asante sana Mzee. Mimi nimeombwa na Professor niseme jambo moja tu kwamba aduhuri imefika, ikiwa kuna mtu anataka kwenda kuswali, tafadhali utoke tu uende uswali halafu urudi. Shukran.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana - Bwana Aden Ibrahim.

**Adan Ibrahim Arale:** Kwa jina naitwa Adan Ibrahim Arale, natoka Bangale Division. Mimi langu ambalo nitaanzia la kwanza ni kuhusu hii pesa ambayo wale wafadhili kama NGOs na Serikali inatoa kufanyia miradi kwa wananchi. Hii pesa huwa inatolewa juu ya wananchi, na wananchi wenyewe haifikii kamwe. Kwa hivyo katika hii mambo ya Katiba mpya tunataka mahali ambapo miradi inafanyika wananchi wenyewe wahusike, hiyo pesa wao wenyewe wapewe jukumu, wawe katika hesabu, waone mali yao kama imewafanyia kazi ama bado. Pia mambo ya Waislamu, katika sherehe ya Islamu iwe imesajiliwa katiba Katiba ya Kenya kwamba ni mambo ya kurithi, na mambo ya kuoa na mambo mengine ambayo wewe una jukumu kama wale majaji wengine ama haswa mtu achaguliwe Muislamu katika bunge ambaye anasimamia maslahi ya dini ya Kiislamu ambaye anajulikana yeye ndiye analinda dini ya Kiislamu katika hii Katiba ijayo.

Mambo mengine ni wabunge tunaowachagua na ma-Councillors mimi mwenyewe ningependa wananchi wenyewe wapewe jukumu fulani ikiwa mjumbe, councillor na watumishi wa umma ambao wanaitwa watumishi wa umma. Wao wenyewe hawajui yule mtu ambaye amewaajiri. Sisi ndio tunakuwa watumwa. Sisi wananchi, wao wako juu yetu, wao ndio wako na nguvu kuliko sisi na huku tunawaita watumishi wa umma. Watu kama hao tupewe jukumu katika hii Katiba ijayo mpya tuwe na uwezo wa kuwafuta na kuwaadhibu wao. Kama mjumbe amekosea, kama councillor amekosea, ametumia mamlaka yake vibaya, kama ametumia ardhi ya wananchi kwa njia mbaya ambayo amegawanya ovyo ovyo ama ameuzi kwa matajiri, tunataka yule councillor tupewe hii Katiba ijayo itupatie sisi kifungo ambacho wananchi wako na uwezo wa kuondoa watu kama hao.

Pia mambo ya ardhi, kuna Kora, Michelelu, Galana na Tsavo East. Hii ardhi ya Tana River imeporwa zaidi na imepatiwa watu wengine, imewekwa baina ya wale Wakenya wengine, kama sasa National Park, kama sasa nini yote, na sisi hatuna faida na wakati ardhi hii ilikuwa alikuwa inatengwa sisi wenyewe hatukuhusishwa. Kwa hivyo tunataka Katiba mpya hii irudishe hiyo haki yetu kwa mikono yetu ili sisi wenyewe tuwe tunapata manufaa kutoka pale ama hiyo ardhi irejee kwa mikono yetu ili sisi wenyewe tuitumie kama mali yetu ya Tana River.

Hati ya kusafiria nje, tunataka iletwe katika wilaya, na katika locations vile vipande vinatolewa katika division hata hiyo hati iletwe kuliko mwananchi anayetoa kodi kwa Serikali yake anaenda kusafiri kwa hiyo huduma kidogo kutoka hapa mpaka Nairobi mpaka atafute maelfu kadhaa ya pesa. Kwa hivyo hiyo hati ya kusafiria iletwe pamoja na kipande, vile vipande vinatolewa katika mahali ambapo wananchi wenyewe wako karibu na wao, hiyo huduma wapate. Iwekwe katika hii Katiba ijayo mpya hiyo hati ya kusafiria iletwe kwa wilaya, iletwe kwa division, halafu ije karibu na wananchi.

Langu la mwisho ambalo nitafupisha, ni mambo ya kutahiri wasichana. Hayo maneno yameleta hatari, na kuna ugonjwa mbaya siku hizi ambao unaenea na hata dini ya Kiislamu imekataa. Hiyo mambo nataka Katiba mpya isimamishe tufuate vile dini inatuamrisha na maamrisha ya Serikali hayo mambo ya kutahiri wasichana isimame.

Asanteni.

**Com. Prof. Okoth –Ogendo:** Asante Bwana Aden. Sasa mwenyekiti wa County Council.

**Abubakar Salat:** Ahsante sana Bwana Commissioner. Ilitajwa kwa wingi sana haswa kuhusu mambo ya ardhi ningependa kuhakikishia Commissioner kwamba .... Oh kwa jina ninaitwa Abubakar Salat Garacha, ni kijana wa hapa Madogo Division, kwangu ni hapa hapa Madogo, ni Chairman wa Tana River County Council. Ninasema ilikuwa imetajwa sana kuhusu mambo ya ardhi haswa kuhusu sehemu ya Tana River, nawahakikishia wananchi, ama ningependa kutoa maoni yangu kwamba ardhi kweli ni ranches mingi zimebuniwa katika wilaya ya Tana River na hiyo imesababisha upungufu haswa kwa wale watu wa mifugo, kuweza kulisha sehemu mbalimbali. Kama vile mfano nikitaja sehemu kama Galana, nikija tena Darso Godana, nije sehemu nyingine kama Mchelelo, ama Kora Game Reserve. Hizo sehemu zote ni sehemu ambazo ni nzuri sana kwa mifugo na zimekuwa ni ranches pamoja na National Parks, pamoja na Reserve. Ningependa kutoa maoni kwamba tungependa kuuliza Serikali kama vile ardhi kama Hola Irrigation Scheme, na Bura Irrigation Scheme, ipewe wananchi, wagawiwe wananchi, na wapewe title kwa kila mmoja aweze kugawiwa. Badala ya irrigation scheme isimamiwe na National Irrigation Scheme, wapewe wananchi wenyewe ili waweze kumiliki hizo ardhi kuweza kujisimamia wenyewe.

Nikija kwa upande wa Kora Game Reserve. Kora Game Reserve ni ardhi ambayo imekuwa National Park, hata haiko upande ya County Council. Kwa vile ardhi hiyo ni ardhi ya wananchi na ilikuwa ikisimamiwa na County Council, ingekuwa vizuri, tunauliza Serikali, sehemu hiyo, kuna sehemu ambazo zina wakaaji wengi wananchi wa Tana River, na sehemu hiyo itengewe wananchi sehemu moja ili Katiba ijayo iwe wananchi wa mifugo wapate ardhi ya kuweza kulisha ili ipunguke msongamano wa upande wa mto Tana kwa malisho. Kwa sababu sehemu hiyo kuna chemichemi ya maji na wakulima wa mifugo wanaweza kuendelea kuweza kulisha sehemu hiyo. Na hiyo inaweza kupunguza clashes kati ya wakulima wa mashamba ndogo ndogo na wale wakulima wa jembe.

Nikiongeza sehemu za TARDA shamba lile la mpunga sehemu za Garsen ni ardhi kubwa sana vile vile ambazo zimechukuliwa na kampuni zinazokuza mambo ya mchele. Na hizo ardhi ni sehemu kubwa sana imelala bure. Ingekuwa vizuri pia ipendekezwe kama vile nilivyopendekeza kuhusu Hola Irrigation Scheme na Bura Irrigation Scheme. Sehemu hiyo pia ipewe wananchi, wakulima wapewe title waweze kumiliki hiyo ardhi badala kuweza kukaa bure kwa mikono ya parastatal.

Bwana Commissioner, ningependa kuweza kuzungumzia haswa mambo ya maji, vile upungufu wa maji sehemu mbali mbali unatleta taabu. Ingekuwa vizuri, iweze kutengenezwa boreholes kwa wingi sehemu ya juu ya mto ili msongamano wa watu kwenda kupata kunywa maji uweze kupunguka kwa upande wa wakulima wa upande wa chini. Na ikiwa wakati borehole itakuwa ukame umeingia ingekuwa vizuri itengenezwe corridor kutoka juu - nikisema juu ni sehemu za malisho kuteremkia upande wa mto Tana. Ifanywe corridor ya hayawani kuweza kuingia kuweza kunywa maji.

Nikizungumzia tena Bwana Commissioner, upande wa mipaka, kusema kweli, mipaka ya Kenya ndiyo vile ilivyo. Sasa



tunasikia ya kwamba kuna baadhi ya sehemu nyingine inadai mipaka ya sehemu za Coast Province. Basi kama itakuwa hiyo mipaka itabadilishwa inawezekana basi iwe ni Kenya nzima, isiwe ni Tana River peke yake ama iwe ni North Eastern peke yake. Iwe ni Kenya nzima kwa sababu hii mipaka imewekwa na Serikali na vile ilivyowekwa ingekuwa vzuri ikae hivyo bila kuleta ghasia baadaye kwa sababu hiyo inaweza leta shida na ni hapa karibuni tu tumetoka kwa kisanga cha vita tusije tukazuwa tena vita vingine ambavyo hiyo mipaka inaweza kuzuwa. Hiyo inaweza kuwa na madhara .

Kitu kingine Bwana Commissioner, nikiwa nitamalizia, ni kuhusu uandikishaji wa kazi. Haswa kwa wakati huu Serikali inawapatia vijana katika uwajiri kama ni polisi, ama kama ni game wanaajiriwa kutoka kwa District. Tungeomba kwa Katiba ijayo iwe ikifanywa kwa Division, badala ya kufanywa kwa District. Kwa sababu kuna watoto wengine kama vile divisions zingine ni kama kilometers zaidi ya mia mbili (200 Kms) kutoka kwa District basi hawatoweza kuifikia mahali nafasi ya kazi iko. Vijana wengi wanakosa kazi.

Kwa upande mwingine wa mwisho Bwana Commissioner, ningependa uandikishaji ama uchaguzi wa ma-chief utokane na wananchi wenyewe badala ya kuchaguliwa na Serikali. Chief, Chief, akichaguliwa tungeomba raia wenyewe wachague badala ya Serikali kuchagua kwa sababu huyo mtu anaweza kuwa Serikali wamemchagua ni mtu wa Civil Service ama kuna wengine wanatolewa kwa department direct wanapelekwa kwa Chief, wengine wanachukuliwa kwa kazi ya polisi, wengine wanachukuliwa kwa kazi parastatal tofauti tofauti. Kwa hivyo inakuwa ni huyo mtu mara nyingi haelewi mambo ya culture yaani mila ya wananchi. Mara nyingi watu kama hao wakija kuongoza wananchi wanakuwa na taabu kwa sababu haelewi mila ya community fulani anakuja hapo anataka kutumia ule uwezo wa askari, kama vile alikuwa askari na anataka kutumia kwa raia.

Kwa hivyo ningependa kupendekeza kama vile councillors wanavyochaguliwa ama kama wabunge vile wanavyochaguliwa, chief pia achaguliwe na wananchi wenyewe. Bwana Commissioner asante sana. Kwa haya machache, thank you .

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana. Said Randu

**Said Randu:** Kwa majina naitwa Said Randu. Mimi ningependekeza ya kwamba kuhusu usalama. Katiba mpya itoke na taratibu fulani ambayo askari wanaohudumu wakati huu haswa kikosi cha polisi wajumuike pamoja na raia kwenye vijiji. Hii mambo ya kukaa kwenye ma camp katika town kubwa kubwa kuwe tu pengine na wachache ambao watakuwa kwenye ma camps na wengi wao wajumuike pamoja na raia kwenye vijiji. Kwa sababu ukiangalia sasa askari polisi, kwa crown yake imeandikwa “utumishi kwa wote” na ile attitude ambayo watu wako nayo kuhusu hicho kikosi ni kwamba hawana uhusiano. Kwa hivyo kule kuleta uhusiano wa karibu kati yao na wananchi hawa askari wapate kukaa pamoja na raia, kutunza usalama wao pamoja na vitu vyao manyumbani.

Pendekezo la pili ni kuhusu mipaka, na ilivyoenezwa, huu ukanda wa maili tatu uliwekwa tangu enzi na si jambo ambalo leo tunaweza kulikuwa na mvutano kati yake. Mpaka huo tunataka Katiba mpya iweke mkazo na ubakie hapo hapo bila ya vikwazo vyovyote ama ya kuleta madhara yoyote. Kwa sababu jamii zile ambazo zilikuwa zikitumia hiyo ardhi, walitumia kwa muda mrefu na mpaka sasa wako huko na kama tu kutakuwa na mabadiliko yoyote kidogo, basi athari zitakuwa ni nyingi.



Pendekezo la tatu ni kuhusu hao viongozi ambao wanachaguliwa. Katiba hii mpya tungependa itoe fungo fulani la kupatia uwezo wale watu ambao wanawachagua hawa viongozi. Kuliko kukaa muda wa miaka tano akingojewa huyo kama ni mbunge ndiyo arudi, akataliwe na wananchi ama akubaliwe tena kurudi bungeni, kuwe na kifungo fulani pengine ambacho kinaweza kumfuta kabla ya kumaliza huo muda wa miaka mitano na kuchaguliwa kiongozi mwingine. Na hii ningependekeza kwamba pengine Katiba mpya ipendekeze Constitutional offices za MPs, awe na afisi katika constituency na ule mda ambayo pengine huyo MP atakuwa hatakuja kupata shida ama mawazo ya wale anao wahudumia basi Speaker pia awe na uwezo kwamba wananchi waki-complain kwamba huyu mbunge wetu tangu tumpeleke haja fika hapa, basi Speaker awe na uwezo wa kumfuta na kuitisha uchaguzi mpya.

Langu lingine Bwana Commissioner, sijui kama nitakuwa niko nje kidogo lakini pia limegusiwa hapa. Mimi nilikuwa na maoni kwamba pengine kama Katiba mpya inaweza ikatoka na sheria fulani kwamba kabila zote zile ziko hapa nchini zilandikishwe tena upya ndiyo zile kabila ambazo pengine zimenyimwa haki fulani zipate kutoka nje vizuri na kujulikana. Kama vile ilivyoongelewa hapo mbeleni ni kwamba baadhi ya kabila zile tuko hapa Tana River District hatujulikani katika nchi hii na ndipo mzee fulani alikuwa akizungumzia juu ya kuitwa others. Na sisi ni Wakenya kwa nini tuitwe others? Kwa hivyo pengine kuwe na registration ya kabila zote Kenya ndiyo tupate kujieleza vizuri haswa sisi tunaitwa kabila gani. Na pengine nikifafanua kidogo, tunaona kama haswa sisi wakaazi wa Tana River tumekuwa displaced. Kwa sababu ile kabila kubwa iko Tana River ama iko katika record ni Pokomo na ndipo unaona kitu chochote kikitoka juu kinakuja na jina la Pokomo na hiyo Pokomo kwangu mimi sioni kama kuna kabila yoyote hapa anaweza kudai kama yeye ni Mpokomo. Kwa sababu kati ya Pokomo tuko na kabila tofauti; tuko na Malalulu, tuko na Malanchini, tuko na Zubaki, tuko na Malakote wako hapo ndani, ambayo hata ukiangalia pengine lugha zenyewe ziko tofauti, lakini sasa hawa watu ambao wanaitwa Pokomo wote na lugha zao pia ziko tofauti wamewekwa chini ya hiyo Pokomo. Pengine kama tutapewa uwezo sasa ya kujieleza ni kwamba Malakote pengine, tunaweza kujitoa kwa sababu tuwetunasimama tu kama kabila. Nikienda zaidi ni kwamba Malakote huyu

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Can you summarize?

**Said Randu:** Yes. Malakote ukimuuliza sasa wewe ni kabila gani, atakwambia mimi ni Malakote, na ukimuuliza kwa lugha anakwambia mimi ni Muilwana. Kwa hivyo kabila moja ambalo liko ni majina mawili hiyo haiko na hili jina la Malakote limeletwe tu na watu fulani pengine kwa madhumuni yao binafsi. Ambapo kukija mambo ya registration tunaweza kujisimamia kama Mailwana na si Malakote kama vile tu ndungu zetu Munyoyaya walijifanya walikuwa ni Korokoro na sasa wamesimama kama Munyoyaya na tungependa zitoke vizuri katika record kwamba kuna kabila zinaitwa Munyoyaya, Malakote na pengine Pokomo (ikiwa watachukua hilo jina Pokomo in general wabakie hivyo). Lakini sisi tutambulike vizuri.

La mwisho ni kuhusu hawa murder suspects. Tungependa Katiba mpya itoke na sheria ya kwamba a murder suspect huyu ni mtu ambaye hajaoneka ni anafumaniwa tu kwamba pengine amehusika. Kwa hivyo kama amehusika kwa nini kuwekwa kizuizini muda huo wote mrefu? Kwa hivyo kuwe na muda fulani, kama itakuwa na wiki mbili, kama itakuwa ni mwezi, lakini

kuwe na muda fulani ambapo investigations zinaweza zikafanywa na ithibitishwe kama ni kuhukumiwa ahukumiwa kwa court, na awekwe ndani. Otherwise kama si hivyo basi aachiliwe huru, bila vikwazo vyovyote.

Nikimalizia ni mambo ya travelling documents ambazo zilikuwa zimegusiwa. Mimi niko na maoni kwa Katiba mpya ili pengine zile kabila ndogo ndogo ziko kando kupata uwezo pia wa kupata hizi traveling documents. Mambo ya traveling documents yasiwekwe tu Nairobi lakini pengine ziletwe mpaka katika district level ndiyo wale wengine at least wawe na access to them, waweze at least kujimudu na kama ni kutafuta mtu aweze kuzipata kwa urahisi kuliko kusafiri mpaka Nairobi kutafuta hivyo vitu. Kwa hivyo kwa hayo machache nasema asante.

**Prof. Okoth-Ogendo:** Habiba

**Habiba Abanyela:** Mimi nitaongea Munyoyaya, Mimi naitwa Habiba Abanyela.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Ongea kwa microphone.

**Habiba Abanyela:** Kwanza vile nataka kuongea nafikiri watu wote wameongea sasa ni kuongeza tu, lakini nimesema mpaka uwe pale pale mkoloni aliuweka, mpaka ikuwe pale pale. Ya pili, sisi wanawake hatuna, sisi wanawake tunalaliwa, wanawake tunalaliwa. Tunataka na sisi tupewe jukumu. – Tunapewa namna gani? Wanawake wengine tunaona tunakaa vizuri, tunakula vizuri lakini kuna wengine wanaumia sana, na wanajiita wako na mabwana. Huyu bwana anayetesa huyo mwanamke tunataka achukuliwe hatua. Tunataka achukuliwe hatua na hao wanawake wanaenda kuchukua tu haya majani wanaenda kuuza ili kulisha watoto wao na baba yuko, tunataka yule bwana aadhibiwe. Na wale watoto vile Serikali inaweza kusaidia, afadhali ichukue yule mtoto ako na baba lakini baba yake hamsaidii mwanamke anateseka naye hao watoto wafanywe kama walemavu, wakuwe kama walemavu wasaidiwe.

Sasa nafikiri mimi sina mengi ya kusema. Tena kunasemekana kuna kazi, ikisemekana kuna kazi hiyo kazi inakuwa ni ya wakubwa. Watoto wetu wanatoka hapa wanaenda Hola, wakifika pengine yule mtoto amechukuwa deni ndiyo ameenda, na akienda kazi yote inaenda na wakubwa, watoto wanarudi hivyo hivyo. Nasijui ni kwa nini. Afadhali tunasema hayo mambo ya kwenda Hola yaawhwe yaletwe hapa division. Kama ni kukosa kazi akose hapa na kama ni kupata apate hapa. Hakuna haja ya kuingia gari unatoa nauli unaenda na unakosa kazi na unarudi. Na tuna ma-DO hawana masomo, na wengine wako na masomo lakini wanapata shida hivyo hivyo tu na sijui tunalaliwa na wapi. Na mimi naweza kusema pengine tunalaliwa tu na Serikali. Kwa hivyo tetezi langu ni hilo tu. .... (inaudible).

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana. Ali Guyo, Ismail

**Ismael Solola:** Mimi kwa jina ninaitwa Ismael Solola kutoka Mbalambala. Ningependa kutoa maoni yangu kwanza ninaanza na kitu kinaitwa afya. Nafikiri afya ni kitu muhimu sana ambacho kila mwanadamu lazima akuwe nacho. Na tukiangalia kila mahali saa hii Serikali inatafuta kila juhudi kuhakikisha ya kwamba kila mtu ako na afya na amepata huduma ya afya sawa. Hivyo hivyo watu wote si sawa, kuna watu ambao wako na uwezo ya kujitibu ki pesa na kuna wengine ambao hawana huo

uwezo. Kwa hivyo mimi maoni yangu ninatoa ya kwamba Serikali itoe, cost-sharing kusikuwe na cost-sharing, kwa sababu kama mimi, mfano saa hii sina chochote, na nikienda hospitali ama nikipeleka mtoto yangu hospitali, ninaambiwa nilipe shilingi ishirini, na mimi pengine sina pesa yoyote hata asubuhi pengine sijakunywa chai sijafanya chochote. Nitatoa wapi shilingi ishirini? Kwa hivyo maoni yangu ni kwamba cost-sharing kwa hospitali itolewe.

Jambo la pili ni kuhusu ardhi. Wengi wameongea kuhusu ardhi na maoni yangu ni kwamba ardhi itolewe kwa ujenzi, yaani kama ni ardhi ya kujenga itolewe kwa mwenyeji. Ninamaanisha hivi, mfano tuko Madogo hii, kuna wale baba yao, na ma-babu zao na nini wote wamezaliwa Madogo hii na leo wanakosa ardhi ya kuishi Madogo hii. Wanahamishwa kule kunaitwa, nini huko, Boji, huku Secondary na upande huo na wewe ni mzaliwa wa Madogo hii. Sasa maoni yangu ni kwamba ardhi ipewe mwenyeji awe na pesa asikuwe na pesa. Mtu ajenge ile kiasi anaweza. Akitaka alale hapo hapo nje lakini kiasi chake akatiwe alale hapo hapo. Ndiyo baadaye ardhi ikileta shida isisemekane huyu mtu hana pesa anahamishwa mahali pengine, akae. Mambo ya kuleta mtu pengine ni mgeni na ni mfanyikazi, anakuja anatoa pesa ako na fee, fee ya County Council anakuja anapewa ardhi na wewe mwenyeji huna fee unakatazwa, hayo maneno yatolewe kwa hivyo ardhi ipewe mwenyeji awe na pesa asikuwe na pesa.

Jambo la tatu ambalo ningetoa ni kuhusu vitambulisho. Zamani wakati tulikuwa watoto na mpaka kufikia hivi mwaka ya 90s vitambulisho kupatikana at least vilikuwa rahisi, kwa sababu namna ya kupata ilikuwa rahisi kupitia Chief, Location Elders ndiyo unapata vitambulisho, na zinaletwa at least hata kama ni kwa uchache at least mara mbili kwa mwaka zinazungushwa na gari. Yaani kuna kile kitu sijui kinaitwa mobile, wanazungusha wanapea watu vitambulisho sehemu za mashambani na sehemu za miji.

Lakini leo tunaona ya kwamba kama mtu anataka kitambulisho lazima pengine aende locational level ama aende District level ambayo kuwa hiyo ni kitu ngumu. Wewe unajulikana ni mzaliwa wa hicho kijiji nafikiri ni rahisi wakati ambaye wewe umepitishwa na Chief na wale village elders wewe ukishapitishwa hiyo nafikiri imetosha, mambo ya sasa kuja kwa divisional levels, sijui inafanyiwa vetting, sijui mpaka sahihi ya nani, sijui mpaka sahihi ya DC, sahihi ya nani hiyo tunaona kama Serikali inatunyanyasa. Kwa hivyo ningependa kitambulisho kitolewe vile kilikuwa kinatolewa haswa iwe isambazwe kwa locational level, hata ikizidi hata kwa sub-locational level ndiyo watu wasipate shida ya kitambulisho.

Hoja yangu ya mne ni kuhusu kazi. Kazi wakati inapotokea kuna watu ambao sana sana sehemu za Tana River wananyima watu nafasi kwa hivyo sitafafanua zaidi, tungependa kazi iandikwe ikiwezekana locational level kama si divisional level. Kwa sababu wakati kazi pengine inatangazwa nafasi ikitokea na mtu pengine ako Madogo, anatakikana kwenda Hola, huwezi kupanda gari ya mtu hivi hivi na it is a distant na lazima utapata tikiti ya kwenda. Kwa hivyo ni jambo ngumu ni lazima kazi iandikwe divisional ama locational level.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Summarize.

**Ismael Solola :** Sawa, nita-summarize. Jambo langu la mwisho ni kwamba hatutaki siasa ya pesa. Nikisema hivi, ni kwamba nafikiri hata ni hatia lakini kuna jambo ambalo linatusinya sana, sisi wananchi. Nafasi inatokea ya u-Councillor, au ya ubunge

ikishafika wakati wake wa kuchagua, raia ni jukumu yao kuchagua yule mtu wanahitaji. Lakini shida kubwa ni kwamba watu ambao wanajiweza, wenye pesa, wanakuja hapa wanadanganya raia na pesa halafu mtu anachaguliwa kutokana na hiyo pesa, mtu anaangalia kwamba yule mwenye pesa, akitoa pesa ndiye huyo. Hiki ni kitu kinaitwa bribing. Kwa hivyo ningependa katika hii Katiba ya saa hizi sheria ibuniwe, yeyote atakayepatikana akitoa hongo ama akinunua ile voting card kutoka kwa wananchi ili kupata kura ashtakiwe. Sina mengi, ni hayo machache, asanteni.

**Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana. Mohamed Ibrahim, Hussein Diba. Daudi Ali Loka

**Daudi Ali Loka:** Kwa majina naitwa Daudi Ali Loka, kutoka Madogo Division. Kabla nafikiri sijaendelea na maoni yangu ningelitaka kuuliza Commissioner swali kidogo. Sijui mumewekewa muda wa kiasi gani, kama ni mchana mzima ama ni kuanzia pengine saa moja pengine mpaka saa sita hatujui aona saa saba kwa sababu, kuna munung'uniko huko nje, kwa sababu mtu akiongea maneno mbili, tatu, anaambiwa fupisha. Sasa wakati watu walipotoka kusali kuna manung'uniko mengi kule nje na hatungelitaka Commissioners walaumiwe. Kwa sababu itasemekana wamekuja Madogo na wamekatizia katizia watu maoni. Kwa hivyo ninaomba kujua mtakaa mpaka saa ngapi?

**Com. Bishop Njoroge:** Sikia, nafikiri binadam anaweza kuishi vile apendavyo, akitaka kuishi ubinadam wa kunungunika kwa kila kitu anaweza kuishi hivyo. Nafikiri kile Commissioners walisema kama ukiniambia zile shida mumepata hapa, hiyo shida haitaenda kwa Katiba. Unasikia? Ukiniambia hapa munaenda na mguu mpaka kwa mto, hayo ni maneno hayataenda. Lakini ukiniambia hii barabara tunataka iwekwe lami, hiyo itafanya nini?

**Daudi Ali Loka:** Itafanyika.

**Com. Bishop Njoroge:** Ukiniambia tumekaa bila masomo, kwa sababu hatuna pesa, hiyo haitaenda kwa Katiba. Ukisema tunataka masomo ya bure itaenda wapi, kwa Katiba. Kwa hivyo kuna njia unaweza kufupisha na ufanye kazi nzuri kuliko kuzungumza mambo ambayo hayatafanya nini – hayatakusaidia. Kama tukisema, najua watoto wenu wanaenda mbali kutafuta kazi, mbali mpaka Hola ama district headquarters. Badala ya kusema vile wanaenda, wanaenda, wanaenda; na hawana pesa, mbona hutuambii leteni mambo ya kazi in the location. Si umeseme jambo hilo tu? You are saying the same thing but spending little time. But if you want us to give you time to tell us everything and it does not go into the constitution, is that really what you want? We are guiding you, please zungumza mambo ambayo mambo hayo yataingia kwa nini – kwa Katiba ili watu wengi waweze kuzungumza. Tukikubali mtu mmoja azungumze muda mrefu, kuna watu watatoka hapa bila basi kufanya nini – kuongoa, na ni watu wengi. Tumeenda katika Province nyingi na hakuna manung'uniko. Lakini muktaka tufanye hivyo mtu mmoja azungumze nusu saa, tutafanya hivyo, na mtaona wengine watatoka bila kufanya nini – kuzungumza.

**Daudi Ali Loka:** Ahsante.

**Interjection:** Endelea basi

**Daudi Ali Loka:** Ya kwanza katika maoni yangu ni kwamba nafikiri tangu Kenya imepata uhuru karibu miaka arubaini sasa,

sehemu zetu elimu iko chini sana, na watoto wetu saa hizi katika kabila letu hakuna kijana ambaye amewewahi kwenda university, kwa sababu elimu iko chini na mapato ni kidogo. Watu walikuwa na mali lakini imeporwa na majambazi kutoka sehemu fulani Fulani na watu wamekuwa maskini. Kwa hivyo ikiwa tutalinganishwa sisi kama wakaaji wa wilaya ya Tana River haswa part of the North na Kenya ingine, bila shaka sisi tutakosa mambo mengi. Kwa hivyo mimi kwa upande wangu ninatoa maoni yangu, sisi upande wa Tana North tupewe elimu ya bure, na kukitokea kazi isemekane inatakikana kuandikwa kijana ambaye amepita ama college fulani inatakikana kuchukuliwa kijana amepita grade yake ni ya A anatakikana pengine college ya nurses ama education, sisi ikiwa yule kijana atakuwa na C sasa hawezi kuchukuliwa kwa sababu hakuna siku pengine tutakuja kufikia hicho kiwango cha sisi vijana wetu kupata A kwa sababu ya hali mbaya ya kwetu. Kwa hivyo kwa maoni yangu ni kwamba tupewe elimu ya bure kwanzia nursery, mpaka primary, mpaka secondary na ikiwa kuna mtoto atapita kwenda university basi Serikali itutengee pesa ya kupeleka watoto wetu university. Saa hizi Madogo Secondary kuna watoto wawili wa kabila letu wamepita kwenda university lakini hatuna uwezo wa kuwapeleka. Kwa hivyo hao watoto wamekosa university, na saa hii mmoja jana alikuwa msituni akichunga mbuzi, hana baba yake, hana uwezo wa kumpeleka university. Kwa hivyo Serikali itutengee pesa katika Tana River District, katika haswa upande wa North mtoto wetu akipita kwenda university iwe kuna ile pesa ambayo itamwezesha kumpeleka university na sisi angalao tuweze kujifananisha na Kenya ingine kwa upande ya education.

Huduma ya afya. Nafikiri hapo mbeleni tulipokuwa wadogo Serikali ilikuwa inatuma magari ya mobile kuchanja watu msituni na kila pahali. Lakini tangu miaka chache za nyuma Serikali imeanzisha huduma ambayo inaitwa cost-sharing. Kusema ule ukweli, nyinyi kama wakubwa ama Commissioners ambao mumetembelea hii area, ama kuzungukia Kenya nzima kuchukua maoni ya watu, hii cost sharing imeumiza watu wengi haswa wale ambao hawana mapato. Vile mwenzangu saa hii ametangulia, utakuta umechukua mtoto umempeleka hospitali na wewe pengine mzee amehangaika amechoma makaa amepata shilingi mia moja. Mtoto ni mgonjwa amekimbisha mtoto hospitali, daktari ameandika dawa ameandika ameandika

**Interjection:** Tunajua kuna shida hizo. Ungetaka nini?

**Daudi Ali Loka:** Tupewe huduma ya bure ya medical katika hospitali.

Huduma ya Serikali. Kwa mfano kama saa hizi sisi kama wakaaji wa North Tana tunalaumu Serikali, kwa sababu kuna Katiba ile inasema Serikali inalinda nafsi yako na mali yako. Sisi kama Tana North, Serikali inaonekana imeshindwa kutulinda. Kwa hivyo tukiangalia location zetu kuna location nyingi zimevunjika since 1993 na hadi mpaka leo hakuna huduma ya Serikali, hakuna security na mpaka wa leo watu wanaishi maisha ya kichohehahe. Kwa hivyo katika hii Katiba itakayo kuja itakayo undwa mpya tunaomba katika kila location kuwe na security ya kulinda mwananchi.

Tukiingia ya tano kuhusu NSSF, kuna watu wengi wamefanya katika Serikali, na wame-retire kutoka kwa Serikali na hawajapata hiyo benefit yao hadi mpaka mtu ameaga dunia. Kwa hivyo ikiwa mtu amefanya kwa Serikali na barua yake ile ya

ku-retire imetoka, basi NSSF ilipe huyo mtu mara moja pesa yake na apate haki yake aende zake, kama ni kununulia ng'ombe aende, kama nikulewa aende alewe, na akufe aingie karibuni bila yeye kudai NSSF.

Ya saba, ya sita, katika budget ya Serikali, sisi kama wale jamii watu maskini kutoka area haswa zile za drought, basi Serikali itutengee kiwango fulani cha pesa kuanzia district, kwenda hadi division mpaka location hadi mpaka sub-location ili tupate huduma na sisi tuweze kujiendeleza kama sehemu zingine. Kwa sababu tukitembea Kenya nyingi kila sehemu maendeleo imepatikana lakini sehemu zetu hadi mpaka wa leo miaka arubaini hatuoni yale maendeleo Serikali imetupa. Kwa hivyo kama ni kodi watu wanalipa, lakini yale maendeleo ya Serikali hatuoni. Kwa hivyo mimi maoni yangu ni kwamba, kwanzia district, location, division, mpaka sub-location Katiba hii itengewe Serikali itenge pesa ya kuleta maendeleo katika hizi sehemu ili kuanzia kule sub-location pia na wao waweze kujimudu angalau waweze kujifanisha na Wakenya wengine.

### **Interjection (in audible)**

**Daudi Ali Loka:** Okey nafupisha kidogo. Katika wafanya kazi wa Serikali, ya saba, kuna watu wengi wamefanya kwa hii Serikali, mtu amemaliza miaka hamsini na tano (55) kwa Serikali ameletewa barua kutoka kwa DPM. Baada ameshaenda nyumbani huyu mtu kufutwa zile pesa zake inakuwa ni shida. Anazunguka Nairobi huko na huko, anaambiwa hakuna file, hakuna jina lako, yule mtu anakuja kuaga dunia bila yeye kupata ndururu yake kutoka kwa ile Serikali. Kwa hivyo mimi kwa maoni yangu ni kwamba, iwe mtu anaweza kuruhusiwa ku-retire akiwa amefanya miaka kumi kwa Serikali, akiwa amefanya miaka ishirini kwa Serikali, na kama akipendelea kumaliza ile miaka hamsini na tano (55) amalize, but iwekwe kiwango mtu ukimaliza miaka ishirini kwa Serikali unaweza ku-retire kwa kupenda kwako na upate ile benefit yako. Kuna watu wengi leo wamefanya kwa Serikali, wamemaliza miaka hamsini na tatu lakini benefits zao hawajapata. Kwa hivyo Serikali wakati ile mtu anapo retire, barua amepata kutoka DPM mara moja ile haki yake alipwe na aende akapumzike.

**Prof. Okoth-Ogendo:** Please summarize

**Daudi Ali Loka:** Namaliza ya mwisho. Asante. Ya mwisho iwe mfanyakazi wa Serikali anaruhusiwa ku retire akipenda yeye ama kwa muda wa miaka kumi ikiwa amefanya kwa Serikali, basi akisha retire apate ile benefit yake. Kwa mfano, mtu anafanya kwa Serikali kwa mfano nyinyi Commissioners ama mimi pia ni mfanyakazi wa Serikali. Unaweza kuwa umehudumia Serikali miaka thelathini na umefanya kosa Fulani, pengine umekosana na mtu kwa shamba, umefungwa mwaka mmoja. Baada umeshatoka jela huwezi kupata ile benefit yako. Kwa hivyo ikiwa mtu atafungwa na yeye alikuwa amefanyia Serikali kazi nzuri, basi akitoka kwa jela Serikali imlpe ile benefit yake. Apate ile haki yake, kwa sababu lile kosa alifanya afungwe ni la shamba. Kwa hivyo ile benefit yake ya miaka thelathini amefanyia Serikali basi Serikali imlpe hiyo haki yake kwa sababu hakufanya kosa kwa Serikali. Hii imeumiza watu wengi waliofanya kwa Serikali. Kwa hivyo haki hii ipate kutekelezwa kwa wale ambao wamefanya kwa Serikali kama ni parastatal ama hata ni kampuni. Nafikiri langu la mwisho ni hilo.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana. Hamunyo Ali. Hamunyo Ali, mama ni wewe? Jina kwanza.

**Hamunyo Ali:** Jina naitwa Hamunyo Ali. Asalaam Aleikum, kwanza. *Ann kiswahili dhansa hindageissu maana an takka hinsomne. Annmaoni tann tiyy, (att affan kenn akk dhansa betta). Taa ann silla dhubbad tuttu dhattan dhurra ya dhubbate leissiteammo allen dhikko irbaa yeddin. Taa ann kabbu mpaka tenn taa gaff Kolony taa meli sagali, issi guyya nuu danganyanni nurra fuddan hinfenu, bayyi dhurrasunnumat haa nulakissani.*

**Translator:** Ule mpaka ambao umewekwa na wakoloni wa maili tatu anataka ubaki vile

**Interjection by Hamunyo Ali:** Maili tisa .

**Translator:** Wengine wanasema maili tatu wengine ..

**Hamunyo Ali :** Maili tisa, aaa ni maili tisa.

**Interjection by speaker:** Nafikiri amesema maili tisa.

**Translator:** Maili tisa amesema, ubaki vile vile ambavyo umewekwa na wakoloni.

**Hamunyo Ali:** *A heey. Tunni guddho shidda kabna*

**Translator:** Anasema wao wako na shida kubwa sana.

**Hamunyo Ali:** *Shidda nuu kabnu Kenyan tokkotuyyu yeddani. Laff chuff taan, marr chuff taani amm taa Kolony serkal gargarr kodhu am chuffa walt gath lakkisanni.*

**Translator:** Anasema wakati wa ukoloni, Serikali ya ukoloni ilikuwa ina-control movement ya watu kutoka district hii kwenda district nyingine. Lakini sasa wamechanganywa wote watu wana move vile wanavyotaka tu.

**Hamunyo Ali:** *Maal walti gath lakkisanille gath iyya gudho taabu nuut kennite*

**Translator:** Na wakati hiyo movement ilipoanza imeleta shida kubwa sana kwa wakaaji wa hapa.

**Hamunyo Ali:** *Taabu issin nuut kennite, dhatth nuuijjesille issanum kanna*

**Translator:** Anasema wanaletwa mauaji kwa wingi, wanatuwa ,

**Hamunyo Ali:** *Nuutille obbole y tenna yenne, uffit lakkifne wall dthingamn saan ammo adhui tenna*

**Translator:** sisi tunataka kukaa nao kama ndugu, lakini wao wanageuka wanatuwa.

**Hamunyo Ali:** *Maendeleo uffum challa uffi feddan lakkis nuut namu nuun hinfeddu*

**Translator:** Na wakitaka maendeleo wanataka kujiendeleza wao wenyewe hawataki tushirikiane

**Hamunyo Ali:** *Obbru tussan kuttin namma kenn namma orwaati nudhaggallan taa obrattu*

**Translator:** Anasema wao ni watu wako kando kando ya mto Tana na ni watu wa kulima.



**Hamunyo Ali:** *Duffan obboless obbru nullad yeddani marra amm tambbare owradd yetten abba kuun arm owrrat itdhebbiyye kessambarre sunnit dhebbiyyu.*

**Translator:** Mtu anakuja anakuambia nipatie ka-sehemu hii nilime, akisha kaa basi atakuwa ameimiliki na inaendelea kuwa ni yake.

**Hamunyo Ali:** *Ann taan tiyy garran jirti taa issa garrasin jirti ilman daatte owrru issa kess boon*

**Translator:** Hapo, hapo mahali ulimpa mtoto wangu hawezi pita tena sasa itakuwa ni balaa na mimi ndiye nilimkaribisha.

**Hamunyo Ali:** *Lassimma hindannani*

**Translator:** Atapigwa na atauwa.

**Hamunyo Ali:** *Horri kannke yoon banne horri issa isshen dhandhenne barbadhanno duffnne funna issa dhurri hinjenna*

**Translator:** Ng'ombe wangu akipotea akienda kwa kizuizi yake huyo ameenda sitampata tena.

**Hamunyo Ali:** *Dhubb dhubbi tann nuu gudho uchungu daggaree*

**Translator:** Anasema wamesikia uchungu sana

**Interjection:** *Mooni ttee mann dhubb*

**Hamunyo Ali:** *Shidda tann mooni tiyy haiin namma issuma nurra foffsan fedda.*

**Translator:** Kwa hivyo anasema kwa sababu hiyo anataka wote warudishwe kule ambako wametoka sehemu zingine na kila mtu awe restricted mahali ambako ametoka.

**Hamunyo Ali:** *Namm walba badde inni dhursan itt duff serkali gossissani itt galchunn*

**Translator:** Wote warudishwe kila mtu akae mahali ambako amezaliwa.

**Hamunyo Ali:** *Amm tann Katiba yettani, amm ann yoo ann fikirulle, amm kossollu annuma semeyya ammo ann yoo an fikirulle hujjuntessan middaffano dufftan lakkissi wann issan wananchi karr karrtan hinjirtu.*

**Translator:** Yeye amesema vile mume chukua kalamu mumekaa hapo haoni vile mume kuja kutusaidia, mumekuja tu kukaa, kutusikiza na kuondoka. Lakini kama kweli mumekuja kufanya hiyo kazi, chukueni hayo maoni yangu na muyapeleke.

**Hamunyo Ali:** *Maana yoo arma kaani gallan nutinni tarehe akkasi tarre akkas hujji akkana middassinn, mann akkana middassane yoo eddani lasima musharra lippani*

**Translator:** Anasema kuna wengi wamekuja hapa kutuuliza maoni na kuondoka kwenda ku-claim ma-allowances kubwa



kubwa na kuchukua na hakuna kitu tumeona baada ya hapo. Kwa hivyo anataka kujua kwenu kama mnaweza kusuluhisha tatizo lake.

**Hamunyo Ali:** *Dhubb yoo duggum dhakkan tanna mooni tenn nurra futte dhub, guyya kaan serkallat gessite kaa serkall nuu karkarru*

**Translator:** Kama nyinyi kwenu ni ma-Commissioners ambao mnahusika na Katiba na munataka kusaidia sisi –

**Hamunyo Ali:** *Ishaa serkall dhubbi sunn hatua fuddatte nuu karkarr sunn fenna*

**Translator:** tunataka kuona matokeo ya hiyo shida yetu ambayo tumewaelezea.

**Hamunyo Ali:** *Ta lamessa ilmann somsiffadda yettani, ilman somssiffana, raffanne somsiffne maal guyya kunn ilman kunn somme wakkati silla inn kibarua darggatt nuu ilman kenn kibarua hindarggattu*

**Translator:** Serikali inatuambia tuwaelemishe watoto. Tunapata taabu, tunavunja kuni, tunafanya nini, tunawasomesha akimaliza hakuna kazi anapata.

**Hamunyo Ali:** *Location ilmann it himbaressanu, division ilman itt himbarresanu lasimma distrikk yeddann armma garri timmany yaani yoo acch gett tokk ilman kenn hinfuddan*

**Translator:** Kazi inaandikwa kwa district headquarters, watoto wetu wanatoka kwa ma-locations, wanapiga mguu, wanapiga mguu, wengine wanaomba nauli wanaenda na kurudi hakuna mmoja anaandikwa kazi.

**Hamunyo Ali:** *Shidda duggum yoo mooni nurra futtani mwanainchi karkattan issi tanle injia issan hagg kann serikalit nuu gessittan issan illaltan fenna.*

**Translator:** Kwa hivyo anaomba hiyo pia muichukue muipeleke ili recruitments zikifanywa zifanywe at locational level or divisional level.

**Hamunyo Ali:** *Naam walba adha saa kabba, namm ammo addha tante lakkis koyy taa tiyy seen eddaninullen hinjirtu*

**Translator:** Kila mtu ako na mila yake.

**Hamunyo Ali:** *Nuu islammumma*

**Translator:** Na sisi ni Waislamu

**Hamunyo Ali:** *Garrba kenyya kessa kessaduffiile ta ilman kee ka islama shida guddho irra kabanna*

**Translator:** Watoto wetu wa Kiislamu wanasema wako na shida sana.

**Hamunyo Ali:** *Manna sirkall koittin hinjirti, AP hinjirtu, hattua dhansa tokk namm fuddat hinjirtu, ilman kenn dhaddy dugga bayya ilam kiristo nuu taanat detta kennat galla*

**Translator:** Huu mchanganyiko wa watu ambao yeye alikuwa amesema umeleta shida sana mpaka umebadilisha tabia za watoto. Wengine wameanza kunywa pombe, kuvuta mabangi na kadhalika. Na watoto hao kabla mchanganyiko walikwa watoto wazuri wanakaa kwa njia ya Kiislamu lakini sasa huu mchanganyiko umeleta shida mingi.

**Hamunyo Ali:** *Sunn tuttunnu yoo mooni taan tiyyarishittani nuu karkkartani hatua fuddate sirkalli nuu karkkar sunn fedda.*

**Translator:** Hata hiyo nataka Tume ya Katiba iangalie hayo maneno ili kusuluhisha kwa njia ile inawezeka.

**Hamunyo Ali:** *Mamma hoggadda tan waddatta. KPR taantillen anyimani*

**Translator:** Anataka kuongea kuhusu KPR. KPR, anasema hawa askari ya KPR wamenyimwa sana.

**Hamunyo Ali:** *Hoo guyya kaan tusemme mafanno dhubbada amma halkanni, arm hodhhu armmaill sikabbatein amma hoddhuinna hoo yeddeamm tta, polisiacchi nuut hindufftu, KPR nuu karkkarra.*

**Translator:** Anasema popote shida ikitokea kwa kijiji mtu wa kwanza ambaye tunamwuona ni KPR, polisi hutawaona hapo.

**Hamunyo Ali:** *Dhubb KPR sulle issi kawwe dhansa G3 itt kennani issi agg kan nuu karkarti mooni sirkalla sun fenna*

**Translator:** Anataka wapewe bunduki ambazo zinawafaa kama G3 na kadhalika waondolewe hizi zingine, na wapewe mshahara kwa sababu wanafanya kazi kubwa sana

**Hamunyo Ali:** *Issillen binnadamumma,ilmann kabthi, warr kabthi, issi sirkalli illalletiff garr musharralle wann dhikkolle tatte karkkaran an mooni tiyy akkass fedda.*

**Translator:** Anasema hata wao wako na watoto, wako na famaly na wanafanya kazi ya kulinda wananchi, kwa hivyo anataka Serikali, hata kama ni kitu kidogo, iwaangalilie badala ya kuwaacha tu bure hivyo.

**Hamunyo Ali:** *Amm issa bebbha all hiffade*

**Translator:** Yake ni hayo tu.

**Com: Prof. Okoth- Ogendo:** Asante sana mama ( in audible) Ibrahim Abdalla – okey.

**Ibrahim Abdalla:** Mimi ndiye ninaitwa vile mumesikia. Na imani ya Mungu iwe juu yenu nyote mlio hapa. Sijui kama mnasikia?

**Interjection:** (in audible)

**Ibrahim Abdalla:** Oh jina langu? Jina ninaitwa Ibrahim Abdalla vile mumesikia.

**Interjection** – Endelea basi

**Ibrahim Abdalla** – Ninasema amani ya Mungu iwe juu yenu nyote mlio hapa. Na ninataka kuchangia machache pale ninasikia ndani yangu kwa sababu ninaona kwamba ninataka kuongea juu ya wanawake vile ilivyoandikwa hapa. Wanawake, amaniseme kwa jina nzuri wamama, wanakuwa na hali ngumu sana katika manyumbani mwao huko, wanapata shida nyingi sana. Hao ndio wanaovunja kuni, wanaofanya mambo mengi sana, kazi ngumu sana. Kuwaelimisha watoto na kusaidia hali ya manyumbani yote. Na hawa ukija huko ndani wanapata shida sana na mabwana zao huko manyumbani. Bwana anaweza kuwa anakaa nyumbani na bibi ndiye anaenda kuleta mapato yote nyumbani, sio hapa Tana River peke yake lakini hata North Eastern. Sehemu nyingi sana zina hiyo shida sana. Na hao wanaume wanakaa tu wakitegemea mapato yale yanaletwa na wamama. Na tena wanapigwa mara nyingi wanaumizwa, wanafanyiwa mambo mengi sana ambayo siya kibinadamu ambayo hata hayapendezi machoni pa Mungu, hata Mungu hawezi akafurahiya mambo mengine yanayofanyika kwa wamama. Na tena isitoshe hawapati elimu kama wengine. Kama wasichana tuseme hawapati elimu kama vile kama vile wana wa kiume wanapata elimu. Wengine wanaambiwa wataharibika wakisomeshwa wataharibika na hawatakuwa na maana sana, wanakuwa wanabaki nyuma sana kielimu na kimaendeleo pia hata wanabaki nyuma sana wamama. Ninataka Tume ya kurekebisha Sheria ijaribu kuangalia juu ya hilo jambo nimeongea na hiyo ninasisitiza sana.

Tena ninataka nitoe maoni juu ya walemavu. Walemavu ni pia watu wamebaki nyuma sana, tena ni watu ambao hawajiwezi, ni watu wangepaa kuangaliwa sana. Hata katika community wanakuwa ni watu wanadharauliwa sana, hawapati elimu sana kwa sababu hawawezi wakatembea wakafika kama sehemu ya shule. Wangepaa kusaidiwa kwa mambo mengi sana hata hali ya kusafiri ama kuweza kwenda kwa shule ama kuweza kupata mashule makubwa, makubwa ama hata kuweza kazi. Kwa sababu sioni kama walemavu wengi ndio wale ambao wanapata kaza kwa sababu hawajiwezi, na inakuwa hata hali ya kimaendeleo na hali ya kisiasa wamebaki nyuma sana.

Na tena ninaongea juu ya watoto. Watoto mara nyingi wanapata shida nyingi sana nao, kwa sababu wengine wanawalazimisha watoto hao kuenda vile hao wenye wanataka. Vile wazazi wanataka mtoto awe na inakuwa ni ngumu saa zingine. Mtoto analazimishwa kuchunga mifugo na kuwa katika hali ingine ngumu sana. Na hawa watoto pia ninaona wanapata hali ngumu sana ndiyo ninachangia juu yao.

Na tena ninachangia juu ya mwanadamu, haki ya mwanadamu. Kila mwanadamu anafaa kuwa na haki yake mwenyewe na haki yake mwenyewe ni kuweza kufanya mambo yake mwenyewe. Kama mtoto hawezi kuwa na haki yake mwenyewe, kuanzia mika kumi na nane (18) mtoto anafaa kuwa na haki yake, kama ni mali anafaa kuwa na mali yake kutoka ile boma, anafaa kuwa anaweza kufanya yale mambo yeye anataka. Na haki ya ulinzi, kila mwanadamu anafaa awe anapata ulinzi kamili

ili aweze akafanya mambo yake, aweze akaingilia na hata community ingine, aweze akaingilia na hata makabila zingine, ili aweze akajiendelesha kimaisha. Akaweza kuendelea kisiasa. Aweze kuendelea katika hali yake yote. Hayo ndiyo yale mimi ninachangia, na Mungu awabariki na neema ya Mungu tena iwe juu yenu.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana Bwana Ibrahim.

**Omar Bonaya:** Mimi ninaitwa Omar Bonaya. Jambo la kwanza maoni yangu ni juu ya ardhi na jinsi wenzangu walizungumza kwa mambo ya border. Mababu na mababu zetu ni watu walikuwa wanapigana na Wasomali. Hata kuna watu wetu mpaka saa hii wako Mogadishu wako Hargeisa, waliotekwa nyara. Kwa hivyo border si Tana River peke yake, tuko na boundary Somalia, tuko na boundary ya Ethiopia tuko na boundary ya Sudan, Uganda, Tanzania. Lazima boundary iheshimiwe. Ardhi hii ni urithi wetu sisi wakaaji wa Tana River. Kuna wenzangu wametangulia wamesema Tana River District iko kabila tano, kabila ni sita. Bajuni tuliwacha wapi? Kabila ni sita katika Tana River District. Mimi wakati niliondoka nikiwa mtoto, niliona North Eastern Province hii, ikifika saa kumi na mbili hiyo daraja hauwezi kuvuka, wakati wa mkoloni. Magari yote yanalala upande huu kwa shauri ya security. Mtu kutoka Somalia hawezi kuingia North Eastern Province. Sijui siku hizi imekuwa kutoka tumepata uhuru hata wilaya ya Tana River imekuwa sehemu inawachiliwa free kwa watu wengine wageni. Juzi juzi, imesemekana Machakos hapo iko ndege imetua, Radar yetu haikuona. Hiyo ndege haikutua siku hiyo peke yake pengine imeshatua karibu mara hamsini kuleta silaha. Ulinzi wetu unaonekana umezoroteka, sababu sisi watu wa Tana River District haswa Coast Province, ni watu tunapenda amani, sisi hatutaki fujo. Na hii balaa yote, mzogozogo ya kupigana yote imeletwa na makabila mengine kuingia hapa. Tana River kutoka ukoloni sisi bado hatujapigana, hatujauwana. Kwa hivyo boundary iwe ile ile ya mkoloni sisi tone moja, kipande moja ardhi yetu hatuwezi kuwacha. Ni maili tatu kutoka mji wa Garissa. Hebu angalieni, inasemekana Ijara District, district mpya ya Ijara iko katika wilaya ya Tana River, kuna wakaaji kule wa Pokomo, wakina Komba, inakuwa ni kunyanyaswa, kukata ndizi zao, kuwekwe mifereji na nguvu. Hiyo Katiba hii mpya lazima ilinde haki ya Mwanakenya wa wilaya ya Tana River. Sababu hii itakuja kuleta ugomvi, na sisi hatutaki kumwagika damu.

Ya pili, yangu, ni juu ya wale madiwani tunaowachagua. Ikiwa ni councillor tukichagua yeye, hakuna kitu anatumfaa yeye ni kupora ardhi, kama Kurawa wa Kipini, nani nyinyi mliopewa hayo mabeach hata moja? Lakini mtu kutoka Somalia ana beach Kurawa. Hiyo haki ni yetu, ardhi hii ikiwa ni diwani akichaguliwa, ikiwa ni chairman, asikate na kichwa chake iwe na wazee. Wawe na mamlaka yao katika ardhi yao ya Tana River.

Ya tatu tulisema hapa saa ile ma-Chief kuna – iko wale watu wana elimu, na mimi kutoka mimezaliwa nimeona Chief kila mtu yuko na tabia yake ikiwa ni Munyayaya, ikiwa ni Malakote, ikiwa ni mu Orma, ikiwa ni Pokomo, ikiwa ni Bajuni, watu waliokuwa hawana Chief ni Wata peke yake. Na ukiangalia ni kabila changa haitambuliwi katika wilaya ya Tana River. Na wako na haki, hawakukutwa pahali pengine walikutwa katika wilaya ya Tana River. Haya mambo ya uchuki ya Chief, ni kutoka mtu analetwa kutoka location hii, aende location ya Mbalambala aende aambiwe akae kule kule. Katiba yetu mpya hii ilinde haki ya kila mtu na location yake. Ma Chief wachaguliwe kama zamani, location aliyozaliwa achaguliwe hapo hapo. Ikiwa mu-Orma awe na Chief wake, ikiwa ni Munyayaya, awe na Chief wake, ikiwa ni Wata awe na Chief wake, ikiwa ni

Mpokomo awe na Chief wake, ikiwa ni Malakote awe na Chief wake, ikiwa ni Bajuni awe na Chief yake. Sababu hii kila kitu yote chuki inaleta, leo mu-Orma akikaa hapa kesho Muwata atasema kuwa huyu si kabila langu, Malakote akisema huyu si kabila yangu mashtaka saa yote fitina kwa DC, kwa Member of Parliament. Kwa hivyo Katiba hii ilinde mwananchi wa Tana River sababu ikiwa ni Chief, aajiriwe mtoto aliyezaliwa hapo hapo. Sababu tumeona Serikali ndiyo inagombeza watu. Serikali ndiyo inanyanyasa watu wa Tana River, ikiwa ni Chief hata hiyo katika location wafanye na mlolongo hatutaki mambo ya interview, yule wananchi wanasimama kumchagua.

Ya mwisho hawa ndugu zetu Wasomali wako Garissa hii, ardhi hiyo ni yetu, wanafanya biashara, unafhamu, Local Government Authority ya Tana River, wachukue hiyo rasilmali hao Wasomali wanachukua wako ardhi yetu. Yangu ni hayo tu.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** (inaudible)

**Mugo Ali:** Asante sana, kwa jina naitwa Mugo Ali kutoka Madogo. Ninataka kutoa maoni yangu. Maoni yangu ambayo ninatoa watu wengi wameongea sitapitia lakini nikiunga mkono tunataka ma-hospitali yetu ya Kenya yawe bure. Sababu kwa haya binadamu ni uduma kama wewe huna pesa ya kuhudumia lazima utakufa bure na ugonjwa wako. Kwa hivyo mimi ninawaunga mkono hospitali iwe bure.

Nikiongea kuhusu nchi yetu ya Tana River – uwezo ambao ukoloni ulipatia Local Government ni uwezo ambao umepoteza rasilmali ya Tana River, hali kwamba sisi tumekuwa wakaaji wa Tana River, watu wasiwo na haki yoyote. Kwa hivyo naomba maoni yangu uwezo ambao Local Government ilipewa mbeleni na wazungu, ama wakoloni, huo uwezo urudi katika mikono ya wananchi. Uwezo walio nao leo katika Tana River naomba katika Katiba mpya upunguzwe sana wawe wakifanya na maoni ya wananchi. Sababu walalamishi wengi wanadai kutoka Kora National Park kwamba sehemu zingine ambazo zinatokana na rasilmali ya Tana River resource yoyote lazima hiyo kitu yote iwe ni kitu ambayo imepitishwa na Local Government. Kwa hivyo kama hii nchi zamani ilipewa na wakoloni, Local Government nafikiri wakaaji wa Tana River sasa amepatika tunatakikana uwezo leo wanatumia wao itumike maoni ya kutoka wananchi.

Wengi ambao waliongea hapa, waliongea kuhusu ma-Chief, wachaguliwe na wafanywe na uwezo ya wananchi. Nafikiri katika administration kuna laini ambayo imepanga Serikali yetu kuanzia PC, mpaka DC mpaka DO wanaenda transfer. Nawaomba ma-Chief wapatiwe transfer zao kulingana na vile administration zingine wanaendanga transfer. Na huyo Chief kama ananyanyasa wananchi, na wananchi hawaridhiki na anakaa mpaka retire yake, sioni kama itakuwa manufaa. Kwa hivyo nawaomba ma-Chief pia lazima wapatiwe ma-transfer.

Maoni yangu ya mwisho ambayo ninawachangia, katika nchi yetu ya Kenya wananchi wawe na sauti ya kuongea, ya kusikia maoni ya ki Katiba na mahali walipo wale wamehudhuria ama wale hawajahudhuria wote lazima ni haki yao wazisikie, hata maoni yao yapelekwe katika Katiba mpya. Nikiongea ya mwisho, nikimalizia, kuhusu mambo ya ma-korti. Mtu akiu mtu

kuna mila ambayo watu wetu wanatumia. Kuna wazee wanakaa, wanalipa, mtu akiua mtu damu yake. Wazee wawili saa hii wakiuwana, kwa mfano, wote wako na family, mmoja kwa hatua ya kiSerikali anafungwa hata yeye maishani mwake cells. Yule naye anateseka hapa watoto wake hakuna mtu wa kuwalinda, yule mwingine amepita amekufaa. Kwa hivyo ningomba, mtu akiua mtu, katika ma-korti, inaitwa murder, huyo mwingine anafungwa maisha na Serikali. Huo uwezo urudishwe kwa mikono ya wazee, badala ya watoto wote upande mbili kuteseka. Ni hayo, asante sana.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana Bwana Mugo Ali. Mumina Aron

**Mumina Aron:** Kwa jina ninaitwa Mumina Aron. Nilikuwa na maoni mengi sana lakini kila nikitaka kuongea, ninaona maoni yangu yametajwa na baadhi ya wenzangu. Lakini still, na mimi kwa vile ni maoni nilitaka kutoa, lazima nitatoa. Maoni yangu ya kwanza ni kuhusu wanasiasa, yaani ma-councillors na wabunge. Hao wanasiasa wachaguliwe na wananchi, isiwe wanachaguliwa na Serikali. Sababu ya kusema hivi, kuna baadhi ya wabunge wanachaguliwa na Serikali. Na pia wajue kusoma na kuandika, isiwe ni watu ambao hawajui kusoma na kuandika. Naona shida mingi inasemekana kuwa mbunge amechaguliwa haonekani, shida hiyo inatokana na huyo mbunge kuwa siyo mzaliwa wa hapo mahali. Mbunge akichaguliwa, awe ni mzaliwa wa hapo mahali, akiwa ni councillor awe ni mzaliwa ya hapo mali. Kwa sababu ninasema hivyo, yule mbunge wananchi wanataka, pengine Serikali haimtaki hivyo, munaona wananchi wanachagua mbunge wao, lakini in the long run, munaona mbunge ametokezea ni wa Serikali, amechanguliwa na Serikali. Hauwezi ukajua hiyo mbunge amepitishwa namna gani, wananchi hawamtaki lakini unaambiwa mbunge wenu ni huyu. Yule ambaye amechaguliwa na wananchi hawezi kupata hicho kiti. Na ninaona kama hayo makosa yanatokana na Serikali, Serikali ndiyo inatunyanyasa sisi raia tusiweze kuchagua yule mtu ambaye tunamtaka.

Maoni ya pili, ma-Chief na manaibu wao pia wachaguliwe na wananchi. Na wawe wanajua kusoma. Shida yetu kubwa ni kwamba baadhi ya ma-Chief hawajui kusoma na hawajui kuandika. Sasa hao ndio wana-let down maendeleo. Tuseme kama kwa mfano wakiitwa mahali pa seminar wakuje, mtu kwa vile hajui kusoma na kuandika anaona aibu kwenda kukaa kwa huo mkutano, anaona heri afichike, wale wanaojua kusoma waende wakapate manufaa lakini yule ambaye hajui kusoma atabaki nyumbani amejificha na hapo pahali pake ambapo amesimamia pamelala hivyo. Shida ingine ni hiyo.

Ingingine ni kwamba mambo ya urithi ya vyeo, sisi hatutaki. Mimi ninatoa maoni hayo mambo yasiendeleo, kwa sababu kuna baadhi ya sehemu zetu bado mpaka saa hii kinarithiwa hicho kiti ati fulani alikuwa Chief zamani hicho kiti kinaondoka, huyo mtu amekufaa, kijana wake anachukua urithi. Huyu kijana wake akikufa, utakuja kukuta mjukuu huyo wa huyo aliyekufa amechukua urithi. Hayo mambo mimi natoa maoni mambo kama hayo yasikuwako. Mtu apate kiti kulingana na hata kama ameenda seminar ikiwa amechaguliwa na wananchi, apate hicho kiti lakini kisiwe ni kiti cha kurithi. Na kama nikisema hivyo inamaanisha kwamba Serikali pia, naona kama Serikali pia wanahusika, maanake wananchi pengine yule aliyekufa hawampendi.

Lakini unaenda unaona wanaenda kwa interview, ikirudi interview aliyechaguliwa ni mtoto wa yule aliyekufa ambayo sasa hayo maneno huwa yamepitishwa kule mbele, sio wananchi, yamepitishwa huko ati kwa vile aliyekufa si alikuwa babake, eh wacha sasa huyu kijana wake achukue. Serikali inachangia. Kwa hivyo hiyo pia ninatoa maoni maneno kama hayo yasikuweko.

La mwisho bado ninarudia kwa wanasisia, kuna baadhi ya wanasisia ambao wakiwa wanasimama ama ikiwa ni bunge ma ikiwa ni kiti gani wana kosa. Baada ya kukosa ninawaomba warudi manyumbani, ako na shamba, kama ni yule ako na mifugo aendelee kulisha mifugo yake, ama aendelee kulima shamba lake. Asiwe ni kwa vile alisimama kiti bado still ni mwana siasa anataka kuhangaisha wananchi, hatutaki, mimi nimesema. Na nikisema hivyo, nina lengo Fulani. Arudi ajifanyie kazi yake, na kama kuna kazi fulani baada ya kusimama kiti anapewa na Serikali, Serikali itufahamishe kwamba mwanasisia baada ya kukosa hicho kiti alipewa cheo fulani tujue sisi wananchi. Yangu ni hayo.

**Speaker** (inaudible)

**Jilo Galagha:** Mimi naitwa Jilo Balagha. Maoni yangu ya kwanza, mimi ninazungumza habari ya Tana River, sababu Tana River ndiyo mahali tulikozaliwa na tukakua hapo hapo kutoka jadi na jadi. Tulipata utishi wa kutosha kutoka Tana River. Kabla ukoloni kuingia tulipata shida sana sisi watu wa Tana River, sababu shida tuliyoipata ni hivi: kutoka Msomali tunasumbuana sana, ajabu ndiyo hiyo. Wao wakija wanataka kutuvamia sisi tunatoroka ng'ambo ile tunarudi ng'ambo hii, tunakaa. Bado tunapata tena utishi ng'ambo hii kutoka wapi –Wakamba, Wakamba wanaingia, wanavamia hawa watu wa Tana River. Iile nchi Somali wametuvamia tukaitoroka ndani tukaja ng'ambo hii na leo pia Wakamba wakija tunarudi ng'ambo ile ile na ni vile tuliishi, mpaka bahati yetu ukoloni ukaingia ndiyo tulipata usalama watu wa Tana River, tukaishi kama binadamu ama kama wanadamu. Kwa hivyo Tana River nafikiri hatukuwa wakimbizi kutoka Tana River tukaenda sehemu nyingine tukawa wakimbizi. Sisi tuko hapa hapa na bahati yetu ukoloni ulipoingia tukapata nafasi tukawa na mgawanyiko fulani. Kutoka Mbalambala, mpaka Masabubu unaingia tu, lakini wakati unaingia sehemu ya Malalulu ni ngoma mpaka uingie na masharti Fulani, tena kwa muda kisha urudi mahali pako. Kutoka hivi mpaka Kipini, lakini tangu tulipata uhuru wetu wa Kenya watu tulitawanyika, hakuna mtu anajali, pahali popote anataka anaingia tu. Kwa hivyo kama inawezekana pia hawa watu wa hayawani wakati wa ukoloni tuliishi hivi, hii ni shamba unalima, shamba haitembe, kitu kinachotembea ni hayawani. Hayawani walikuwa mbali na watu wa mashamba. Wanakuja mahali Fulani, wanateremka, wanakuywa maji, wanapanda, wanaenda. Ilikuwa na usalama hivi.

Lakini sasa hii ni shamba na kizuizi cha mbuzi ama ng'ombe iko hapa. Shaka ndiyo hii.

**Com. Bishop Njoroge:** Sasa mzee ungetaka tufanye nini?

**Njilo Balagha:** Naam

**Com: Bishop Njuguna:** Maoni yako, ili tuondoe hiyo shida, Katiba itafanya nini?

**Njilo Balagha:** Shida hii twataka hivi, hawa watu wa hayawani watenganishwe mbali na watu wa mashamba, wawe mbali na



watu wa mashamba. Wawekwe mbali na sisi, wakija, hakuna marufuku na huu mto, kwa sababu kila mtu anautaka mto na hii ni baraka yetu sababu hayo maji inatembeka ikiwa ni ya hayawani, ikiwa ni binadamu, ikiwa ni nani, sote tunatumia hayo maji.

Kuhusu hii mipaka sasa inayotajwa, ajabu tunaizungumza habari ya mipaka. Hii mipaka ni ya nini? Tunashukuru ukoloni ulikwisha gawanya na Serikali yetu wakati ilikamata usukani nao pia wameshika hapo hapo. Kwa nini leo tunazungumza habari ya mipaka, kwani wale waliofanya mbele walifanya makosa? Kwa hivyo habari ya mipaka iishe hapa hapo na maoni yangu ya mwisho ndiyo hiyo.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante sana Mzee. Hayo tumeyapokea, tumeyaandika. Habiba Ndagana, Habiba Ndagana, Abdullahi Dala – Abdullahi tupatie mapendekezo.

**Abdullahi Dara:** Asante sana nimeshukuru wale Commissioners wa Katiba ambao wametembelea tarafa hii. Mimi naitwa Abdullahi Shure Dara, natoka Shara location. Mimi nikitoa maoni katika kikao hiki, kwanza Kenya haitumii haki yoyote yakibinadamu katika Kenya sababu yake, kabila iliyo .... (in audible) katika Kenya wengine amechukizwa na wengine wamefukuzwa na wengine wametupwa nje, Serikali haiwatii maanani. Nikisema hivi kabila ambazo zinazungumzwa hapa katika Tana River kabila sita: Bajuni, Orma, Pokomo, Munyayaya, Malakote, Wata. Wata wametupwa nje. Kuonyeshwa yeye, amepewa majina mengi sana juu yao. Wanasema Bolisanye, hili ni jina la matukano ya kwanza, Haiti Wata si jina lao ni jina la madharau, mara ya pili. Wata hakuna katika Katiba, kama ni Katiba mpya awekwe Wata original katika Kenya. Na Wata katika Tana River hapati Chief yao, amenyanyaswa vibaya sana, hapati maendeleo, elimu hakuna, afya hakuna, tumelia kama mimi ni councillor saa hii ninaomba Serikali haiwezi kusikia maana inasikia wale wakubwa ndiyo wanawaambia hawa Wata sio wa maana. Basi ndiyo ninaomba Katika ibadilishwe kwa njia inayofaa kila mtu apate haki yake. Hakuna kabila kubwa au bora kuliko nyingine.

Ya pili, watoto wetu wa Tana River hawapati kazi ya askari, huko Hola ndiko wanakwenda kuhojiwa. Ningependa kutoa maoni yangu, katika tarafa kama ni polisi, kama ni KA, kama ni idara yoyote wahojiwe katika tarafa yao. Maana yake, leo, kesho inasemekana inatangazwa kwa radio Hola iko na mahojiano, kwa kuandika jeshi. Kijana ambaye ni mzuri lakini hana pesa ya kukimbia huko anakosa. Sasa hii kabila ya Wata hakuna mmoja hakuna Chief, hakuna yeyote katika kazi ya Serikali, ametupwa nje, basi kwa hivyo Serikali iangalie kwa njia mzuri – asante.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante kwa maoni yako. Ali Wario, Ali Wario.

**Ali Wario:** Asante Commissioner. Nikianza ninaomba Katiba mpya ambayo tunaibuni sasa idhihirishe haki zetu, values, aspirations ikiwemo haki na usawa kwa Wakenya wote. Ikiwemo free and compulsory education, elimu ya lazima na ya bure mpaka darasa ya nane. Welfare for less advantaged and marginalized Kenyans such as the people of Tana River District particularly Northern Tana dhulma tuliyofanyiwa ni mingi, Bwana Commissioner. Ningependa kutoa pendekezo kwamba Commission hii, Tume hii na bunge letu isipitishie sheria itakayo overrule Qur'an. Sheria ile tutakuwa nayo iwe chini ya amri ya Qur'an tukiwa Waiislamu, sababu kuna baadhi ya sheria inapita inatulazimu sisi kutoka katika imani ya dini yetu. Tunataka

sheria itakayopitishwa, bunge ama hii Tume isipitishie sheria itakayo-override Qur'an kwa sababu italeti dispute, permanent dispute. Tunaomba Kadhi apewe mamlaka na Katiba ya kuhukumu mambo yote ya Kiislamu, isiwe kufunga mke ndoa na kufunga tu. Mambo yote yale yanayohusu jamii ya Kiislamu, korti ya Kadhi ipewe nguvu kama korti ingine yoyote ile ya kuweza kuendesha jambo hilo.

Bwana Commissioner, ningependa jela tulizo nazo, ikiwa ni rumande ya polisi na jela ya kawaida, maudhui ya kuweka hivi vitu ni kubadilisha mtu atakapofanya kosa. Lakini jela zetu zinaharibu mtu zaidi badala ya kubadilisha. Kwa sababu unaweza pata wanaume ishirini, wanaume mia moja wana-share the same room, hali ambayo imeleta uharibifu wa tabia kati ya jamii zetu za Kiafrika. Neno Lord, the word Lord, should not have equivalent in meaning except God the creator. Neno Lord, ni Maulana, na neno hili linatumwa kwa wanadamu. Unaona hali unaenda kortini unamwita jaji Lord halafu unamsujudia wewe si Muislamu tena ushatoka katika imani ya dini.

That an urgent poverty alleviation programme be formulated and implemented as follows:- Mambo ya upunguzaji umaskini isiwe ni tafadhali ya kuomba donors iwe ni sheria. Lazima Serikali iweke hii sheria ya kupunguza umaskini katika nchi ya Kenya ikiwemo ufufuzi wa miradi ya ukulima ya Bura, na ufufuzi na kusaidia irrigational schemes ambazo ziko chini ya mto Tana – micro credit scheme and entrepreneurship education to advance through a government policy to help establish and promote trade and savings. Ningependa kuomba Commission hii, sisi ni watu tumeumbwa sawa na watu wengine wowote na tunaomba haki sawa na Wakenya wengine wowote hatuombi haki kuzidi Wakenya wengine ila tusipunguziwe haki wakati tunapewa haki kama Wakenya wengine.

That a new democratic Constitution should be established in Kenya and correct and remove the injustices perpetrated against the people of Tana River District by both Kenyatta and Moi Government. Dhulma kubwa tumefanyiwa tukiwa watu wa Tana River. Watu wakiuawa kiholela pasipo na sababu yoyote, leo hii tunaomba Katiba itakayo buniwa, iondowe dhulma iliyowekwa dhidi ya watu wa Tana River. The Pastoral communities in Kenya are the biggest victims of historical, economical and political marginalisation and their pastoral economy has not been fully mainstreamed into the national economy despite its great potential. Needs for a special and legislation and national policy to address and deal with pastoral issues including management, use, sharing of benefits of pastoral resources based on their unique ecological, social, cultural and economical and political context as well as customary nomative systems. We again recommend that the new Constitution should compel the Government to put in place either Ministry of Pastoral Development or Ministry of Livestock and Industry. Bwana Commissioner, zao tuliyo nayo tukiwa wafugaji, tukiwa watu wa Tana River, tunayo mifugo inatutosha sisi, hatustahili kuenda kuomba msaada kutoka mahali popote.

Lakini mifugo hawa Serikali haishuguliki, hungojea ukame ukakuja ukamaliza. Tuko na zao kama maembe, tuko na rasilmali kila aina katika nchi hii, lakini hakuna wizara maalum inayoshugulikia rasilmali ambayo sisi kama watu wa Tana River tunayo.

Special consideration be made for the people of Tana River and of this area such as entry points to universities, special education and literacy development programmes. Tunao watoto, kama watoto wengine werevu, ukosefu wa vifaa yanafanya watoto wetu kuongoza kutoka nyuma kila tunapofanya mitihani. Hii tunaomba Serikali watupatie entry points za hali ya watu wa Tana River na sisi tuweze kupata watoto watakaosoma katika Universities. Ninaomba pastoral education system should be introduced and implemented within the pastoral areas kwa sababu elimu tuliyo nayo it is meant for people with permanent settlement. Ukiwa mfugaji wewe uko hapa, mwaka ujao unahama, lazima mtoto wako analazimika kuhama hivyo basi kupoteza fursa ya kuweza kusoma.

Traditional, religious, judiciary mechanism to be respected. Tuko na dini, tuko na mila ambazo kwamba zinaweza kuhukumu baadhi ya vitu leo vinavyohukumiwa na korti ya Kenya. Na korti hizi hukumu yake ingine ni ya dhulma. Mtu anakufa, mtu huyu alouwawa na mtu mwingine, katika dini yetu, aliyeuwawa jamii yake inalipwa either ng'ombe mia moja, ng'ombe mia mbili au ngamia mia moja. Jamii ile inapata manufaa na jamii ile inalindwa. Lakini katika korti yetu ya leo aliyekufa ashakufaa na yule ako hai anaenda anafungwa so family mbili zote wanahangaika pamoja. Tunaomba sheria itakayobuniwa iheshimu mila na dini ambazo tayari tunayo na zinaweza zikasaidia watu wetu.

An identity card should be used instead of cash bail. Ninaomba korti kwa sababu sheria tuliyo nayo leo mtu akiwa na makosa akiwekwa jela ni lazima atoe cash bail, cash bail ikiwa ni maskini huna cash, inaaminisha wewe utaaumia katika jela. Kwa hivyo tunataka sheria itumie identity card, hauwezi kuchukuwa account pesa, hauwezi kutoka nje ya Kenya mpaka uwe na national identity card. Instead of cash bail tutumie national identity card kama bails.

All land known as Trust land, which is still un-adjudicated and un-registered, is to be referred as held under customary enterprenuer. Umiliki wa ardhi kwa jamii. Ulisikia kuhusu vita vya Tana River District ni kwa sababu arrangement is conflicting. The farming communities want to own land individually while the pastoralists want to own land communally. Kwa hivyo tunaomba tenure arrangement ya communal yaani communal tenure arrangement. Trust lands which is used or occupied by the local indigenious people and from which they derive their daily livelihoods shall be vested in them on the basis of either private or customary tenure depending on the prevailing circumstances.

**Com. Bishop Njoroge:** Mr. Ali can you shorten and give us the points.

**Ali Wario:** Okey Sir, okey Sir. nikienda ku-shoten Bwana Commissioner, moja ni kwamba tunataka kupewa uwezo wa kuchagua mayor, town chairmen na chief officers wa County Council zote. Na kwa vile Bwana Commissioner unasema nifanye haraka, I want the current Constitution to prove a Livestock Industry Development Act that will take will take care of the following areas;

- Creation of Ministry of Livestock and Industry,
- Establishment of appropriate policies for livestock productions and marketing,

- Establishment of appropriate development of activities relevant to livestock industry. Nikiendelea –

**Interjection:** Please summarize.

**Ali Wario:** Okey, I'am summarizing Mr, Commissioner. Nominations of Councillors and Parliamentarians iende kwa minorities. Kuna kabila lina uwezo, linachagua mtu, halafu kabila lile lile tena ndilo linapewa nominated councillor, anapewa nominated MPs. Tunataka sheria hii ipatie fursa wale jamii ambayo hawawezi kuchagua mtu – minorities wewe considered.

Finally, on compensation, incase of a conflict between wild animals and human beings, tunataka compensation kwa wanadamu iwe shilingi milioni moja na damages iwe either a half depending on the degree. Ikiwa ni mifugo walipwe na market rates. Lastly, Mr. Commissioner, ninaomba hii Commission leo hii na hii iwe sheria that administrative boundaries should be recognized and respected. This can only be upheld if our administrative boundaries are going to be defended in the Constitution, both Provincial and District boundaries. Iwe katika Katiba na Katiba ielezee as at nineteen sixty four (1964) kwamba hii ndiyo map ya Tana River na nchi moja ya hii map isiende kwa district ingine yoyote wala isiende kwa province ingine yoyote. This map should remain land of Tana River mpaka kufa kwetu sisi. Thank you very much.

**Commissioner:** (in audible)

**Osman Habatano:** Asalaam aleikum Commissioners na wengine. Kwa vile mnataka summary na muelewe yale mtu anazungumza, yangu itakuwa ni summary. Point yangu ya kwanza ni vote of no confidence kwa wale councillors ama Members of Parliament ambao hawafanyi kazi ile ambayo wanahitajika kabla ya kumaliza ule muda uliowekwa. Kwa hivyo kama councillor hawezi kuhudumia watu ama mjumbe hawezi kuhudumia watu anaweza kutolewa kabla ya kumaliza ile miaka iliyowekw. Jambo lingine, councillor awe at least anajua kusoma na kuandika ili aweze usaidia watu. Point ingine Chiefs, Assistant Chiefs wawe at least wamesome hata kama ni darasa la nane ama Form Four. Point nyingine, mambo ya usalama. Katika sehemu yetu hii ya Tana River tuko na shida nyingi sana haswa North Tana. Kwa upande wa usalama, location mingi hazina askari, hakuna polisi, hakuna AP na wanainch wamevamiwa, waliuawa, mifugo wameenda, kila kitu. Kwa hivyo hapo ninapendekeza ya kwamba iwe askari ya AP na polisi wawe at each location kuangalia mambo ya usalama wakisaidiwa na KPR wakipatiwa bunduki – automatic weapons.

Mapendekezo yangu mengine – Rais asiwe mbunge wa constituency fulani, Rais awe amechaguliwa na wananchi wote kwa jumla, asiwe anasimia constituency yoyote. Jambo lingine ni juhudi ya Serikali kuangalia usalama wa wananchi wake, kulinda mali yao, kwa hivyo mali ya mwananchi ikipotea, ikiharibiwa, mwananchi akiuawa na mnyama wa porini ama mwananchi akiwawa sana sana na bandits ambao tukiangalia ni makosa ya Serikali kutoweka usalama katika eneo hiyo. Kwa hivyo yule mwananchi aliyuawa na mnyama, Serikali I-compensate, na hiyo hiyo compensation, mwananchi pia akiuawa na bandits, ikiwezekana ifanywe malipo ama community ile imesababisha yule mtu kuuwawa alipe damu ya huyo mwananchi.

**Interjection:** Summarize.

**Osman Habatano:** Okey, okey, - let me summarize. Na vile vile mwenyekiti wa county council, ama mwenyekiti wa urban council, mwenyekiti wa town council na hata municipal asichaguliwe tu na councillors kuwa mwenyekiti wao, wananchi katika sehemu hiyo wamuchague kama yeye ndiye mwenyekiti wao kwa sababu hao ndio wamemchagua. Wacha nimalizie hapa kwa sababu umeniambia ni-summarize, niwachie hapa.

**Commissioner:** (in audible)

**John Wanjala:** Kabla ya kutoa maoni, nawashukuru sana wageni mlio safiri safari ndefu. Mimi naitwa John Wanjala, naka hapa hapa Madogo. Kabla ya kutoa maoni nawashukuru sana Commissioners kwa safari ndefu mlio safiri mpaka hapa ili muweze kusaida wananchi. Maoni yangu kidogo, ya kwanza kabisa nitazungumzia kuhusu uchumi wetu wa nchi yetu ya Kenya.

Nchi hii kweli imezoroteka sana hata kama tutalalamika ubadilishaji wa sheria. Kwa sababu kama hapa Tana River utapata kila mwezi watu wanatarajia kuletewa chakula cha relief ambahoo katika uchumi wetu wa Kenya Serikali ingejitolea sana kuweza kufanya mpango wa irrigation. Tulikuwa na mradi wa irrigation hapa Bura ambao ulikuwa ni muhimu sana. Ilisaidia wananchi Kenya nzima. Walikuwa wametoka watu kutoka Western, kutoka Rift Valley, pamba ilikuwa inasafirishwa katika nchi za nje, huo mradi ulikufa. Ukisafiri ukifika Hola, irrigation hiyo yote ilikufa, wale watu wote walikuwa ndani ya mashamba hawana chochote. Haya ukirudi nyuma pia katika uchumi ambao ulikuwa unasaidia Kenya sana, kama kahawa, huo uchumi wote ulikufa. Maziwa, ilikufa, Kenya Meat Commission, ilikufa, majani chai, ilikufa, sasa hii

**Speaker:** Pendekeza sasa.

**John Wanjala:** Mapendekezo yangu ni kwamba, Serikali ingeweza kufufua hizi miradi zote, ili Wanakenya wasipate umaskini. Sababu kama wakati huu mara nyingi tunalia tupate wafadhili ambao miradi yetu mingi iliweza kufa. Kama hapa kwetu Tana River vile nilisema mwanzoni, maji mto unapitisha lakini uwezo wa wananchi kuchota hayo maji watumie kwa mashamba hawana. Sasa kila siku tunaletewa mahindi ya yellow, kwa sababu hatuna kitu.

Haya, mapendekezo ya pili ni kuhusu malipo ambayo watu kama wabunge wanalipwa mishahara kubwa sana hali mwananchi mfanyakazi wa Serikali kama askari, analipwa shilingi elfu nne. Unapata mtu kama mwalimu, hata juzi walikuwa wanalalamika wanataka wagome, kwa sababu gani wanaona ile amount wabunge tuliochagua wakaenda kule juu, wanapata pesa mingi na hao wanapata pesa ndogo na wanasema wakiwa bungeni

**Interjection:** Tafadhali tupatie mapendekezo yako.

**John Wanjala:** Hayo ndiyo mapendekezo yangu ya kuwa kuhusa mishahara ya wabunge ni kubwa kuliko ya... Katiba iweze kuangalia hii mishahara ya wabunge ni kubwa zaidi kuliko ya watu wengine ambao kama wangelipwa hiyo mishahara kama shilingi elfu mia moja, ile ingine iliyobaki ingesaidia wale wengine. Pengine ni kuhusu usafiri kama walivyosema, passport. Watu wengi wanapata shida sana upande wa passport. Ya mwisho watu wamelalamika sana kuhusu mipaka. Kukitokea mabaliko

ya mpaka kama vile tulivyosema itakuwa ni Kenya nzima kwa vile kila mtu atataka kwakwe kuwe na mabaliko. Kwa hivyo ile mipaka iliyowekwa tangu mwanzoni ibaki vile vile. Kwa hayo asanteni.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante Bwana Wanjala. Ali Wachicho.

**Ali Wachicho:** Mimi jina ni Ali Wachicho. Jina langu ni Ali Wachicho. Maoni yangu ni mbili ama tatu hivi. Jambo la kwanza ni mambo ya ardhi. Ardhi hii mara tunasema National Park, mara tunasema mpaka, nini, wewe unazaliwa ndani ya nchi hii yako bila ya kujua ardhi inapewa namna gani, utakuta tu mtu anakuja kuhamia. Kama national ya Mbalambala huku Kalzago, tukiwa huku huku mara ya kwanza hatuna habari nayo, George Adamson aliamisha watu wake na mnyama na kuja kuweka hapo, na sisi wananchi hatuna habari nayo na tuko na haki ya kujulishwa ardhi tunapewa hivi na hivi na hivi. George alipokufa kidogo namna hii watu wa Game wanaingia tena hapo na nchi hii vile mnavyoona kuna wakati mwingine nchi hii huwa hata mvua hakuna na ukame ukiingia mara nyingi tunaenda hapo kwa Kora tunalisha. Tafadhali, mimi mapendekezo yangu naona kama tukipewa uwezo juu ya ardhi hii irudishwe kwa mikono ya wananchi mara moja.

Cha pili haswa sisi Waiislamu hatujulikani. Mara nyingi tunaona ugomvi hapa na pale na hawa wenzetu Wakristo. Juzi juzi ulikuwa hapa, watu walikorofishana na wakaumizana na sijaona Mkristo mmoja akiwekwa ndani isipokuwa Waiislamu peke yake ndiyo walisanywa ndani ya cell. Kwa hivyo Mwiislamu awe na haki kama wale wengine, sio mnalaliwa tu upande mmoja halafu upande mwingine unakanyagwa shingo. Iwe kila mmoja awe na haki iangaliwe mara moja.

Na cha tatu, kitu kimoja kizuri sana, mambo ya hapa na pale iko na masomo nini, hiyo sisi hapa masomo yametupita sisi, kusema kweli. Watoto ambao wanaondoka sasa ndiyo wanapata masomo ya kutosha. Naomba pia Tume hii tupate masomo angalau mpaka Standard Eight Serikali ituangalilie watoto wasome bure. Hayo tu maoni yangu.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** inaudible

**Speaker:** Mimi maoni yangu ni kama hivi.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Anza na jina kwanza.

**Adan Molu Gatana:** Jina yangu ni Adan Molu Gatana ama Golicha pia ni jina langu. Mimi maoni yangu ni kama ifuatavyo. Walemavu wa district hii ya Tana River sijui katika Kenya kwingine lakini district hii ya Tana River, walemavu hawana haki. Walemavu wa Kenya ingine labda wanaweza kusaidiwa kwa njia nyingine maanake radio iko, gazeti iko tunaona tu. Lakini wa district hii ya Tana River hakuna msaada wowote mlemavu anawachwa vile alivyo. Kwa hivyo maoni yangu niliona district hii ya Tana River ni kama district zingine za Kenya, walemavu walioko ndani ni kama wananchi wengine wa Kenya na wao pia wangesaidiwa kama wale Wakenya wengine.

Secondly, hii habari ya mpaka wa Tana River na North Eastern, mimi nilipokuwa mdogo babu yangu alinihadidhia akasema

wakoloni walipoingia hapa nineteen twenty (1920), walikuta kabila zetu peke yake, kabila ya wa Tana River peke yake wakati ule hakukuwa na Msomali hata mmoja. Wakoloni walitawala sehemu hiyo wakina babu zangu wanamwambia walete shilingi moja, sijui sumni sijui ya kodi wakawa wanaitikia wanatoa hivo hivo kufikia nineteen thirty-six (1936) ndiyo Somali wanaingia. Kuingia wakoloni walikuwa wanajua watu hawa ni matata sana, hawakuweza kuwapa nafasi ya kukaa kila mahala waliwapatia tu mahala pa kunywa maji peke yake, ng'ome wao, ngamia wao ni kuingia, kukunywa maji na kutoka kabisa nje wanalisha huko, hawana ruhusa na Garissa wala nini. Ikakaa hivyo hivyo hadi mpaka nineteen sixty-three (1963). Kufikia nineteen sixty-three, wakoloni wanaondoka Kenya wanajitawala. Sasa hawa watu ni werevu na huku wana mali, wakawa wamepata jukumu ya kuomba na nini hapa na pale akapatiwa mpaka ni maili tatu kutoka mto wa Tana. Wakati huo watu wa Tana River.

**Interjection:** Summarize, summarize, pendekeza.

**Adam Molu Gatana:** Maoni yangu sasa ninasema mpaka uwa ule ule waliouweka wakoloni, wakoloni walikuwa si wajinga, walikuwa wanajua mambo ya hawa watu ndiyo wakafanya hivyo wakapeleka wao maili tatu wakapatia watu wa Tana River haki yao. Hata hii ya leo Katiba hii ya Kenya ya kurekebisha wananchi wote kufanywa sawa isinyime haki ya wananchi wa Kenya. Ifanye mpaka ule ule wa maili tatu, ingawa tungetaka maili tisa lakini iwe hiyo hiyo ya maili tatu. Yangu ni hayo.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** Asante sana. Ali Baricha Kangicha.

**Ali Baricha Kangicha:** Asante sana nafikiri sina mengi lakini jina, Ali Baricha Kangicha mtu wa Ngoma. Ngoma ni..... (in audible). Sina mengi ya kusema lakini, kuna maneno, kuna kitendo. Mimi huyu mwembamba mnaniona nimezaliwa nineteen twenty four (1924). Mkoni wa kwanza, wa pili, aaitwa Shabu na Dalak. Ana bibi Borana anajua lugha yetu. Ndiyo mwanzo wa kuona mtu mweupe, tukakimbia, mpaka leo amejitawala lakini kuwa yeye anajiita British Government, Kenya Colony amepatia sisi haki yetu. Mshahara ulikuwa shilingi tatu na sumni, kwa constable lakini ni kama haba nzima. Tumechukua uhuru yetu kama wananchi nikikumbuka Hayati hajakula matunda ya uhuru na Wakoloni, lakini alikataa akachukua. Leo tuliona kitu kingine ngoma ambayo inaimbwa hapa. Wewe husikia lugha, mimi ninasikia lugha, Somali akisema baraguto mimi ninajui maana yake, akisema namboro je, mimi ninajua maana yake. Kitaliani hicho wewe haujuwi unajua Kiingereza. Kuna shida hapa, oh, ni hivi. Somali sisi hatukukataa jirani wageni wamehama kutoka Djibouti, Baidoa, Mogadishu, British Somaliland yote iko hapa, tumesema welcome, tunakaribisha. Wanakuja na bunduki wanatupiga, ng'ombe wanachukuwa, mbuzi wanachukua, mwisho wanaleta kazi ya ushenzi wanachukua wasichana wanaingia nao msituni na tunavumulia. Akageuza sasa kusema nyimbo za kututusi, nyinyi hamjui mimi ninajua ..... (in vernacular) maana yake nini, ardhi ni yao lakini mafuta ni yetu. Tunavumulia. Kidogo namna hii anasema.

**Interjection:** (inaudible)

**Ali Baricha Kangicha:** Maoni yangu ambayo sasa mimi ninatoa ile boundary isipitishwe kabisa, ikae hivyo hivyo. Siku ya kuchaguliwa hivyo sio sisi. Mmoja anatoka Australia, mmoja anatoka Nigeria ndiyo Commissioner of boundary na



wamechagua. Kama nikupitisha, au kutaka kubadilishwa Jamhuri nzima yote itateseka . Lakini hiyo tumekataa lazima hii .... mipaka iweko.

Ya mwisho, watoto wetu hawapati kazi kwa sababu – ‘asiyejuwa maana aelekee jiwe’. Kuna ngoma hapa, ngoma la pwani Bajuni amesema ‘nimenena lakini sikusema’. Watoto wenye afya zao wakienda kazini, bado tosha kazi, tunajua sisi cha mvunguni, lakini wakati wa kuajiriwa watoto kwa kazi, tunataka wazee wetu wako pale waone hawa chawa wanakula watoto kila saa wanakosa kazi. Vita ya Italiano, na Ujerumani na Burma wote wale watu wasiojua. Kizungu ndiyo wanapika. Watoto wetu hawatoki nyota, kwa Serikali hakuna mmoja na daraja ukifika huko hata OCS hakuna, askari afande tu, Shifta ametokea hapa, we shifta iko hapa, ngoma inakwenda kutafutwa, hapa iko nini, muhoga hana Mungu.

**Interjection:** Asante sana mzee.

**Ali Baricha Kangicha:** Lakini tumevumulia. Hivo hivo tunawaomba Serikali itusaidie. Mimi mwalimu wangu alikuwa Ochieng Oneko, Mbiu Koinange, Jomo Kenyatta, Bildad Kaggia, Kungu Karumba, Paul Ngei, Lokitang na Manda Island. Sina masomo lakini nina akili ya kutosha kujua tu ule msemo wa miwani ‘iko na ngoma na usikatae. Asante. Thank you very much. Jina langu Ali Baricha Kangicha.

**Com.** (Inaudible)

**Daudi Mwangangi:** Asante, asante. Asante Bwana Commissioner. Maoni yangu kwa hali ya kutengeneza Katiba yetu, si yangu pekee ni pamoja na ile .. ( in audible) ambayo ni service provider wa haya masomo. Katika utangulizi wetu katika Katiba tungeomba a map of our country and law be in the Constitution, map ya Kenya na law pia katika hii mapu tuwekewe mikoa na wilaya, ikionyesha makabila kila sehemu vile yalivyo, ikiwa ni Tana River, makabila gani yako pale, mpaka uko vipi imekwe kulingana na hali katika map vile ilivyo. Na hayo ndiyo yalikuwa maoni yangu kwa upande wa utangulizi.

Katika sehemu ya pili, tulikuwa tumeonlea katika hali ya ufisadi ili tuumalize katika Katiba tulikuwa tumeonelea kama ingewezekana kiwe na ile rasilmali ya mtu kiwango kiwe at least kinajulikana. Sababu sasa katika ile hali ilivyo sasa mimi ninaenda ninanyakua vitu vyangu wenzangu wako hapa, majirani wanalia, watoto wanakufa na chochote lakini sina hali ya kusaidia, sina roho, na ndiyo hata sasa professionally hata ikiwa umesoma kwa sasa , ule usaidizi unaoneka hauko katika jirani yako. Kwa hivyo ninaonelea kwa maoni yetu, tulikuwa tunaonelea kama ingeweza hii rasilmali iwe mimi vile ninavyo pata mwenzangu anaweza pia kuwa katika ile kiwango hatutakuwa na faragano. Tutakuwa katika hali moja asanteni.

**Com. Prof. Okoth-Ogendo:** (inaudible)

**Ali Loka:** Jina langu. Ali Loka.

**Translator:** Jina lake ni Ali Loka

**Ali Loka:** Wann ann dhubbaddu yadufftani dhubbi tanna nuu jarrolle dhurrati, kaa gaan gugurdhatti. *Dhubbi tanalle akk issin barassatiff kunille annin amm tan gargarran bennyu.*

**Translator:** Amesema yeye ni mzee wa zamani na saa hii hajui hii ni mkutano au ni nini inaendelea.

**Com. Zein.** Muelezee kwamba hii ni mkutano ya kuchua maoni ya wananchi.....

**Ali Loka:** *Nuu guulum idhem ree, nuu gullum idhem, maya dhubbi dhubbade, issi aa mukutanotiff barrasalle gargarra himbenu, ammalle amm tann isshiyya moyooni wananchi akk yeddaniille kaan walbe.*

**Translator:** Sasa ametambua ya kwamba huu ni Tume ya kuchukuwa maoni ya wananchi.

**Ali Loka:** *Waan dhubbadelle laff taan gudho itt shiddha kabn*

**Translator:** Amesema hapa wako na shida sana.

**Ali Loka:** *Kenya yeddani Kenyan suun keyya, ammo wann boffa, shimpirre binnes nyattu, waan kasshin, butti, boffa dhimma, wann kaan kess jirra yedd.*

**Translator:** Tunaambiwa ni Kenya lakini iko na takataka nyingi sana, nyoka kubwa kubwa mandenge balaa nyingi yote iko ndani.

**Ali Loka:** *Kenyan kabilla tokkochanit yedd*

**Translator:** Kenya sio kabila moja inaishi ndani.

**Ali Loka:** *Lakkin sehemu sehemu gargari kabthi yedd*

**Translator:** Lakini iko sehemu tofauti tofauti.

**Ali Loka:** *Tana River yeddani, mpaka kissinya athi, mpaka kora*

**Translator:** Tana River inaanzia Kipini mpaka Kora.

**Ali Loka:** *Kabila shannit kess jir yedd*

**Translator:** Iko kabila tano

**Ali Loka:** *kabila dibbit nuu duff yeddin*

**Translator:** Tuliingiliwa na kabila zingine kutoka ngambo hiyo

**Ali Loka:** *Kenyallo amm tan Katiba yedde, gaff sirkal engeressalle Katiban sunn hinjirti yedd.*

**Translator:** Hata wakati wa Uingereza Katiba ilikuweko.

**Ali Loka:** *Sirkall engeressa wan inni guyya sunn namm gaffattu, wann chiffaffa, wann iyo wann councilor NFD wann kaan namma gaffata, hayyu kabbada yeddeni dhubb hayyu kabban yeddin.*

**Translator:** Wakati huo wakoloni walikuwa wanakuja kushauriana na wananchi wanauliza chaguweni councillor wenu chaguweni chief wenu na wananchi wanachagua.

**Ali Loka:** *Laff wananchi haffat dhubba ilman illalani, dhubba kunnin chief kenn yeddani chagguan yedd.*

**Translator:** Hawa ambao wananchi wanachagua ndiyo wanakuwa viongozi.

**Ali Loka:** *Yoo headmenille wananchi chaggua yedd.*

**Translator:** Hata ma-headmen wanachaguliwa na wananchi.

**Ali Loka:** *Amm wann sunn hinjirr yedd*

**Translator:** Saa hii hakuna mambo kama hayo.

**Ali Loka:** *Masomo yeddani dhadh dibbin somte, ammale skool issa dhadh dibbin ilamn dikko digri kabbu, dhubb gullan taan application barreffada yeddin dhubb wann jiir yedd.*

**Translator:** Siku hizi yamekuja mambo ya elimu na hao waliosoma soma wamekuwa wakora na ndiyo wanaajiriwa katika kazi ya ma-chief na councillors.

**Ali Loka:** *Skool issi kuun dhubb amm wan tanna, dhubb chief argatte kaa gullan tann nami sumbuul kaan yedd*

**Translator:** Huyo huyo ambaye tunamwita chief ndiye amekuwa mkora, ndiye anaanza kuibia wananchi.

**Ali Loka** *Dhubb amm taan mayyoni yaa*

**Translator:** Kama sasa ni maoni.

**Ali Loka:** *Waan sirkal ammtan feddu himbenn yeddin.*

**Translator:** Hatujui Sirkali inataka nini.

**Ali Loka:** *Katiba tann garr sirkal gargassan feddu nuut himbenu yeddin*

**Translator:** Hatujui Serikali inaekeleza wapi hii Katiba.

**Ali Loka:** *Hakki wananchitunn dhubba wann issin dubbat yoo wan sirkallini Kenya wananchi itt mammas walkutante wall kuttun tanna inni digri taan barbadhulle himbenn yeddin.*

**Translator:** Pengine Serikali nao wako na mipango yao na wanakuja kuuliza wananchi pia maoni na wao kumbe wako na mwelekeo wao hatujui.

**Ali Loka:** *Guyya kaan saa issan nnut dufftan mpaka saa kanna lall jeddin sodalle hindhunne*

**Translator:** Kutoka asubuhi wamekaa hapa hata soda hawajakunywa

**Ali Loka:** *Dhubbi nurra fudda dufftan yedd*

**Translator:** Mmekuja kuchukua maoni, hata nyinyi wenyewe hamjakunywa soda.

**Ali Loka:** *Shidda yedd wann kaan*

**Translator:** Shida kubwa sana hii.

**Ali Loka:** *Hinhiffatina yeddin*

**Translator:** Na msichoke.

**Ali Loka:** *Booku kann namm wadhubbat tuttukodhaniff yeddin.*

**Translator:** Mumegawa hivi vitabu vyote kwa mtu ambaye amekuja hapa.

**Ali Loka:** *Akka guyya kannaanzittani, burrolle issi arm jirttaniff issi kann jirtan himbenn yeddin*

**Translator:** Sijui kama ni leo tu muko hapa ama ni kesho na kesho kutwa.

**Ali Loka:** *Mooyoni nuu feen,*

**Translator:** Vile tunataka

**Ali Loka:** *Waan shidda kaan kaa Kenya shidd*

**Translator:** Shida kubwa ambayo iko Kenya saa hii

**Ali Loka:** *Kanna issan dhurrani paka kipinya, mpaka kora uffumma akkum gallan yauu kaan akkan kakabonofft fedd.*

**Translator:** Tana River kutoka Kora mpaka Kipini ilikuwa na amani na watu walikuwa wanakaa shwari kabisa.

**Ali Loka:** *Amm taa amma owditt yeddin*

**Translator:** Lakini sasa imekuwa moto kabisa

**Ali Loka:** *Waa owddisellen,*

**Translator:** Na kitu ambacho kimeifanya moto

**Ali Loka:** *Kenya mizima,*

**Translator:** Kenya mzima

**Ali Loka:** *Daggara gath duffte yeddin*

**Translator:** Hawa ambao wametoka ngambo ile ndio wameleta.

**Ali Loka:** *Sommali garran duffte*

**Translator:** Hawa waliyoyataka Somalia ndiyo wameleta shida yote na wakafanya kila kitu kuwa moto.

**Ali Loka:** *Sirkal Kenyalle ya dhikko ballai yeddin.*

**Translator:** Na Serikali ya Kenya imepotea kidogo

**Ali Loka:** *Sirkall guddho akilli kabba,*

**Translator:** Serikali iko na akili

**Ali Loka:** *Dhubbi taan akkam ilale komishu daddab yeddin.*

**Translator:** Kwanini wanashindwa kutatua shida hii?

**Ali Loka:** *Kawee amm taa nadden chuffti yattun*

**Translator:** Bunduki hata wanawake wako nayo

**Ali Loka:** *Kaa gamm sunn dhadhamassi duffte*

**Translator:** Na wametoka nazo huko

**Ali Loka:** *Nuu kaa tana River hinkabbnu*

**Translator:** Na sisi hatuna

**Ali Loka:** *Kawwe Kenya misima immede amm nami wallin ijees*

**Translator:** Na wananchi wanatumia kumalizana nayo

**Ali Loka:** *Garran dufft yeddin*

**Interjection** *Maooni tante maan*

**Translator:** Anasema maoni yake

**Ali Loka:** *Ann mooni tiyy wann ann feddu, wann kawwe kan tuttu*

**Translator:** Haya mambo ya bunduki

**Ali Loka:** *Sirkal haa nurra kkommeshuu yeddin*

**Translator:** Serikali watumie akili yao. Wako na ujuzi, wapoteze kabisa na kuangamiza.

**Ali Loka:** *Taa lamessa*

**Translator:** Ya pili

**Ali Loka:** *Tanna River kaan golla bayya ya nurra fuddatan yeddin.*

**Translator:** Hiyo sehemu yetu ya maili tatu tumeshanyang'anywa tayari.

**Ali Loka:** *Issa sirkal nuu fikire*

**Translator:** Tunataka Serikali

**Ali Loka:** *Nuttin kabila Tana River, sillaha akk dhagga achi nuduffe hinkabnu*

**Translator:** Sisi kama watu wa Tana River, hatuna silaha

**Ali Loka:** *Sirkall nuu fikire,*

**Translator:** Serkali itifikie,

**Ali Loka:** *Namm walba*

**Translator:** Kila mtu

**Ali Loka:** *Uhuru kenne*

**Translator:** Apewe uhuru

**Ali Loka:** *Garrasif garrkalle*

**Translator:** Hapa na huko kila mtu akae kwake

**Ali Loka:** *dhubb sunn uhuru irra kabn*

**Translator:** Na sisi tuwe na uhuru

**Ali Loka:** *Akkan fenna yeddin*

**Translator:** Tunataka hivyo.

**Ali Loka:** *Yoo issan wa haqqi amm illach idduftann*

**Translator:** Kama mumekuja kuangalia haki

**Ali Loka:** *Wann haqqi sunn*

**Translator:** Hiyo haki

**Ali Loka:** *Dubbi namma guddhat wadhubatta*

**Translator:** Wengi wanaongea

**Ali Loka:** *Dhubbi sunn chagua*

**Translator:** Mchague

**Ali Loka:** *Dhubbi sunn nuu gessa yeddin*

**Translator:** Muipeleke.

**Ali Loka:** *Sirkall hinbekka*

**Translator:** Serikali inajua.

**Ali Loka:** *Ann tiyykittum kannu, hayya*

**Translator:** Yake ni hayo tu.

**Com. Zein:** Ndugu, ndugu mimi nitakurusu uzungumze, lakini kama unavyoona Mzee, mwangalie hebu Mzee huyu? Unaona Mzee alivyokuangalia hivyo – ni kwa sababu ulikwenda mbele yake na tulisema baada ya yule Mzee mwingine tutakuja kwake mzee, wewe endelea tu lakini ujue umefanya hivyo Baada yako mzee utakuja wewe. Taja jina halafu twende haraka haraka.

**Mohamed Sanei:** Mimi jina langu naitwa Mohamed Sanei kutoka Maram sub-location. Shida kidogo mimi nataka kutatua leo hapa, ninataka kuzungumza machache kidogo. Sisi kama Wakenya, hatuwezi kusema watuelemishe mashule zote bure, tukisema shule zote bure Serikali yenyewe itapata pale hasara. Hatutaki Serikali yetu ipate hasara. Kama sisi sasa hapa Madogo, ni division, hapa wasomeshwe bure, mahali pengine waendeleo kawaida. Maramtu sub-location hivo hivo, mpaka Tana River yote, all.

Na ninataka kuzungumza shida tuko nayo sisi hapa Wanakenya, all, mzima. Si Tana River peke yake ama, mahali kama Madogo ama Maramtu ama Bangale, hapana. Ya kwanza tunataka sisi kama wafugaji, wafugaji iwaangalie Serikali iwaangalie.

Wafugaji Serikali haiwaangalii. Tukisema kweli, Serikali inajua mtu anajenga ploti, na ana shamba na ana elimu na pia wafugaji iko kazi ya hawa watu, waangaliwe. Wafugaji na kila akae district yake. Mmoja asivuke kwa district ya mwingine. Wafugaji wametoka district nyingine kila siku wanakuja kututawala hapa kila siku. Tumeona wafugaji wametoka mahali



pengine wanakuja kulisha hapa.

**Com. Zein:** Mohammed?

**Mohamed:** Hapa

**Com. Zein:** Mohammed? Umesema umependekeza maslahi ya wafugaji yaangaliwe, umependekeza kila mtu akae kwa district yake, umependekeza watu wasiingiliane kwa sehemu za malisho. Sawa, endelea.

**Mohammed:** Ya pili Chief tunataka wachaguliwe, chief tunataka wachaguliwe, chief tunataka wachaguliwe. Vile Bwana Garacha amesema.

**Mohammed:** Ya tatu, ya tatu, ya tatu, sisi tunataka hospitali zipelekwe kila sub-location, ama location, na hospitali ziwe bure. Kunao wengi hawajisaidii, hawana nguvu yoyote.

**Interjection:** inaudible

**Mohammed:** Wapelekwe bure

**Interjection:** Sawa

**Mohamed:** Ya nne, tunataka, ya nne, kila sub location ama location, division kama Magodo hivi sasa, Kenya all, mzima iwe na soko ya maana. Soko. Ng'ombe au mifugo yoyote asifuge kwa mahali pengine, asipelekwe huko. Ndiyo.

**Com. Zein:** Mohammed, uko karibu kumaliza, fupisha kabisa.

**Mohammed:** Ndiyo, yes. Ya tano ninataka, ardhi, ni yetu wananchi, ni ya Serikali, hatutaki ardhi kugawanywa bila kabila ya ardhi hiyo kukaa. Kama sasa tunajua mahali panaitwa Galana, ni petu na hatujui mahali pamepewa watu na hiyo Galana tuko madai.

**Com. Zein:** Mohammed , Mohammed,

**Mohammed:** Ndiyo,

**Com. Zein:** Mohamed, we ngoja Mohammed ngoja. Umependekeza ardhi ya wenyeji wa watu wa kabila linalo husika washauriwe kabla ardhi hiyo haijafanywa kitu chochote. Sawa endelea.

**Mohammed:** Waturudishie haki yetu, na ardhi isigawanywe bila kukaa wananchi. Bila kukaa wananchi. Na mtu ametoka sehemu nyingine anapatiwa hapa ardhi, hiyo hatutaki. Ya kipande, tunataka kipande, watu wanaotoka mahali pengine

wasikatiwe hapa kipande, na katiba ya leo mpya hiyo irekodiwe kabisa, irekodiwe, asimpatie mtu ametoka Mogadishu wachukue kipande hapa hatutaki. Ya sita, election,

**Interjection:** Ya mwisho, ya mwisho hiyo Mohammed

**Mohammed:** Ndiyo, election, tunataka tafadhalini hiyo Katiba ya leo mpya mtu akatiwe kipande yake hapa, election yake apelike mahali pengine. Kura apeleke mahali ingine, na kipande achukue hapa hatutaki hiyo. Tana River, sisi tunajuwa kabila sita, bwana Commissioner, sikia sauti yangu vizuri sana, usikie vizuri. Tunajua kabila sita, kabila sita hiyo moja ni mu Orma, ya pili ni Mpokomo, ya tatu ni Wardhei wale wanaitwa Wardhei, ya inne ni Munyayaya, ya tano,

**Com. Zein:** Mohammed, Mohammed, Mohammed,

**Mohammed:** Ya tano, ya tano ni Malakote, nimetoka

**Com. Zein:** Mohammed, Mohammed, hiyo ndiyo

**Mohammed:** Ya sita, ni Wata, hakuna Bajuni hapa Katiba ijue namna hiyo.

**Com. Zein:** Mohammed, Mohammed, usifanye hasira kwa mambo haya. Nenda pale ukaandikishe. Usifanye hasira Mohammed.

**Speaker:** Wandugu zangu, huyu ndugu yetu anasema hakuna Bajuni, sijui Kipini nani anaishi.

**Com. Zein:** Ah, ngoja, ngoja, ngoja, ngoja, ngoja kwanza tuelewane. Tumeendelea vizuri siku nzima tusije tukaiharibu mwisho. Mohammed anasema yeye maoni yake hakubali Bajuni kuwa ni watu wa Tana River, nyinyi munasema hapana ni watu wa Tana River. Lakini, ana maoni yake na ana haki ya kutoa maoni yake au si sawa hiyo? Mzee endelea.

**Boya Son of Tukale:** Mimi ninaitwa Boya son of Tukale,

**Com. Zein:** Tumia microphone ndiyo tusikie jina vizuri.

**Boya Son of Tukale:** *Waan att yettuni*

**Translator:** Anasema,

**Boya Son of Tukale:** *Inna maa jaah kka Tana River jirr*

**Translator:** Hawa watu sita

**Boya Son of Tukale:** *Inna namma jaah kka Tana River jirru, kweli dhadhi suun uhuru hagargatte?*

**Translator:** Hawa watu sita ambao wako Tana River, kweli wamepata uhuru? Anauliza.

**Boya Son of Tukale:** Orma, Munyayaya, Malakote, Pokomo, na Wata watu tano, wamepata uhuru kweli?

**Translator:** Kweli wamepata uhuru? Anauliza.

**Boya Son of Tukale:** Mimi nina swali nyingi. Ya pili kitu moja sisi tunzshangaa *wann nuu shaggon dhubbi tokk shangoon*

**Translator:** Kitu ambacho wao wameshangaa

**Boya sonof Tukale:** *Chiefgf yoo amm tann chaguan, serkali chagua yeddin*

**Translator:** Serikali ndiyo wanachagua chief

**Boya son of Tukale:** *Mall shaguulle akk nam dhansatiff kaa naam hamma gargarri hinbeku yeddin.*

**Translator:** Na hawajui kama huyo wanayemachagua ni mtu mzuri au ni mtu mbaya.

**Boya son of Tukale:** *Labdha gaal dhegg chaguan nammatin duffan yeddin*

**Translator:** Pengine wanachagua mayonda wanaleta sisi kwetu kama chief.

**Boya son of Tukale:** *Mmoni tiyy taa kwansa issi Chief amm wananchin chaggat fedda yeddin*

**Translator:** Anataka chief achaguliwe na wananchi wenyewe

**Boya son of Tukale:** *Taa lamessa yeddin*

**Translator:** Ya pili

**Boya son of Tukale:** *Waan ann feddu,*

**Translator:** Vile anavyotaka yeye

**Boya son of Tukale:** *Sammani wakati kolonia*

**Translator:** Wakati wa ukoloni,

**Boya son of Tukale:** *D.C. maal chungu maal issin amm tann barasa duffi*

**Translator:** DC wakati wa ukoloni akija kwa baraza,

**Boya son of Takale:** *Wasse amm makka gudhiyyu amm naam tokk akk wakae amm wadhubattu jaal nakkae wadhubbat*

**Translator:** Wanatanguliza wazee wale ambao wana umri mkubwa iliwatangulie kuongea.

**Boya Son of Tukale:** *Sirkall amm tanna dadh tanni ta siyasatin wa dhubbadda yedda dhadd siyasallen kashia llati yeddin*

**Translator:** Serikali ya siku hizi wanachukua wanasiasa ndiyo wanatanguliza

**Boya Son of Tukale:** *wann amm jirr hinkortu yeddin, kashia lalte gullan taan makossa jette kessa batti*

**Translator:** Hawaelezi yale ambayo yanatakikana

**Boya son of Tukale** *Issi sunn shaa sirkal nuu lall fedda yeddin*

**Translator:** Hiyo tunataka Serikali ikomeshe

**Boya son of Tukale:** *Yoo barasa duffan, wassee lam sadhi amm taan, wasee wan laff tan kess jirr dhubbada yeddan, dhubb wasee laff kess jirra..*

**Translator:** Wazee wapewe nafasi ili waeleze yale yote ambayo yako katika

**Boya son of Tukale** *Taa sadhessa yeddin,*

**Translator:** Ya tatu

**Boya son of Tukale:** *Taa misho yeddin*

**Translator:** Hiyo ni ya mwisho

**Boya son of Tukale:** *Mooni ann bassu ishian amm ttan wann tunnu harkam tanni wananch ashh eggana yeddini*

**Translator:** Tunataka kila mamlaka iwekwe mikononi mwa wananchi.

**Boya son of Tukale:** *Bunge yoo shagguanit Nairobi galla yeddin yakuffe*

**Translator:** Mbunge akichaguliwa yeye huenda akakaa huko.

**Boya son of Tukale** *Councillor lalle akkas yeddin*

**Translator:** Councillor naye hivyo hivyo

**Boya son of Tukale:** *Waa amm taan sirkal amm tan yoo inni ahadi nurra fudde, naam amtani nuu lakkise amm taan garr dibbit gaall isha nullen garr ishaa sirkal nurra fudde ...*

**Translator:** Tunataka yule ambaye anatumtupa na sisi tumtupe.

**Boya son of Tukale :** Asalaam aleikum

**Speaker: (inaudible)**

**Iman Fomau Rido:** Na jina langu ni Iman Fomau Rido, jina yangu ni Iman Fomau Rido kutoka Mbalambala location, natoa maoni kwa niaba wa watu ya location mbili, ya Mbalambala na Pua. Maoni ya kwanza watu ya Mbalambala na Pua location walisema kwamba wanataka katika Katiba hii ipitishwe watu wa Tana River as a whole wapewe title deed. Maoni ya pili, education. Watu wa Tana River, haswa North Tana Division ni watu ambayo elimu yao iko chini kwa hivyo wanaomba wakati watakapofanya recruitment ya any forces hawa watu wasiangaliwe hali ya education yao, waandikwe vijana kazi ili wakuwa sawa na Wakenya wengine.

Maoni ya tatu, wanasema ya kwamba katika Tana River, hawa watu ambayo wanakuja kuandika watu waandike askari katika location sio kwa district. Maoni ya nne, councillors na ma-chief, wameomba ya kwamba hawa watu wachaguliwe ikiwa ni mtu ambaye amesoma na kuandika, siyo tu mtu ambaye hajasoma. Maoni ya tano kuhusu administration boundaries. Haya mambo ya boundaries tunataka hiyo boundary iwe ile ile ya zamani ambayo imewekwa na colonial. Maoni ya sita, wamesema ya kwamba, councillors wawe wakiteuliwa, wapewe mshahara na Serikali sio wapewe mshahara kutoka kwa mapato kutoka mapato yao.

Maoni ya saba, wanasema ya kwamba ulinzi ambayo unatakiwa katika North Tana Division, haswa sehemu ambayo hakuna security, ambaye hakuna polisi na hakuna AP, wanatakiwa KPR ambaye wako area hiyo wapewe automatic weapons yaani bunduki ya aina ya kisasa ili waweze kulinda mali ya wananchi. Maoni ya nane, wanasema National Parks ambazo ziko karibu na areas za wananchi wanaomba wasaidie wananchi ambao wako karibu nao kimaendeleo kusaidia mambo ya hospitali na mambo ya skuli, wajaribu kuwasaidia wananchi. Maoni ya tisa, kuhusu secret ballot, mambo ya kura. Ikiwa wananchi wamechaguwa yule mtu wanaomtaka Serikali wasimbadilishe huyo mtu kulingana na mabavu yao, ili mtu huyo hiyo awe ni mtu ambaye amechaguliwa na wananchi. Maoni ya kumi, wanasema ya kwamba, President akichaguliwa, asiwe MP wa mahali fulani, awe ni President wa watu yote ilie ajaribu kusaidia kila mahali katika Kenya.

**Com. Zein.** Haya malizia sasa Mzee wangu.

**Iman Fomau:** Hiyo ndiyo yangu ya mwisho.

**Com. Zein:** Tafadhali toa huo mswada tutausoma na uandike jina lako kwenye register mzee. Huyu anaofatia hapa. Ndugu, taja jina na uendele.

**Ibrahim Bonaya Ware:** Asante bwana Commissioner, kwa jina naitwa Ibrahim Bonaya Ware kutoka Sala location, hapa natoa maoni kwa niaba ya wakaazi Sala location. Maoni ya kwanza, walisema mkenya asiwe na uraia wa nchi mbili. Na ya pili, anasema, kila location kuwe na kituo cha polisi. Ya tatu wanasema napendekeza vyama vya kisiasa zisiwe zaidi ya mbili.

Ya inne wanapendekeza kueendeleo kuwa na muundo wa Serikali ya urais. Na ya tano, wanasema mgombea kiti cha bunge au rais awe na umri wa miaka ishirini. Na ya sita, wanasema, rais asiwe mbunge, na akikosea katika kazi yake, apate kushtakiwa mahakamani. Na ya sita, wanasema, ma Kadhi, na Kadhi Mkuu wawe na masomo ya juu kama mahakimu wengine na wapewe uwezo wa kufunga mtu. Isiwe ni kufunga ndoa na kufungua. Ya saba, wanasema mayor, na wenye viti wa mabaraza wachaguliwe na wananchi. Ya saba, wanasema masomo kutoka darasa la kwanza hadi la nane kuwe bure. Na ya nane, wanasema haki za ardhi, wanaongea juu ya haki ardhi, wanasema ardhi kusipewe kwa mtu binafsi hasa mtu kutoka nje ya wakaazi wa area hiyo. Ya tisa wanasema, mahitaji ya wananchi yote, kunapaswa kuhakikishiwa na Tume ya kuangalia haki za binadamu.

**Com. Zein:** Ibrahim malizia sasa.

**Ibrahim Ware:** Bwana Commissioner, sorry, nikimalizia kila dini vile wenzangu walisema kila mtu ako na dini yake na sheria isiwe-overruled dini yetu kwa tohara ya wasichana. Napendekza wasichana watahiriwe. Na wakaazi wa Sala location walimalizia wakisema civic wards kutoka kwao wakiwa wako mbali na Madogo Division twenty five kilometers waregeshewe kwa sababu kuwekwa chini ya Madogo na Mororo wamenyimwa haki yao. Asante Bwana Commissioner.

**Com. Zein:** Kijana, kijana.

**Sala Salat:** Thank you Mr. Commissioner, mimi kwa jina naitwa Salah Salat, Salah Salat.

**Interjection:** Nani?

**Salah Salat:** Salah Salat. My opinion, Suspending or expelling students from school without a proper reason by the headteacher should be scrapped. There should be free education from Standard One upto Standard Eight. Thank you.

**Com. Zein.** Salah, uende ujiandikishe pale, tafadhali. Unaona Salah amefanya mambo yake amemaliza, amempa mtu mwingine fursa. Taja jina ufanye mambo yako umalize.

**Isaac Abadela:** Mimi kwa jina naitwa Isaac Abadela. Isaac Abadela. Ningependa kutoa maoni kuhusu kuzoroteka kwa hali ya usalama humu nchini.

**Com. Zein:** Endelea bwana

**Isaac Abadela.** Tungependa sana sisi wakaazi wa Tana River, Serikali iangalie maisha ya wananchi wake haswa kwamba kuna wakati mwingine kulikuwa na clashes na kunayo baadhi ya watu ambayo wamepoteza maisha yao. Serikali ya Kenya hakuna chochote ambacho imefanyia ama imehudumia ama kuwalipa wale ambayo wamefariki.

**Com. Zein:** Isaack unapendekeza nini?

**Isaac Abadela:** Napendekeza Serikali iwalipe wale ambao wamepoteza maisha yao.

**Com. Zein:** Sawa, endelea.

**Isaac Abadela:** Ya pili ni kwamba tunaomba tujengewe special schools za disabled kwa sababu sehemu hii tunayo walemavu wengi wasiojiweza na hawa walemavu hakuna mmoja wao ambaye anasoma. Hii ni kutokana na hali ya kwamba shule ndiyo, ile shule za disabled schools.

**Com. Zein:** Ngoja kidogo. Naomba watu walioko hapo nje wawache kupiga kelele tafadhali. Watu walioko hapo nje wawache kupiga kelele. Endelea sasa.

**Isaac Abadela:** So, naomba Serikali itujengee shule za disabled. Ndiyo. Basi maoni yangu ndio hayo tu.

**Com. Zein:** Asante sana. Nenda pale uandikishe kwamba umetoa maoni kwa Tume ya Kurekebisha Katiba. Mzee tafadhali kaa na utaje jina lako na uendelee.

**Haron Saparo:** Haya mimi naitwa Haron Sapalo,

**Com: Zein:** Nani?

**Haron Saparo:** Haron Saparo. Yes sir. Waliotangulia walikuwa wameongea mengi sana kitu nilitaka kusema pia ishaongewa.

**Com. Zein:** Sawa

**Haron Saparo:** Lakini kitu ambacho nasisitiza sana ni kuhusu boundary, mpaka. Huu mpaka tuliambiwa ni maili tatu Garissa, na sasa mpaka saa hii naona tunasonga tu tumefika mwisho wa mpaka wa mto Tana. Hata huu mto wamevuka mpaka hata bridge yao wamesimamisha hapo askari kutoka North Eastern walikuja wakakaa hapo mwisho. Kwa hivyo inaonyesha hatuna kitu. Je ikiwa mkoloni aliweka yaani maili tatu huko na saa hii sisi tunataka tuoneshwe sehemu zetu, mpaka wetu ambao tuliwekewa na mkoloni. Kwa hivyo sina mengi ya kusema.

**Com. Zein:** Asante sana.

**Ramadhan Divayu Babisan:** Kwa jina naitwa Ramadhan Divayu Babisan. Maoni yangu ya kwanza ni kuhusu mpaka. Kuhusu mpaka sitazungumzia zaidi. Mpaka ni ubaki vile vile usibadilishwe. Halafu, hawa watu wa North Eastern Province, town zao especially district headquarters na division zimejengwa katika area yetu, halafu inaonyesha hawaelewi tofauti ya kujenga ofisi zao katika area zetu. Kwa hivyo naomba Katiba ieleze wazi wazi. Kutulinda sisi watu waelewe tofauti ya kusaidiwa mahali p kujenga headquarters zao. Mfano, Ijara. jara district ilipoundwa, walipoambiwa wajenge district headquarter hapo Masalani walianza kufukuza wenyenji hapo wanataka mashamba pia. Kwa hivyo tunaomba Katiba hii mpya ieleze wazi wazi kuwa hiyo area wakipewa katika Tana River district kwa sababu hii iko karibu na maji wajue mpaka wao ni upi wasije wakasumbuwana na sisi wenyeji.



Maoni ya pili ni kuhusu kupunguza wafanyai kazi wa Serikali, retrenchment. Kunzia Kenya ianze tumekuta kuwa kuna tatizo. Makabila mengine ni wengi zaidi katika Civil Service kuliko makabila mengine. Natunajua bado kuna idadi kadha itapunguzwa.

Kwa o kitu ninaomba katika Katiba hii mpya wale wanfanyakazi wa Serikali watakao punguzwa, lazima kwanza iwe studied ile namba kulingamana na ma-abila, wale ma-bila wengi wapunguze angalao tupate balance, kuliko iiendelee kupunguza wale wachache hiilance iiendelee.

Maoni yangu ya tatu ni kuhusu ufadhili unaoingia nchini. Wengi tunaelewa hali ya inchi vile ilivyo, lakini hivyo hivyo inaonekana bado ule ufadhili kidogo unaotokea hauendi kisawa. Maoni yangu ni kuwa, ufadhili ukiingia lazima iangaliwe nchi nzima ile dharura iliyoko ndiyo isaidiwe. Kwa mfano Tana River District, miradi yetu yote imeanguka, schemes, maisha ni magumu, lakini utakuta district zingine one hundred million, two billion, three billion zinasaidiwa na Tana River District tunaumia. Katiba mpya ni ionyeshe wazi wazi, misaada ikiingia hata kama ni michache igawike ki sawa.

Maoni yangu ya nne ni kuhusu mwanzilishi wa vita vya kikabila, inciter of civil clashes. Inasikitisha sana wakati wa civil clashes unaweza kushuhudia mtu anauwa baada ya siku mbili ameachiwa. Ambapo hiyo ina-incite yule ambaye hajauwa pia anaona kumbe nikiua nitaachiwa. Lazima sheria iundwe iwe ngumu kabisa, yule mwenye kuanzisha clashes awe na adhabu kali kabisa.

Maoni yangu ya tano ni kuhusu uwezo wa Rais kuteuwa hawa wakubwa katika Serikali, mfano mabalozi, chairman wa vile tourism, chairman wa railway na ma shirika mengine. Unakuta kuwa watu waki-retire wakubwa wa kubwa kwa mfano Commissioners, CGS, Majorss baada ya ku-retire bado wanapewa vyeo kama hivyo. Tukiangalia kuna watu wengine wanastahili wapewe vyeo kama hivyo. Kwa hivyo tunaomba Katiba mpya ieleze sawa sawa, vyeo kama hivyo viangaliwe wale ambao pia wanaweza wakajisaidia.

Ya sita ni, naomba Katiba mpya itusaidie. Katika Tana River District tuko na matatizo sana, tuko na yatima wengi. Serikali ihakikishe kuwa Tana River District kila division tujengewe Children's Home ya mayatima ili itusaidie maanake wafadhili wametusaidia ya kutosha.

**Com. Zein:** Sawa, fupisha sasa Ramadhan.

**Ramadhan:** Inginge nitazungumzia kuhusu Kenya Power & Lighting. Kenya Power & Lighting dams nyingi zinatoka Tana River District. Katiba mpya iundwe kuwa ile faida inatokea katika Power & Lighting kila mwaka itengwe pesa fulani za kutusaidia watu wa Tana River. Kwa kumaliza ya mwisho, kuhusu mishahara ya wabunge, imedhihirika kuwa wabunge wote si upinzani, si Kanu, wanajipendelea. Katika mamlaka ya mishahara ya wabunge iundwe kamati kama vile watu wa ma kanisa, mashirika ya wanawake, mashirika ya vijana wawe watajadili mishahara ya wabunge, isiwe wao wenyewe. Asante.

**Com. Zein:** Thank you haya nenda pale uandike jina lako kwamba umetoa maoni kwa Tume. Anayefuatia? Endelea. Ni

wewe ndiwe ulikuwa na sauti ya kusema? Haya, kuna mtu yeyote ambaye hajazungumza sasa anataka kupewa fursa ya kuzungumza? Keti Mzee, keti, lakini kabla haujaanza nataka kujua, kuna mtu mwingine yeyote ambaye alikuwa anataka apewe fursa ya kusema na hajapata fursa hiyo? Kwa hivyo mzee ndiye atakuwa mtu wa mwisho, asante Mzee, endelea.

**Ali Abajila Awacho:** Asante sana, asante sana mimi kwa jina Ali Abajila Awacho, Madogo location. Kwa jina Ali Abajila Awacho, kwa jina. Basi sasa kwa maoni yangu ni kidogo sana sitaki maneno mengi, kidogo tu. Sasa sisi watu wa Tana River, kweli watu tano ndio kabila walikuwa wanakaa hapa nchi. Sasa inasemekana wanaongezeka kuwa watu sita. Katika watu sita wanakaa hii Tana River, sisi ardhi yetu ilikuwa iko hasara mara mbili, walikuwa wanakata huko Kora Game Reserve, na ingine wanakata huko pande ya Malindi kwa kuwa iko National Park ingine. Sasa maoni ya watu wetu, jirani zetu mandugu zetu tu nakaa Tana River pamoja, kama kabila kama Pokomo na Orma alikuwa shida juzi jiyokea alikuwa anataka agawe ardhi pahali mbili mpaka na watu wametoa. Na sisi hatutaki kwa maoni yangu sasa ile Tume hii sitaki ardhi tugawe ile kabila sisi tunazaliwa pamoja hapa Tana River ile tukae pamoja.

Na ingine yangu ya tatu, ile Tana River Madogo, Madogo ipate soko mzuri kama Bangale. Ile soko hiyo, siyo mifugo peke yake, hata kama ni kuni, hata kama ni makaa ile kila mtu ni sokoni na tajiri wachukuwe achukuwe mali ingine. Ile mambo watu wa North Eastern wana kuja kupatia ile kuni ipelekwe huko Garissa. Hiyo fursa hiyo ilikuwa shida sana, achukuwe, kwetu ile soko hapa. Sipati soko. Wengine watu kama Mbalambala dispensary inajengwa, hakuna watu wa usalama askari nakaa huko, sasa hiyo dispensary ipate watu wa msaada askari wapelekwe huko na wakae kama watu wengine. Watoto wapate shule, iko shule mbili huko Roga na huko Mbalambala hakuna yoyote, ile shule bado ... karibu miaka minne. Sasa yangu ya mwisho hapa, asanteni sana.

**Com. Zein:** Asante sana Mzee. Omar nafikiri yeye ndiye alikuwa Mzee mtu wa mwisho nameuliza hakuna mtu mwingine anataka kutoa maoni. Sasa ningependa kukuomba, utufungie mkutano Mimi ningependa kusema ya kwamba kikao hiki kimefikia ukingoni na ningemuomba Professor kama ana maneno machache aseme, halafu nirudi kwa Omar Dhadho, tufunge mkutano mupate kitu kidogo alichosema Dhadho cha kushika tumbo kabla watu hawajaenda mahali mbali.

Professor hana la kusema, sisi ni kuwashukuru sana kwa maoni yote mliyotoa. Mzee mmoja aliuliza swali kwamba sijui maoni haya mtafanyia nini? Kama tulivyosema mwanzo kwamba maoni haya tutayatumia pamoja na maoni ya Wakenya wengine wa nchi nzima, kama misingi ya kugeuza Katiba yetu. Na tutatoa ripoti, itarudi kwenu muone kama maoni mliyotoa yamo katika repoti hiyo. Ningependa kuwa shukuru sana, wale wanakamati kama alivyosema Bwana Omar Dhadho kwamba wamekuwa na shida nyingi na kamati mara inaanzishwa mara inatoka lakini, kama hivo hivo kazi kubwa imefanyika mpaka watu wengi wameweza kufika leo na kutoa maoni yao na tulisikia Bura chini watu walitoa maoni yao hivyo. Na hilo ni swali kujibu pia Mzee alisema mko hapa peke yake au mtakuweko tena. Sisi ndiyo tumefunga kazi hapa, lakini kabla yetu kulikuwa kuna mkutano Bura, na watu wakatoa maoni yao pia kule Bura kuhusu marekekebisho ya Katiba. Katika kila sehemu ya wakilishaji bungeni, tunakaa katika vikao viwili. Asanteni sana ningemuomba Bwana Dhadho atoe maoni ya mwisho, na kumuomba mtu

atufanyie dua halafu tuombe Mungu twendeni tunavokwenda. Asanteni sana.

**Omar Thatu:** Asante sana, Prof. Okoth-Ogendo, Bishop Bernard Njoroge, Commissioner Abubakar Zein, Chairman Tana River County Council Salat Garacha, ma-councillor wengine, Provincial Administration representatives, viongozi wa tabaka mbalimbali, mabibi na mabwana. Nafikiri tumefika ukingoni mwa shughuli zetu za leo hapa. Ningependa kwa niaba ya wakaazi wa sehemu hii ya Madogo, Mororo, Bangale, na Location ya North Tana, kutoa shukran kubwa kwa Commissioners ambao wamekuwa wavumilivu, tangu asubuhi wameketi wakisikiza maoni yetu. Na ningependa pia kuwashukuru wananchi, haswa wale ambao wametoka sehemu za mbali, kwa ajili ya kuja kwa huu mkutano. Na yale maoni ambayo mmetoa kama vile tulivyohakikishiwa, si kwamba tumeyatupa kwenye ombe tupu, bali yamehifadhiwa kwa njia mbalimbali na yatashugulikiwa namna yatakavyo shugulikiwa maoni ya watu wengine.

Na nisingependa kuchukua muda mrefu kurefusha mkutano, maana mkutano umeisha ila kutoa shukrani kwa kila mmoja wenu ambaye amefanya mkutano wetu wa leo uwe wakufana na pia kumkumbuka Chairman wetu wa Tana River County Council. Mengi yaliyosemwa kwa bahati nzuri yametajwa naye yuko hapa I am sure pia ame-take note yale ambayo mlikuwa munaambia Tume maana mengine yanamhusu yeye.

Kwa hivyo natoa shukrani kwa kila mmoja wenu na kusema tutafunga mkutano kwa njia ya maombi, na kawaida yetu tukianza na maombi ya Kiislamu tunakuwa democratic, tunafunga na maombi ya Kikristo, ili kila mmoja asikie ameomba kwa njia ambavyo kwamba hakuoneka kama hahesabiwi kwamba yuko. Kwa hivyo nitamwita Josiah Githinji, wa kanisa la ACK ambalo ndilo limetoa madawati haya mnayaona hapa aje atufungie kwa njia ya maombi. Kkutoka kwangu nasema asanteni sana na Mwenyezi Mungu awabariki, shukrani.

**Josiah Githinji:** Na tufunge macho tuombe, Bwana katika jina la Yesu Kristo tunakushukuru kwa ajili ya kikao ambacho umetupa. Yunakushukuru Bwana kwa wageni ambao tumekuwa nao wa Tume hii ya Katiba. Tunakushukuru Bwana kwa vile maoni yametolewa ya mbalimbali, na Bwana utaishughulikia bwana, tunakubariki kwa ajili ya vile tumekaa kutoka mwanzo na kutoka mwisho, natunaomba Bana hata akati tunapo achana sasa baraka zako ziendanishwe na kila mmoja na uweze kujifungulia kwa kila mmoja ili aweze kukujua wewe Mungu Baba. Tunaomba haya machache tukiamini katika jina la Yesu Kristo ewe Bwana na Mwokozi wetu. Amen.

..... **THE END**.....